BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Sita –Tarehe 20 Juni, 2016

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI: Maswali.

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa Mbunge wa Chunya, sasa aulize swali lake.

Na. 389

Tatizo la Ukosefu wa Chumba cha Kuhifadhia Maiti

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Kituo cha Afya Chunya kilipandishwa hadhi kuwa hospitali ya Wilaya mwaka 2008 lakini kuna tatizo la ukosefu wa chumba cha kuhifadhia maiti:-

Je, ni lini Serikali italitatua tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Chunya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tayari imeanza mchakato wa ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali ya Wilaya ya Chunya ambacho kinatarajiwa kugharimu shilingi milioni 230 hadi kukamilika. Ujenzi wa jengo utagharimu shilingi milioni 60 na majokofu yatagharimu shilingi milioni 160. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti yaani *mortuary*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hospitali ya Wilaya ya Chunya kwa sasa kipo chumba maalumu ambacho kimetengwa kikiwa na uwezo wa kuhifadhia maiti mbili tu. Chumba hicho hakitoshelezi huduma hiyo hali ambayo inawalazimu wananchi kufuata huduma ya aina hiyo katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Mbeya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Victor Mwambalaswa swali la nyongeza!

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri amesema mwaka huu Serikali imetenga shilingi milioni 50. Hizi hela ni hela za Halmashauri, *own source* ya Halmashauri na mimi Mbunge nitachangia katika hela hizo. Mimi ninalosema Serikali kutoka Makao Makuu iwe Wizara ya Afya au TAMISEMI watachangia kiasi gani kwenye hospitali hiyo ambayo ni ya wananchi wa Wilaya ya Chunya hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Bunge lililopita la Kumi Serikali ilianzisha mpango wa kukarabati hospitali za Wilaya kumi, kuziinua kiwango ziweze kutibu maradhi yote ili kupunguza *congestion* kwenye hospitali ya rufaa na Chunya ilikuwa mojawapo katika hospitali hizo kumi katika Tanzania.

Je, huo mpango umefia wapi? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli safari hii imetengwa shilingi milioni 50 na tunapofanya *mobilization of resources* mara nyingi sana kuna vipaumbele, najua wazi kwamba pesa hizi ni *own source*. Lakini siyo kusema kwamba kwa vile ni *own source* basi Serikali maana yake haina jicho lake ndiyo maana mchakato wa bajeti kuna pesa nyingine zinatoka katika Serikali za Mitaa na nyingine zinatoka katika Serikali Kuu. Wakati mwingine kipaumbele cha baadhi ya vipengele inaenda katika miradi mingine. Kwa hiyo, lengo kubwa ni Serikali kupeleka mchakato huo mpana na mwisho wa siku ni kwamba wananchi kuweza kupata huduma.

Mheshimiwa Mwambalaswa naomba nikuhakikishie kwamba hela hii ni *own source* na ninajua kwamba na ninyi mmefanya harakati na wewe mwenyewe ulikuwa ukisimamia ile harakati ya harambee. Mimi naomba niwapongeze kwa sababu miongoni mwa watu ambao wamefanya wenyewe kuhakikisha kwamba wanafanya harambee tena ikiongezewa na Mbunge Mwambalaswa nikupongeze katika hilo. Naomba nikuhakikishie kwamba katika mchakato wetu najua hii itakapokuwa imekamilika lazima kutakuwa na mapungufu mengine yatakuwa yanajitokeza katika kuhakikisha hospitali ile inaweze kufanya kazi. Jukumu la Serikali mwisho wa siku ni kwamba hospitali ile ya Chunya iweze kuwa na hadhi sasa kama nyingine, naomba nikuhakikishie kwamba tutakuunga mkono kwa nguvu zote kwa vile umekuwa ukipigania katika hili tutashirikiana kwa jinsi zote.

Suala zima la ukarabati kama ulivyosema kulikuwa na mchakato wa ukarabati ni kweli, na maeneo mbalimbali ukarabati huu ulikuwa unaendelea. Lakini bado tukiri wazi tatizo hili bado ni kubwa sana ukiachia ukarabati; hata niliposema wiki iliyopita, kwamba ukiacha ukarabati halikadhalika kuna majengo mengine ambayo hayajakamilika. Ndiyo maana tumetoa maelekezo wiki iliyopita nimesema Halmashauri zote hata Mheshimiwa Mwambalaswa tulikuuliza kule Chunya kuwa Mkurugenzi atakuwa amepata waraka kutoka TAMISEMI, lengo letu ni nini, najua kuna mambo tumeyafanya lakini bado mapungufu yapo makubwa zaidi, tuweze kubainisha hizo changamoto tuzipangie mkakati wa pamoja sasa jinsi gani tutafanya kurekebisha matatizo haya hasa ya magofu ambayo hayajakamilika lakini kuhakikisha hadhi za hospitali zetu za zahanati ziwe sawa sawa. Nadhani mchakato huu utakuwa mpana sana ili kukidhi matakwa ya ilani ya Chama Cha Mapinduzi kama tulivyoahidi wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuahidi Mheshimiwa Mwambalaswa kwamba tutakuunga mkono katika juhudi kubwa ulizozifanya katika Jimbo lako la Chunya na Halmashauri yako ya Chunya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Keissy!

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nkasi leo ina miaka 40 tangu ilipoanzishwa, lakini haina hospitali ya Wilaya, wala Serikali haina mpango wa kujenga hospitali ya Wilaya. Ni lini Serikali yetu itakuwa na azimio la kujenga hospitali ya Wilaya hasa katika Makao Makuu ya Wilaya katika Mji wetu wa Namanyere?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninamfahamu Mheshimiwa Keissy kuhusu suala la

tatizo la afya. Miongoni mwa mambo ambayo ninayakumbuka Mheshimiwa Keissy alipendekeza kituo kimoja kile cha afya kukipandisha *grade* kuwa hospitali ya Wilaya kama sikosei. Alizungumza hapa Bungeni kwamba kituo kile cha afya licha ya kuwahudumia wananchi wa Jimbo lake, wengine wanatoka katika nchi mpaka ya Congo. Hili nilisema siku ile kwamba Mheshimiwa Keissy jambo hili tumelichukua, katika mpango wa pili wa afya kila Halmashauri kuwa na hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Keissy naomba niseme tu kwamba tutaungana pamoja katika mipango kwa sababu tunajua Wilaya yako ipo pembezoni na ina changamoto nyingi. Tutajitahidi kwanza kuhakikisha kile kituo cha afya tunakiangalia na mimi nimekiri wazi kwamba nikija kwako lazima nikitembelee kituo cha afya, tutashawishi wenzetu wa Wizara ya Afya wakiangalie kama kimefikia vigezo kipandishwe kuwa hospitali ya Wilaya, tutakuunga mkono ili wananchi wa eneo lako lazima wapate afya. Jambo hili umelipigia kelele sana toka Waziri Mkuu wa mwanzo Mheshimiwa Peter Pinda nilikusikia ukilizungumza, nasema kwamba tupo pamoja katika hili.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mary Mwanjelwa!

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona na mimi naomba niulize swali moja tu dogo la nyongeza;

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya hii ya Chunya ni mojawapo ya Wilaya kongwe sana Tanzania, lakini hospitali hii haina vifaa tiba wala matibabu ni kweli. Pia akina mama kwenye wodi ya wazazi wanapata shida mpaka wanajifungulia chini, naomba kujua Serikali ina mkakati gani kuiangalia jicho la ziada Wilaya hii kongwe nchini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya vifaa tiba na siyo vifaa tiba tu maana yake kuna changamoto nyingi, ukienda kwenye vifaa tiba utakuta changamoto ya madawa, ndiyo maana katika mpango wetu wa sasa ninawashukuru sana wenzetu wa Wizara ya Afya ukiangalia mpango mkubwa tunaondoka nao, suala zima la vifaa tiba, madawa katika bajeti ya mwaka huu imeji-*reflect* kabisa ni jinsi gani tutafanya hasa hospitali zetu za Wilaya ziweze kuwezeshwa. Maelekezo makubwa tumeona hospitali nyingi sana mara nyingi zinasuasua katika suala la madawa na vifaa tiba na ndiyo maana mpango wetu mkakati sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunafanya *collection* ya kutosha, mara nyingi pesa zilikuwa zinakusanywa lakini siyo zile zinakusanywa zinaingia katika Halmashauri na hospitali, nyingi zilikuwa zinapotea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tumeasisi hii mifumo ya ki-*electronic,* hata mwanzo pesa zikikusanywa zilikuwa hazitumiki zote kwa

matumizi ya hospitali, mengine watu walikuwa wanatumia kwa ajili ya kulipana *per diem* mwisho wa siku ni kwamba hata dawa na vifaa tiba vinakosekana. Kwa hiyo kutokana na mwongozo tumesema kwamba pesa zote zinazokusanywa katika hospitali za Wilaya ukiachia na mafungu mengine, lengo letu kubwa kwamba hii mifumo ya *electronic* tutakusanya fedha lakini lazima mwongozo ufuatwe. Je, asilimia ngapi inaenda katika vifaa tiba na asilimia ngapi inaenda katika dawa, mwisho wa siku tuweze kutatua tatizo la dawa na vifaa tiba katika hospitali zetu.

Hili Mheshimiwa Mwanjelwa tutaenda kulisimamia katika mwaka huu wa fedha ili kuongeze ufanisi katika hospitali zetu za Wilaya na hospitali zetu mbalimbali wananchi waweze kupata huduma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje!

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nina swali dogo la nyongeza;

Kwa kuwa, wananchi wa Kijiji cha Majami, Kibolianana, Mlembule na Mgoma tayari wameshaonesha juhudi ya kujenga majengo ya zahanati, kilichobaki ni Serikali kusadia. Lakini Igodi Kusini, Isalanza jengo lipo tayari limekamilika pamoja na Igodi Kaskazini.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri utakuwa tayari kuwapelekea watu wa Igoji Kaskazini na Kusini huduma ya madawa na kusaidia hawa ambao tayari wameonesha nguvu za kujenga zahanati?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kilio hiki na bahati nzuri Mheshimiwa Lubeleje kama ukifanya *reference* mwenyewe hili ni miongoni mwa maswali mengi sana aliyouliza katika sekta ya afya, Mheshimiwa Lubeleje nikuhakikishie kwamba katika eneo hilo kwanza ahadi zetu zile za kwanza ni lazima tutazitembelea zahanati hizi kuziangalia kama kuna changamoto tuweze kuzitatua; hali kadhalika tutafanya utaratibu jinsi ya upatikanaji wa dawa, kwa sababu nikijia Jimbo lako ni kubwa, maeneo yako ni makubwa. Nimefika katika sehemu wanaita Makutupa, kutoka Makutupa mpaka mtu anaenda kufuata huduma ya afya ni mbali sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Lubeleje juhudi unayoenda kufanya endelea kuifanya, tutaunga mkono lakini lazima tu-*visit* tuangalie kama kuna changamoto nyingine tuweze kurekebisha, tuwaambie wataalamu wetu tuweze kufanya hata *allocation* ya wataalamu wa ndani na madawa tutafanya ili vituo hivi viweze kufanya kazi na wananchi waweze kupata huduma.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abood Mbunge wa Morogoro Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 390

Msongamano Mkubwa kwenye Wodi za Akina Mama Hospitali ya Rufaa Morogoro

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD aliuliza:-

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro ina tatizo kubwa la msongamano katika wodi ya akina mama ambao wamekuwa wakilala zaidi ya wawili kwenye kitanda kimoja;

(a) Je, ni lini Serikali itaongeza wodi ya wazazi katika hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Morogoro?

(b) Je, kwa nini Serikali isiboreshe baadhi ya zahanati kama Mafiga Sabasaba ili kuwa na uwezo wa kupokea kina mama wajawazito kujifungua na kupunguza msongamano katika hospitali ya rufaa ya Morogoro?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdul-Azizi Abood Mbunge wa Morogoro Mjini lenye sehemu a na b kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, msongamano wa wagonjwa katika wodi ya wazazi ya hospitali ya Mkoa unatokana na kukosekana kwa hospitali ya Wilaya ya Morogoro. Ili kukabiliana na tatizo hilo Serikali imepanga kuanza ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Morogoro katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Fedha zilizotengwa ni shilingi bilioni 2.5 ili kuanza ujenzi wa jengo la utawala na jengo la wagonjwa wa nje *(OPD)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuimarisha kituo cha afya cha Mafiga ambacho tayari kimeanza kutoa huduma za mama wajawazito. Katika mwaka wa fedha 2015/2016 Halmashauri imepanga kutumia shilingi milioni 100 kwa ajili ya kujenga jengo la upasuaji na wodi. Vilevile, zimetengwa shilingi milioni 71 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa ajili ya upanuzi wa wodi ya wazazi katika zahanati ya kihonda. Hivyo, mpango wa Serikali ni kuimarisha huduma za wazazi katika zahanati na vituo vya afya ili kupunguza msongamano katika hospitali ya rufaa ya Morogoro.

MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD: Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza;

Swali la kwanza, zahanati ya Mafiga inahudumia kina mama wengi lakini haina madawa kwa ajili ya akina mama na pia haina *ultra sound machine* ya akina mama.

Je, lini Serikali itaipatia zahanati ya Mafiga vifaa hivi?

Swali la pili, hospitali ya Mkoa wa Morogoro ambayo ipo njia panda ya barabara ya Morogoro inayokwenda Mikoa mingine yote ya Bara na ajali nyingi zinatokea, lakini haina mashine ya *X-Ray*, mashine iliyopo sasa hivi haifanyi kazi vizuri.

Je, Serikali haioni kama kuna uharaka wa kuipatia hospitali ya Mkoa wa Morogoro mashine ya *X-Ray*?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yangu ambayo nimetembelea ni Morogoro, na jambo ambalo nimeshuhudia pale ni kwamba kama Mheshimiwa Mbunge pale kwa kweli kwa kutumia, licha ya ushawishi wakati mwingine anatumia *resources* zake mwenyewe kwa ajili ya wananchi wake. Naomba nikuhakikishe kwamba katika hii zahanati ya Mafiga uliyoisema ambayo changamoto kubwa ni madawa pamoja na vifaa tiba *especially ultra sound* na nimesema katika maelezo yangu ya awali. Katika *research* tuliyofanya haraka haraka vitu vingine vingekuwa vinaweze kupatikana kwa ukaribu sana lakini tatizo kubwa tulilokuwa nalo mwanzo ni kutokana na ile *management* ya fedha zilizokuwa zinapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia idadi ya wanaofika katika zahanati ya Mafiga pale lakini *collection* ilikuwa ni changamoto kubwa sana. Ndiyo maana tulitoa maelekezo ya kutosha licha ya kufanya juhudi zingine za upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, changamoto kubwa ni kwamba tukienda kukusanya mapato yetu vizuri ambayo katika njia moja au nyingine unakuta kwamba baada ya kutumia mifumo ya *electronic, collection* imeenda zaidi ya asilimia 800. Watu waliokuwa wanakusanya shilingi laki moja leo wanakusanya shilingi milioni moja, unaona kwamba jinsi gani pesa hizi zikikusanywa vizuri zitaenda kusaidia katika suala zima la madawa na vifaa tiba.

Kwa hiyo Mheshimiwa Abood naomba nikuambie ninakuhakikishia kabisa kwamba katika zahanati ya Mafiga mimi na wewe kwa sababu tumeshaahidi kwamba tutaenda Morogoro, hii ni sehemu ya kwanza kwenda kubaini kuwa tatizo la msingi ni nini, na tutafanyaje kuondoa tatizo la madawa, kwa sababu mwanzo watu hata mwongozo walikuwa hawaufuati, pesa hata zikikusanywa

haziendi katika madawa na vifaa tiba, isipokuwa watu wanagawanya kwa *per diem* na vikao vingine visivyokuwa na maana yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nimhakikishie Mheshimiwa Abood kwamba, hapa tutafanya ukatabati mkubwa ili utendaji wa zahanati hii na nyinginezo zinafanya kazi vizuri kwa ajili ya wananchi wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la hospitali ya Morogoro ni kweli na mimi nikuambie kwamba miongoni mwa *field practical* zangu wakati nilipokuwa Chuo Kikuu mwaka 1998, nilifanya *research* zangu pale na *field practical* nilifanyia pale Morogoro, naifahamu vizuri hospitali ya Mkoa wa Morogoro. Ni kweli inapokea wagonjwa wengi sana na wakati mwingine hata ajali zikitokea watu wengi ni sehemu ya kimbilio, wanaotoka Iringa, Dodoma na sehemu mbalimbali pale ni kimbilio. Tunajua *X-Ray machine* ipo lakini haifanyi kazi vuziri, tuna mpango mpana sasa hivi wa Serikali hasa kwa ajili ya hospitali zetu za Mikoa na hospitali zetu za Kanda. Mpango huo sasa kwa Serikali ya Tanzania kwa kushirikana na Serikali ya Uholanzi tutahakikisha kwamba tunapeleka vifaa tiba katika hospitali zetu za Kanda na hospitali za Mkoa. Ninaamini na hospitali yetu ya Mkoa wa Morogoro tutaipa kipaumbele kutokana na *strategic area* yake ya kijiografia, lazima tuipe nguvu wananchi wa Morogoro waweze kupata huduma, ili wanufaike na huduma njema ya Serikali yao ya Awamu ya Tano ambayo inafanya kazi kwa maslahi ya Watanzania.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya!

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, kuhusu suala la uhaba wa dawa katika vituo vyetu vya afya, ningependa kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba tunapitia upya vigezo vya kugawa fedha za dawa. Kwa sababu kwa kweli tumeona hakuna uwazi, unakuta kituo kingine kina wananchi wengi lakini mgao wa dawa fedha ya dawa ni ndogo. Kwa hiyo, nataka kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge tunaangalia upya vigezo kama ni hospitali ya Mkoa wanatakiwa kupata shilingi ngapi na taarifa hizi tutazitoa kwa kila Mbunge ajue kituo chake cha afya kinapata shilingi ngapi, hospitali yake ya Wilaya inapata shilingi ngapi na hospitali ya Mkoa inapata shilingi ngapi. Kwa hiyo, tunataka kuwa wawazi zaidi katika mgao wa fedha za dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Mawaziri, mtusaidie mnaona watu wengi wanasimama majibu yawe mafupi tafadhali. Kwa sababu watu wanasimama hawapewi nafasi ya kuuliza maswali, kwa sababu wanapewa majibu marefu

halafu hayo majibu marefu wao wanaona maeneo yao hayajajibiwa na hayo majibu, kwa hiyo inaleta tabu kidogo. *(Makofi)*

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona.

Katika Hospitali yetu ya Wilaya ya Geita ambayo imepandishwa hadhi kuwa hospitali ya Mkoa kuna msongamano mkubwa sana wa watu kiasi kwamba kwa kweli changamoto ni kubwa sana. Ningependa hasa kujua kwa sababu tunatakiwa tujengewe Hospitali mpya ya Rufaa ya Mkoa.

Ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi rasmi katika hospitali ya Mkoa ambayo itakuwa ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Geita? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Mheshimiwa Bukwimba tulikuwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais tulifungua hospitali ile ya Geita, kweli kuna msongamano mkubwa, na pale ni kipaumbele, nadhani mchakato wa Serikali tutafanya mambo haya kwa haraka kuangalia bajeti ya mwaka wa fedha unaokuja, tuweke mipango ya pamoja ya Kiwilaya na Kimkoa na mwisho wa siku tujenge hospitali yetu ya rufaa ya Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Na. 391

Ukosefu wa Shule za Kidato cha Tano na Sita Nzega

MHE. HUSSEIN M. BASHE aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Nzega haina shule hata moja ya kidato cha tano na sita na hivyo kuwafanya wanafunzi wengi kulazimika kwenda kusoma nje ya Mji wa Nzega; lakini Mbunge kwa jitihada zake amejenga vyumba viwili pamoja na bweni katika shule ya sekondari Bulende kwa ajili ya kidato cha tano na sita.

(a) Je, Serikali ipo tayari kuanzisha masomo kwa kidato cha tano kuanzia mwaka huu wa 2016;

(b) Je, ni lini Serikali itajenga vyumba vya madarasa ya kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari Chief Itinginya ili angalau kuwe na shule mbili za kidato cha tano na sita?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mbunge wa Nzega Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri ya ukarabati wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya Sekondari ya Bulende, na sasa anaendelea na ujenzi na hosteli, Mheshimiwa hongera sana kwa kazi hii nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha shule ya Sekondari ya Bulende inapata sifa ya kuwa ya kidato cha tano, Serikali imetenga shilingi milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa bweni katika bajeti ya mwaka 2016/2017. Ili shule iweze kusajiliwa kuwa ya kidato cha tano na sita inapaswa kuwa na miundombinu ya kutosha kama vyumba vya madarasa, mabweni, samani, bwalo la chakula, vyoo pamoja na uwepo wa walimu wa masomo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri inapaswa kuwasilisha maombi ya usajili wa shule katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Ufundi ambao watatuma wataalam kukagua miundombinu ya shule kabla ya kutoa kibali. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha miundombinu ya kutosha inajengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi katika shule ya Sekondari ya Chief Itinginya ili kukidhi na kusajili kuwa ya kidato cha tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri imepanga kutenga bajeti katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya sekondari ya Chief Itinginya.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na *commitment* ya Serikali kutoa shilingi milioni 50 kwa ajili ya sekondari ya Bulunde na kutoa fedha kwa ajili ya sekondari ya Chief Itinginya. Nataka nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri swali dogo moja;

Kwa kuwa, jitihada za wananchi na Mbunge wa Jimbo la Nzega ni kumalizaS ya Bulunde ili tuwe na *high school,* na kwa kuwa, mahitaji ya fedha yaliyotengwa na Serikali kwa ajili ya shule ya Chief Itinginya hayatoweza kumaliza ujenzi wa shule ile kuwa na *high school* katika sekondari ya Chief ya Itinginya, mahitaji halisi ni shilingi milioni 250.

Je, Serikali iko tayari kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya Chief Itinginya, ili katika Halmashauri ya Mji wa Nzega tuwe na shule mbili za *A-level* ?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niseme wazi kwamba, Mheshimiwa Bashe kama nilivyosema pale mwanzo, ninajua una juhudi kubwa sana unaendelea kuifanya pale Nzega na umekuwa kila wakati ukija pale ofisini siyo kwa suala hilo tu, hata suala zima la kukuza uchumi wa maeneo yako ya vibanda pale, lengo ni kwamba mpate mapato muweze kuelekeza katika huduma za kijamii, kwa hiyo lazima tu-*recognize* juhudi kubwa unayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali kwa sababu mchakato wa bajeti wa mwaka huu umeshapita na bajeti ya mwakani tunaona ni jinsi gani tutafanya. Lengo ni kusukuma nguvu kuwasaidia watu wa Nzega. Ni kweli haiingii akilini eneo kama lile ambapo *population* ni kubwa, watoto wengi wanafaulu lakini wanakosa fursa ya kusoma.

Kwa hiyo, Serikali tutashirikiana nanyi kwa pamoja, Halmashauri na Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutaangalia jinsi gani tutafanya kuiboresha Nzega sasa iwe na thamani hiyo ya ukuaji wake wa Mji na Mji wa kihistoria tokea enzi za madini ya almasi, basi watu waone mwisho wa siku wananchi wa Nzega waweze kunufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba, juhudi ya Serikali tutakaa pamoja tutajadiliana nini kinatakiwa kifanyike na katika muda gani na kuangalia *resource* zilizokuwepo tuweze kusukuma watu wa Nzega waweze kupata fursa ya elimu.

MHE. KANGI A. N. LUGOLA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la kuanzisha shule za kidato cha tano katika nchi yetu linafanana kabisa na tatizo ambalo liko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, Halmashauri ambayo ni kongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna hata *high school* moja kwenye hiyo Halmashauri yetu ya Wilaya ya Bunda. Wananchi katika miaka mitano tumewahamasisha, tumejenga mabweni na mabwalo lakini tumeshindwa kukamilisha kwa sababu ya fedha na Serikali tumekuwa tukiitaka itusaidie.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari kuambatana na mimi na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ili twende kwenye Halmashauri yetu ukajionee juhudi za wananchi ili muweze kutusaidia?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kiufupi Mheshimiwa Kangi Lugola ndugu yangu nikuambie kwamba, mimi niko tayari kuambatana na wewe na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambaye ni jirani nyuma yangu hapa. Tutajitahidi tuende pamoja siyo kwa suala hilo la shule tu inawezekana tukabaini mambo mengi sana kwa ajili ya wananchi wa eneo hilo. *(Makofi)*

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Kwa kuwa, tatizo lililoko Halmashauri ya Nzega linafanana kabisa na Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, haina Sekondari ya kidato cha tano na sita. Kwa kuwa, Serikali ilitupa ukomo wa bajeti bilioni 14 na tumeshindwa, tumekatwa fedha nyingi za maendeleo.

Je, Ofisi ya Rais TAMISEMI, iko tayari kututafutia fedha kwenye vyanzo vingine ili tuweze kujenga sekondari ya kidato cha tano na sita katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Nsimbo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli najua kwamba, mwaka huu kulikuwa na suala zima la ukomo wa bajeti lakini ndiyo mwaka pekee ambao bajeti yake imevuka tumeenda karibuni kutoka bajeti ya maendeleo ya asilimia 27 mpaka asilimia 40, kwa hiyo kuna kazi kubwa imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa siwezi kusema kwamba, mwaka huu kuna fedha zingine zitaingia kwa sababu mchakato wa bajeti umeshapita. Lengo kubwa ni nini! Nina imani kwamba, katika mwaka mwingine wa fedha unaokuja hii itakuwa ni kipaumbele kwa sababu tunajua wazi kwamba, tumejenga shule nyingi za Kata vijana wengi wanafaulu. Kwa mfano, mwaka huu tuna vijana karibuni zaidi ya elfu tisini, lakini ukiangalia *capacity* yetu inaenda karibuni vijana zaidi ya elfu hamsini, maana yake inaonekana tuna tatizo kubwa sana la kuhakikisha tunaweka miundombinu kuwa-*accommodate* vijana wa *form five* na *form six*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Richard Mbogo katika mchakato wa bajeti wa mwakani tuweze kuliangalia kwa pamoja zaidi. Hata ikiwezekana kwa sababu mambo haya tumesema kwamba, hata shule zingine za Kata ambazo ziko vizuri tunaweza tukazi-*upgrade* zile baadhi ya shule kuziongezea miundombinu kuweza kuwa shule za *form five* na *form six*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyo katika mwaka wa fedha unaokuja tutaangalia kwa pamoja ni jinsi gani tutatanya Nsimbo tupate *high school* moja kwa ajili ya vijana wetu.

MHE. OMARY T. MGUMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, matatizo yaliyopo Nzega yanafanana kabisa na Halmashauri ya Morogoro hatuna *high school* hata moja katika Halmashauri yetu ya Morogoro Vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kutusaidia ambao ukizingatia juhudi za wananchi tumejitahidi tumejenga ile Sekondari ya Nelson Mandela. Je, Serikali ina mpango gani wa kutuongezea nguvu ili kuimalizie shule ile angalau Halmashauri hii iwe na shule hata moja ya sekondari?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nilifika kwa Mheshimiwa Mbunge, ukitoka pale Morogoro Mjini pale kwa mfano unatoka Ngerengere pale, ukienda mpaka kule mwisho unaenda Kidunda halafu mpaka kule mbali zaidi wananchi wanapata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mtoto akitoka pale maana yake changamoto yake ni kubwa. Ni vizuri zaidi tungepata shule moja ya *form five* pale, kwa hiyo naomba nikuambie kwa mwaka huu kwa sababu bajeti imeshapita, imani yangu ni kwamba kwa mwaka wa fedha unaokuja 2017/2018 anzeni kuweka maoteo ya bajeti zenu katika Halmashauri, *then* na sisi huko Ofisi ya Rais TAMISEMI tutaona hicho ni kipaumbele kikubwa ili eneo lile sasa la Mandela tuweze kupata shule ya *form five* na *form six* angalau tupate *high school* moja katika maeneo hayo na Wizara ya Elimu ikija ikiona kwamba, vigezo vimefikiwa basi shule ile itapandishwa kuwa ya *form five* na *form six.*

Mheshimiwa Mbunge, naomba nikupongeze kwa juhudi kubwa tutashirikiana kwa pamoja, naomba lianze hilo wazo kwenu *then* Ofisi ya Rais TAMISEMI katika mchakato wa bajeti itaona siyo mbaya sasa kuipa kipaumbele eneo hili kupata shule ya *form five* na *form six* kwa ajili ya vijana wetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Wizara ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo, Mbunge wa Karatu, swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Flatei Massay.

Na. 392

Hitaji la Huduma ya Umeme Kata ya Quvui

MHE. FLATEI G. MASSAY (K.n.y MHE. WILLY Q. QAMBALO) aliuliza:-

Pamoja na kuwa katika Kata ya Qurus zipo Ofisi ya Kituo cha TANESCO, Vijiji vingi vya Kata hiyo vikiwemo Gongali, Qurus, Qorongaida, Genda na G/ Lambo havijafikiwa na umeme na vichache vyenye umeme, kwango cha usambazaji ni kidogo sana:-

Je, ni lini Serikali itawapaia wananchi wa Kata hiyo huduma hiyo muhimu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Willy Qulwi Qambalo, Mbunge wa Karatu linaloulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Flatei Massay Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jina la Kata iliyoko Wilayani Karatu ni Qurus yenye vijiji vya Bashay, Doffa G'Lambo, Gendaa, Gongali, Qorong'aida na Qurus. Aidha, hakuna Ofisi ya kituo cha TANESCO katika Kata hii. Vijiji vyote 23 vilipangwa kupatiwa umeme katika mradi wa *REA* awamu ya II Wilaya ya vimewashiwa umeme na hivi sasa Mkandarasi *Angelique International Ltd* anaendelea na kazi ya kuwaunganishia umeme wateja. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 99 na utakamilika ifikapo tarehe 30 Juni, mwaka huu. Gharama za mradi huu ni shilingi bilioni 53.24.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge G'lambo, Gongali, Qorong'aida na Qurus vimewekwa kwenye mpango wa *REA* awamu ya III unaoanza Julai, 2016. Kazi ya kupeleka umeme katika Vijiji hivi itahusisha pia ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 8, ujenzi wa njia ya umeme msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 12, ufungaji wa transfoma 5 zenye ukubwa mbalimbali lakini pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 236. Gharama ya kazi hii ni hsilingi milioni 740.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana.

Kwa kuwa, ni makosa ya uchapaji nashukuru amekiri kuwa Kata hii ya Qurus ipo na kwamba Kijiji hiki cha Gongali ndiko ofisi ya *TANESCO* ilipo. Sasa

kuna Vijiji ambavyo amevitaja hapa katika swali la msingi ambavyo vinaitwa Gendaa na Bashay;

Je, ni lini vitapata umeme?

Pia, kwa kuwa Wilaya hii ya Karatu ni pacha kabisa na jimbo la Mbulu Vijijini; Je, Vijiji vya Mbulu Vijiji ambavyo vinafanana kabisa kwa majina haya ya Gendaa ambavyo viko Mbulu Vijijini na Bashay ambavyo viko Mbulu Vijijini na Vijiji vingine vya Endara Gadati na Vijiji na Haidereri, Kantananati, Bashay, Yaeda Ampa lini vitapatiwa umeme? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa katika Jimbo la Karatu ni vijiji vichache vimepata umeme. Lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge anayeuliza swali kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge ambaye hayupo ni kwamba, vijiji vingi sana mbali na alivyovijata vya Qorong'aida na vingine, ikiwemo na kijiji cha Changarawe kitapata umeme kule kwa Mheshimiwa wa Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine kijiji cha Kambi ya Faru kitapata umeme kijiji cha Udongo Mwekundu kitapata umeme, pamoja na Vijiji vingine vya Rositeti vitapata umeme, hilo ni katika Jimbo la Karatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo lake Mheshimiwa Mbunge alivyouliza vijiji vya Mbulu ametaja Qorong'aida, ametaja na vingine. Lakini kuna vijiji vingi ambavyo hajavitaja ni jumla ya vijiji 73 kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mbunge havijapata umeme. Ninamshukuru sana anavyoendelea kuwahangaikia wananchi wa Mbulu, nimhakikishie tu ametaja vijiji vinne lakini bado kuna vijiji vingi ambavyo bado havijapata umeme kwenye Jimbo lako. Nikivitaja vitano tu kati ya vile 78 ambavyo havijapata ni pamoja na Masiedo haina umeme, Labei haina umeme, Mangandi haina umeme, vijiji vyote hivi vitapata umeme kwenye *REA* awamu ya tatu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naona bado mmesimama amesema Vijiji vyote vitapata umeme *REA* awamu ya tatu bado mna maswali? Mheshimiwa Catherine Magige!

MHE. CATHERINE V. MAGIGE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutuhakikishia kuwa Karatu watapata umeme, maana Karatu ni katika Mkoa wangu. Vilevile katika Mkoa wa Arusha kuna maeneo mengi sana wana tatizo la umeme. Mfano wa Arumeru wananchi walitoa mashamba yao, wakachimba mashimo kwa ajili ya umeme wa *REA,* lakini mpaka sasa hivi wananchi wale wa

Arumeru hawajapata umeme. Kuna malalamiko kuwa pesa zinazopangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo hazifiki na hata zikifika hazifiki zote.

Je, Serikali itatatua vipi tatizo hilo la umeme? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Katherine na nimpongeze sana, amehangaika sana hata kwenye ununuzi wa *transformer* tumeamua tununue hapa ndani kwa sababu ya juhudi zake, nakupongeza Mheshimiwa Catherine. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kumuhakikishia tu wananchi wa Arusha watapata umeme, ni kweli kuna matatizo ya umeme Arumeru na kuna vijiji vingi sana kama vya Urojora pamoja na vingine havijapata umeme naelewa. Lakini kumhakikishia Mheshimiwa Magige kwenye Jimbo lote tumetenga bilioni 13.7 kwa ajili ya wananchi wa Arusha. Ili kuhakikisha kwamba, *REA* awamu III matatizo yote yanaisha. Sambamba na hilo yapo matatizo ya umeme hasa kwenye eneo la Arusha la kukatika katika kwa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu nilishazitaja lakini nidokeze tu, kwa sasa hivi Serikali kupitia *TANESCO* pamoja na wakandarasi tunaboresha sasa miundombinu ya umeme. Kuanzia leo, tumesema tatizo la *low voltage* tunakwenda kulikamilisha kwa sababu sasa tunasafirisha nguvu kubwa, tunasafirisha nguvu kubwa yenye kilovoti 400 kwa upande wa Arusha kutoka Dar es Salaam kupitia Chalinze kwenda Bagamoyo, kwenda Arusha mpaka Namanga, kilomita 664.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa upande ule tatizo la kukatika kwa umeme litakwisha kabisa, lakini juhudi nyingine pamoja tumeamua sasa kukatika kwa umeme kuna sababisha pia uharibifu wa *transfomer* na hii inasababisha wakati mwingine na utaratibu wa kununua *transfomer* kutoka nje. Sasa hivi kama mlivyokwisha kusikia tumetangaza na naendelea kusema tena, awamu inayokuja sasa na *transfomer* tutakuwa tumenunua hapa nchini kwa sababu *TANALEC* wana uwezo wa kutengeneza.

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudi nyingine za kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme wakati mwingine ni matatizo ya nguzo. Sasa hivi *TANESCO* imeunda kampuni tanzu ambayo itakuwa inatengeneza *concrete pole* kwa ajili ya kutengeneza nguzo hizo hapa nchini. Hivyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwamba, sasa tatizo la umeme litakwisha mara moja. *(Makofi)*

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Njombe Mjini halimo kwenye mpango wa *REA* limo kwenye mpango wa umeme unaoenda Songea, hiyo kazi hiyo haijaanza.

Je, ni lini kazi hiyo itaanza ili kusudi wananchi wa Njombe na wenyewe waweze kunufaika na umeme?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa wananchi wa Njombe siyo kwamba hawatapata umeme wa *REA* wataendelea kupata umeme wa *REA* kama kawaida, lakini chanzo cha umeme kwa wananchi wa Njombe, Ludewa, Songea Mjini, Songea Vijijini, Namtumbo ni pamoja na ule umeme wa Makambako - Songea ambao ni wa Kilovoti 220.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kweli kwamba Mheshimiwa Mbunge, nakushukuru kwamba kwa sababu hujaona chini, watu nguzo wanaweka chini lakini kazi imeshaanza. Kazi za awali za upembuzi yakinifu zimekamilika na taratibu za Mkandarasi za kuanza kazi zimekamilika, kufikia Januari mwaka unaokuja kazi rasmi za kutifua na kuweka nguzo zitakuwa zimeshaanza kabisa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Seif Ungando, Mwenyekiti wa Wandengereko. *(Kicheko, Makofi)*

MHE. ALLY S. UNGANDO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza la nyongeza. Maeneo ya Kibiti, Ikwiriri, Bungu kumekuwa na tatizo la umeme kukatikakatika.

Je, lini Serikali itamaliza tatizo hili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwishakueleza kwenye jibu langu la msingi na maelezo mengine ya nyongeza. Ni kweli kuna maeneo mengi ambayo bado umeme unakatika katika na sababu za kukatika nimezieleza. Lakini niseme tu, taratibu za kukamilika kwa kukatikakatika pamoja na matatizo mengine ya umeme tutakapokamilisha kusambaza hizi nguvu kubwa za *kilovolt* 400 na *kilovolt* 220 ambapo kazi rasmi itakamilika 2018/2019, kwa hiyo kuanzia wakati huo, maeneo ya Kibiti, maeneo ya Ikwiriri na maeneo mengine ya kule chini, tatizo la kukatika katika kwa umeme litakwisha kabisa.*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto sasa aulize swali lake

Na. 393

Hitaji la Mahakama ya Ardhi na Nyumba la Lushoto

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI aliuliza:-

Wilaya ya Lushoto ni miongoni mwa Wilaya kubwa na Kongwe nchini ambapo ina takribani watu laki tatu lakini haina Mahakama ya Ardhi hivyo Wananchi hufuata huduma hiyo hadi Wilaya ya Korogwe licha ya kwamba majengo tunayo:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha Mahakama hiyo katika Wilaya ya Lushoto ili kuwapunguzia adha wananchi wake wanaofuata huduma hiyo Wilayani Korogwe?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Shekilindi naomba Waheshimiwa Wabunge wafahamu kuwa, lengo la Serikali la kuunda Mabaraza ya Ardhi katika kila Wilaya ni kusogeza huduma za utatuzi wa migogoro ya ardhi karibu na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua hilo, katika mwaka wa fedha 2015/2016, Serikali kupitia Wizara yangu kupitia Gazeti la Serikali Namba 545 ilitangaza kuanzisha jumla ya Mabaraza 47 ambayo yataundwa nchini likiwemo Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu na unyeti wa utatuzi wa migogoro ya ardhi katika Wilaya Kongwe ya Lushoto tarehe 6 Julai, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alizindua rasmi Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Lushoto. Kuanzia tarehe hiyo, Baraza limeshaanza kutoa huduma kwa wananchi wote wa Wilaya ya Lushoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa kutupatia jengo kwa ajili ya uanzishwaji wa Baraza hilo. Vilevile nitoe wito kwa Wakurugenzi wote nchini kuharakisha kutoa majengo kwa ajili ya ofisi za Mabaraza ili huduma hii muhimu iweze isogezwe karibu na wananchi na kuweza kupunguza kama siyo kumaliza kabisa kero mbalimbali za migogoro ya ardhi nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shabani Shekilindi swali la nyongeza!

MHE. SHABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante, kwanza kabisa nimpongeze Waziri Lukuvi na timu yake kwa kunifungulia Baraza hili la Ardhi na hata watu wa Wilaya ya Lushoto sasa walimuombea dua maalum Lukuvi na timu yake kwamba kama kuna gagaziko basi liondolewe Mungu awaletee wepesi liweze kuondoka. Sasa naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza;

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Waziri amekuja kutufungulia Baraza la Ardhi lakini bado tuna migogoro mikubwa ya ardhi kati ya kijiji cha Nywelo na msitu wa Shume; kati ya Shamba la Mkonge Mnazi na vijiji vya Kwemng'ongo na kijiji cha Kwemkwazu; kijiji cha Kwetango na kijiji cha Kweulasi; kijiji cha Kwemashai na kijiji cha Kilangwi.

Je, ni lini Serikali itakuja kutatua migogoro hiyo?

Swali la pili; Kwa kuwa, Wilaya ya Lushoto yenye Tarafa za Lushoto, Mlola, Mlalo, Mtae, Umba, Bumbuli, Soni na Mgwashi. Je, ni lini sasa Serikali itapima maeneo yao kwa kuwapatia hati za kimila ili wapate fursa za kukopa kwenye mabenki kuinua uchumi wao? *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hilo la mgogoro wa ardhi kati ya Mkonge Mnazi *Estate* na vijiji vya Kwemkwazu na Kwemhong'o, Kwemlazi na Kwetango, Kwemashai na Kilangwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, unajua haya majina ya watani wangu kidogo ni magumu kutamka usipoangalia unaweza ukakosea, lakini nadhani nimeyataja vizuri. Kwa sababu tulikwishatoa maelekezo na kwenye kitabu cha migogoro, mgogoro huu umetajwa na hatua za kuanza kwenda kutatua au kutwaa tena lile eneo kuna hatua za kupitia ikiwemo na kutoa *notes* kwa mhusika, tayari Halmashauri wamekwishatoa *notes* kwa huyu Mmiliki wa Mnazi *Estate,* kwa hiyo mara muda wa *notes* zile siku 90 zitakapokuwa zimekwisha, basi hatua zingine zitachukuliwa ili kuweza kumaliza kabisa mgogoro huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana ndugu zangu, watani zangu wa Kwemashai, Kilangwi, Kwaulasi, Kwetango na Kwemkwizu na Kwemng'ongo kwamba *notes* zikikamilika hatua kamili zitachukuliwa kama atakuwa ameshindwa kujitetea kama tunavyotarajia.

Swali lake la pili ameulizia habari ya upimaji katika Tarafa za Lushoto, Mlalo, Mlola, Mtae, Umba, Bumbuli, Soni na Mgwashi. Naomba tu nimhakikishie kwamba iwapo tutapitisha pia bajeti ambayo ndiyo inakwenda kupitishwa leo, tayari kule tumetenga pesa kwa ajili ya upimaji, takribani bilioni 8.8 ambazo zinakwenda kununua vifaa na vifaa hivi vitagawiwa katika ofisi zetu za Kanda ili watu waweze kupima katika maeneo kwenye Kanda zao ikiwemo haya maeneo ya Lushoto, Mlalo, Mtae, Umba, Bumbuli na maeneo mengine kama nilivyotaja hizi Tarafa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye suala la umilikishaji ardhi ambapo tunataka watu wote wawe na umiliki halali kwa maana ya kuwa na hati, tayari katika bajeti yetu tumetenga bilioni 13.8 ambazo zinakwenda kufanya kazi ya umilikishaji wa ardhi. Kwa hiyo haya yote yatakwenda kufanyika mara bajeti yetu itakapokuwa imepita, pia ni jukumu la Halmashauri zetu kuwa tayari katika suala hilo kwa sababu suala la upimaji pamoja na kwamba Wizara inafanya kazi hii, pia Halmashauri zinapaswa kujipanga vizuri kuweza kuona ni namna gani wanafanya matumizi bora ya ardhi katika baadhi ya vijiji vyao. Kwa sababu kiasi hiki bado kinaweza kisikidhi upimaji katika maeneo yote. Hivyo, kila Halmashauri inakumbushwa pia waone nao ni jukumu lao pamoja na kwamba Wizara itafanya kazi hiyo kupitia hizi pesa zilizotengwa, lakini bado Halmashauri wanao wajibu wa kupima maeneo yao.

NABI SPIKA: Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu maswali ya nyongeza yanatokana na swali la msingi, ili umpe Waziri fursa ya kuweza kujibu swali kama hilo kwenye eneo lako. Sasa tusitoke kabisa nje ya swali la msingi, tunakuwa hatupati majibu yale tunayoyatarajia. Mheshimiwa Steven Ngonyani.

MHE. STEPHEN H. NGONYANI: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Kwanza nikupongeze kwa kuzaliwa juzi Muhimbili na Mama Ulega, Mungu akubariki sana.

Swali langu ni kwamba, kwa kuwa baraza la ardhi la Wilaya ya Korogwe linafanya kazi katika mazingira magumu. Kuna kesi nyingi za kutoka mwaka 2009 mpaka leo hazijamalizika.

Je, ni lini Serikali itaongeza Watumishi pale ili kesi zile ambazo zimekaa kwa muda mrefu katika Baraza la Ardhi la Korogwe ziwe zimepata ufumbuzi wa haraka ili wananchi waone umuhimu wa Serikali yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, hii ndiyo sababu tumetenganisha yale Mabaraza na kuunda Baraza jingine la Lushoto, kwa sababu kesi nyingi zilizokuwa zinakuja Korogwe ni za Lushoto na Wilaya nyingine. Kwa hiyo tumeunda Baraza la Lushoto, tutakwenda kuunda Baraza jingine la Kilindi. Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumepunguza mzigo wa Korogwe na hivyo Baraza lile litakuwa limepunguziwa mzigo wa kuhudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tukichukua hatua hizo Baraza lile litahudumia watu wachache zaidi na hasa wananchi wa Korogwe.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zacharia Issaay

MHE. ZACHARIA P. ISSAAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri akiwa Mbulu aliwaahidi wananchi wa Mbulu kwamba Halmashauri ya Mbulu itafute jengo kwa ajili ya Mahakama. Namuomba Mheshimiwa Waziri katika mwaka huu wa fedha Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu itafanikiwa kwa kuwa ina kesi nyingi za ardhi ili Baraza hilo liweze kuzinduliwa na tayari Hamshauri imepata jingo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, rafiki yangu anajua majibu lakini anataka nirudie ili watu wake wasikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishakwenda, nimetangaza kwamba tutazindua Baraza la Mbulu mwaka huu, bahati mbaya sana majengo waliyotupa yalikuwa na 'mushkeli' kidogo, Katibu Mkuu wangu ameandika barua kuomba majengo mengine, nafikiri yakirekebishwa hayo majengo, nimeshamuahidi na nimeshawaahidi watu wa Mbulu kwa sababu nimekwenda mwenyewe na Serikali hii haifanyi longo longo inafanya mambo ya uhakika, kwa hiyo tutazindua hilo Baraza mwaka huu la Mbulu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Allan Kiula swali fupi!

MHE. ALLAN J. KIULA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru kwa kunipatia nafasi hii.

Kwa kuwa Wilaya ya Mkalama ni miongoni mwa Wilaya mpya ambazo hazina Mahakama ya Ardhi na huduma hiyo inapatikana Kiomboi.

Je, ni lini Wizara itaona umuhimu wa kutupatia Mahakama ya Ardhi na kuteua Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika majibu ya swali la msingi, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma hizi kwa wananchi kwa kufungua Mabaraza mengi kama ambavyo tumeyataja namna ambavyo nilisema kwamba tayari Mabaraza 47 Gazeti la Serikali lilikwisha yatangaza. Kwa hiyo kwenye suala la kufungua Baraza la Ardhi katika Wilaya ya Mkalama, naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo tutakuwa tumehakikishiwa eneo kwa ajili ya Mahakama, ambapo tumeomba pia Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya katika yale maeneo yenye uhitaji mkubwa waweze kutupa maeneo hayo ili kuweza kufanya. Hivyo, tutaweza kuangalia tukiona kama eneo lipo zuri la kuweza kutosha basi tutaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa tuliyonayo pia, hawa Wenyeviti wa Halmashauri bado ni wachache ukilinganisha na Mabaraza tunayotaka kufungua. Kwa hiyo bado tutakuwa na Wenyeviti ambao watakuwa wanahudumia pengine zaidi ya Baraza moja kulingana na uchache wao. Pale ambapo tutapata ajira mpya basi tutaweza kuwaeneza katika maeneo yao, kwa sasa naomba tu Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane katika hilo kwa sababu lengo ni zuri, ni jema lakini bado uhitaji ni mkubwa kwa maana ya Wenyeviti wa kuweza kufanya kazi hiyo. Pale tutakapokuwa tumewapata basi tutafanya kazi hiyo.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea, Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea sasa aulize swali lake.

Na. 394

Usambazaji wa Maji Mradi wa Mbwinji.

MHE. HASSAN E. MASALA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza maji ya mradi wa Mbwinji kwenye Vijiji vyote vinavyozunguka mradi huo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mbunge wa Nachingwea kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa Maji safi wa Msasi-Nachingwea kutoka chanzo cha Mbwinji unahudumia wakazi wapatao 188,250 wa Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na baadhi ya Halmashauri za Wilaya ya Masasi, kama vile Nachingwea na Ruangwa. Zaidi ya shilingi bilioni 40 zimetumika katika ujenzi wa mradi huo ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 24 Julai, 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha huduma ya maji katika Wilaya za Masasi, Ruangwa na Nachingwea, Mamlaka ya mradi wa Kitaifa wa Masasi - Nachingwea (MANAWASA), inakusudia kufanya upanuzi wa miundombinu ili kuunganisha vijiji vingi vikiwemo vijiji vya Mtepeche, Naipanga, Chemchem, Mailisita, Mkotokuyana na Nampemba vya Wilaya ya Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kutekeleza miradi ya upanuzi wa miundombinu ya usambazaji maji kupitia katika Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Masasi-Nachingwea na itaendelea kutenga fedha zaidi ili kupanua huduma ya upatikanaji wa maji katika Miji ya Masasi na Nachingwea pamoja na vijiji vyake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hassan Elias Masala swali la nyongeza!

MHE. HASSAN E. MASALA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza:

Swali la kwanza, kwa sababu mradi huu unagusa Wilaya zaidi ya tatu, Wilaya ya Nachingwea, Wilaya ya Ruangwa pamoja na Wilaya ya Masasi, kiasi cha pesa ambacho kimetengwa ni shilingi bilioni moja. Mheshimiwa Waziri anaweza kuwa tayari kunitajia ni vijiji gani ambavyo vitaanza katika awamu hii ambayo imetengewa bilioni moja, hasa vile vinavyogusa Wilaya ya Nachingwea?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ningependa kujua, mwezi Februari mwaka huu Mheshimiwa Naibu Waziri tulifuatana mimi na yeye ndani ya Wilaya ya Nachingwea kwenda kukagua miradi ya maji ya Chiola, Nampemba pamoja na maeneo ya Mkoka. Miradi ile bado haijakamilika na yako mambo ambayo yamefanyika ambayo siyo mazuri, alituahidi ataleta wataalamu kwa ajili ya kuja kufanya uchunguzi ili tuweze kuchukua hatua za kisheria kwa hujuma iliyofanyika kwenye miradi ile.

Je, Mheshimiwa Waziri anatoa jibu gani kwa Wananchi wa maeneo haya ambayo nimeyataja ambao wanasubiri majibu yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa naibu Spika, swali la kwanza, ameuliza katika hii shilingi bilioni moja tuliyoitenga ni vijiji gani katika Wilaya ya Nachingwea ambavyo vitahudumiwa na hii fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji ambavyo vilikosa maji katika awamu iliyopita ikiwemo Kitandi Nakalonji, Mkotokuyana, tutahakikisha kwamba hivi vijiji katika hii fedha ambayo imetengwa mwaka wa fedha huu tunaouanza tarehe Mosi Julai, tuhakikishe kwamba vijiji hivi pia vinapitiwa. Pia, Mheshimiwa Mbunge atusaidie kuwasiliana na mamlaka ya maji safi MANAWASA ili wakasaidine pia kupanga vijiji vingine zaidi ambavyo vinaweza vikapitiwa na fedha hizi kupitia huu mradi wa maji wa Mbwinji.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kweli nilitembelea Masasi Mkoa wa Mtwara na kwenda kujionea hii miradi ukiwemo mradi wa Chiola ambao nilikuta utekelezaji wake kidogo ulikuwa na mtatizo, baada ya kurudi niliwasilisha taarifa niliyoikuta kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri tayarai alishatoa maelekezo kwa uongozi wa Wizara ili kuunda timu kwenda kuangalia nini kilichojitokeza katika ule mradi na kuhakikisha kwamba uboreshaji unafanyika ili wananchi wa Chiola waweze kupata huduma ya mamji safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tumeelekeza kwamba miradi ile ambayo haikukamilika katika awamu ya kwanza, basi Halmashauri kwenye fedha tulizotenga katika Wilaya zihakikishe kwamba zinakamilisha ile miradi ambayo haikukamilika kabla hatujaingia kwenye miradi mipya.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Philip Mulugo!

MHE. PHILIPO A. MULUGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Sika, Mji wa Mkwajuni ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya mpya ya Songwe hatuna maji kabisa, hivi ninavyoongea ule Mji unakua, watu wanahamia kwa wingi sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura na kwa haraka tuweze kupata maji katika ule Mji ambao ndiyo Makao Makuu ya Wilaya na Mkuu wa Wilaya atakuja hivi karibuni pamoja na Wakurugenzi na Watumishi wengine wa Serikali?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tumeelekeza kupitia bajeti hii tuliyonayo kwamba tumetenga fedha katika Halmashauri ili Halmashauri zile ziweze kutekeleza miradi ya maji katika maeneo yao, lakini pia tumeelekeza kwamba Halmashauri zifanye utafiti wa kujenga mabwawa na wakishafanya utafiti walete taarifa Wizara ya Maji ili tuangalie katika mwaka wa fedha utakaofuata, tuweze kutoa fedha za kujenga mabwawa kuhakikisha kwamba miji yetu hii inakuwa na uhakika wa kupata maji, lakini kwa sasa Mheshimiwa Mbunge, ile fedha tuliyoitenga katika Halmashauri yako, naomba sana ushirikiane na Halmashauri ili ile fedha itumike katika kuhakikisha kwamba kwasababu ile Wilaya ni mpya, maji na upungufu utakaokuwa umejitokeza, basi naomba sana tuwasiliane. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya!

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii. Serikali katika kutatua upatikanaji wa maji hasa kwenye maeneo kame vijijini, imekuwa ikihamasisha kujenga miundombinu ya uvunaji wa maji kwa kutumia mapaa ya nyumba za Serikali, Asasi za Umma na nyumba za watu binafsi; na pia imekuwa ikitoa miongozi katika Halmashauri kutunga Sheria ndogo kwa ajili ya uvunaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nimekuwa nikishuhudia uvunaji huu wa maji ya mvua katika paa, ukivunwa kwenye mabati yaliyopakwa rangi. Naomba niambiwe kama kuna matatizo yoyote yanayopatikana kutokana na maji yaliyovunwa toka kwenye mabati yaliyopakwa rangi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Komanya, ameelezea vizuri kabisa kwamba lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba Halmashauri zinaweka Sheria ndogo ndogo na zinapitisha michoro kwenye ujenzi wa nyumba kuhakikisha kwamba kila nyumba inakuwa na kisima cha kuvuna maji kutoka kwenye mapaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la msingi ni kuhusu yale mabati yenye rangi. Mheshimiwa Mbunge nakushukuru kwa swali lako zuri. Rangi ikipakwa, baada ya siku 90 *process* ile ya *oxidation* inaondoa kabisa kemikali katika rangi,

kwa hiyo, baada ya miezi mitatu hata ukivuna yale maji yanakuwa hayana madhara ya aina yoyote. Kwa hiyo, wala hakuna wasiwasi wowote. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, hiyo elimu wale waopaka hizo rangi wanapewa kweli? Kama mvua ikinyesha kabla ya miezi mitatu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Nielekeze Wakurugenzi kwamba wasimamie, kwasababu nchi yetu imegawanywa na katika mgawanyo huo, utawala uko katika Halmashauri na Halmashauri ina wataalam wote. Kwa hiyo, Wahandisi wote walio katika Halmashauri wasimamie suala hili la upakaji rangi kwenye mabati. Ni kweli upakaji rangi umekuwa unafanyika kwa jinsi mtu anavyopata hela yeye mwenyewe, lakini naomba kupitia Halmashauri, basi elimu itolewe kwamba rangi nayo ina sumu ila baada ya muda fulani ile sumu inaondoka. Kwa hiyo, elimu hii itolewe kwa wananchi pale ambapo wananchi wanataka kupaka rangi katika maeneo yao. Utaratatibu ndivyo ulivyo kwamba unapotaka kufanya ukarabati wa aina yoyote kwenye nyumba ni vyema uombe kibali ili uwe na usimamizi unaofaa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Chikota!

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Tatizo la usambazaji wa maji linalokabili mradi wa Mbwinji, Nachingwea, linafanana na tatizo la usambazaji wa maji wa mradi wa Makonde hususan chanzo cha maji Mitema. Kwa hiyo, nataka niulize, Serikali ina mpango gani wa kufanya ukarabati mkubwa ili Miji inayonufaika na mradi ule; Nanyamba, Kitangari na Tandahimba wapate maji ya kutosha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, hili siyo swali dogo, ni swali kubwa la Mheshimiwa Chikota kuhusu mradi wa Mitema kupitia Mamlaka ya Maji ya Makonde.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba Mheshimiwa Chikota unawahisha shughuli na wakati unajua kwamba mradi ule tumeutengea zaidi ya Dola milioni 84, mradi wa Makonde, fedha ambayo inapatikana kutoka Serikali ya India. Nikuhakikishie tu kwamba wakati wowote, inawezekana kwenye mwezi wa Saba au wa Nane fedha hiyo itakuwa imeshaidhinishwa na utekelezaji wa mradi wa Makonde na pamoja na vyanzo vya Makonde na Mitema vitafanyiwa kazi nzuri kukarabati ule mfumo wote wa maji tuhakikishe kwamba wananchi wa maeneo ambayo yako chini ya Makonde wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Tunaendelea. Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 395

Tatizo la Maji Kasulu Mjini

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO aliuliza:-

Mji wa Kasulu ni Mji wa siku nyingi sana tangu enzi za Wajerumani lakini hauna mtandao wa maji unaokidhi mahitaji ya wakazi wa mji huo:-

(a) Je, ni lini Serikali itakarabati vyanzo vya maji vilivyopo ili maji yafike katika mitaa ya Kata za Mrusi, Mwilavya na Kidyama?

(b) Je, ni kwanini Serikali haitoi fedha ili kujenga tenki la kusafisha maji kwa sababu maji yaliyopo ni machafu?

(c) Je, ni kwanini Serikali haitoi pesa ili chanzo kingine kilichoainishwa kijengwe?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwanko, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu(a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto ya mtandao wa maji inayoukabili Mji wa Kasulu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kupanua mfumo wa usambazaji maji katika Mji huo. Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kuboresha hali ya huduma ya maji ikiwemo kuongeza mtandao wa maji Mjini Kasulu ambapo pia Kata za Mrusi, Mwilavya na Kidyama zitapata huduma ya maji safi na salama.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imekamilisha usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni kwa ajili ya mradi wa maji safi Mjini Kasulu. Usanifu huo pia umehusisha chujio la kutibu maji katika Mji wa Kasulu. Kwa sasa andiko la mradi limewasilishwa Tume ya Mipango kwa ajili ya kuombea ufadhili kutoka Serikali ya India. Gharama za mradi huo ni kiasi cha Dola za Marekani shilingi milioni 9.89.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika kipengele (b) hapo juu, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa mradi huo kupitia ufadhili au

mkopo nafuu kutoka Serikali ya India. Fedha hizi zikipatikana, ujenzi wa chanzo kingine utafanyika. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, swali la nyongeza.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO: Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri yenye matumaini ya Naibu Waziri kwa wananchi wa Mji wa Kasulu, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali langu la kwanza nataka kujua, hilo andiko la mradi kama Naibu Waziri anaweza akakumbuka, ni lini limepelekwa Tume ya Mipango ili tuweze kuwa na *comfort* kwamba jambo hili linashughulikiwa? Kama atakumbuka!

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, napenda kujua, naona fedha hizi shilingi bilioni 9.89 takriban shilingi bilioni 10 sasa, zinaombwa toka ufadhili wa Serikali ya India. Sasa kwa sababu zinaombwa toka Serikali ya India, napenda kujua kupitia kwako: Je, Serikali ina *fallback* yoyote endapo Serikali ya India haitatoa fedha hizi? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia masuala ya maji katika Mji wa Kasulu. Ni kwamba andiko hili tulishalipeleka Serikali ya India, kwenye Tume ya Mipango ilishapita, tumeshalipeleka tayari na muda siyo mrefu tunategema kwamba tuta-*sign* mkataba wa makubaliano ya kutekeleza mradi huu. Kwa hiyo, hali ni nzuri. Kama kutatokea kwamba kutakuwa vinginevyo, Serikali ipo. Serikali ya Awamu ya Tano katika vitu vyote ambavyo tayari tumeshavipanga, tutaweza kutumia fedha za ndani, kuweza kutekeleza mradi wa Kasulu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Doto Biteko!

MHE. DOTO M. BITEKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Matatizo yaliyoko Kasulu na yale yaliyoko Bukombe yanafanana kwa kiasi kikubwa na kwa sehemu kubwa yanatokana na ucheleweshwaji wa upelekaji wa fedha za miradi ya maji. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Bukombe juu ya maombi ya fedha, shilingi milioni 96 ambazo zimeombwa kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji iliyoanzishwa? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

MHE. NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dotto Biteko, umeomba shilingi milioni 96 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji katika Vijiji vya Ibambilo, Bukombe na Ikuzi. Katika bajeti ambayo

tumeitenga kwenye Halmashauri, naomba sana Mheshimiwa Biteko kwamba tufanye ushirikiano na Halmashauri kuhakikisha kwamba tunatekeleza kwanza ile miradi iliyokuwa inaendelea, tukikamilisha ndiyo tunakwenda kwenye miradi mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama fedha haitatosha kama tulivyotoa ahadi katika Bunge hili, basi usisite, tufanye mawasiliano ili kuhakikisha kwamba mwaka wa fedha utaofuata tunaendelea kutenga fedha tena kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika. Nitoe taarifa kama ilivyotolewa na Mheshimiwa Waziri kwamba kwa kweli tunashukuru kwamba fedha inatolewa na juzi tena Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametupatia shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, maeneo yote yale ambayo yalikuwa hayajakamilika, tunaendelea kuyakamilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono!

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Butiama linafanana sana na swali lililoulizwa hapo nyuma; nataka kujua, kwanini maji kutoka Mgangu kwenda Butiama hayajafika, sasa ni kipindi kama miaka 20. Itatokea lini maji yafike pale Butiama? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu!

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tunakamilisha usanifu wa mradi wa Mgango Kyabakari na tumeshaomba fedha kutoka Benki ya Maendeleo *KFW* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo, mradi huo utakapokuwa umekamilika utapita kwenye vijiji vingi. Mradi huu tunaukarabati; kwasababu ni mradi ambao upo, tunafanya ukarabati kuhakikisha kwamba tunasambaza maji maeneo mengi na tunaongeza chanzo cha upatikanaji wa maji.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu tunao tayari kwenye andiko na tukishamaliza usanifu, wakati wowote tunaanza kusambaza maji na tutarudi nyuma zaidi, tutaenda mpaka vijiji vya Byaiku Musoma, tutapitisha maji kule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, mradi huu tunao. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, sasa aulize swali lake.

Na. 396

Fidia kwa Wakulima wa Msitu wa Derema

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB aliuliza:-

Wakulima 1,128 wa msitu wa derema kata ya Amani Muheza wamekuwa wakilalamika kwa muda mrefu kupunjwa fidia ya mimea yao kutoka shilingi 3,315 kw a shina moja:-

(a) Je, ni lini wakulima hapo watalipwa stahiki zao,

(b) Je, kwa nini kwenye malip hayo Serikali sijijumiushe fidia ya ardhi yao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, kwa ajili ya majibu utusaidie wataalam wanapotayarisha haya majibu yanatakiwa yawe mafupi. Haya yanakuwa marefu sana.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa jumla ya wananchi 1,128 waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo ndani ya hifadhi ya msitu wa Derema, walihamishwa na kulipwa stahiki zao ili kupisha uhifadhi kati ya mwaka 2001 na mwaka 2009, lakini siyo kweli kuwa wananchi hao walipunjwa fidia ya mazao yao. Ukweli zaidi ni kuwa katika mchakato wa kuhakikisha eneo lote la msitu linahifadhiwa kama ilivyokusudiwa, mazoezi mawili tofauti yalifanyika kwa vipindi tofauti na kwa ufadhili wa taasisi tofauti ambazo ni Shirika la Maendeleo la Nchi ya Ufini, *FINNIDA* lililofadhili fidia kwa mazao kwenye mpaka na Benki ya Dunia waliofadhili fidia kwa mazao ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zoezi la kwanza lililofanyika mwaka 2001 mpaka 2002 chini ya ufadhili wa *FINNIDA* kupitia mradi uliojulikana kama *East Usambara Conservation and Management Programe,* idadi ya wakulima 172 waliokuwa wakifanya shughuli za kilimo upande wa nje wa eneo la msitu walilipwa fidia ya mazao yao. Kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umebaki hadi mradi kufikia tamati yake, shirika hilo liliwalipa wakulima kiwango cha shilingi 28,000/= kwa kila shina moja la mmea wa Iliki, bila ya masharti au kigezo kingine chochote mahsusi kutumika, lengo likiwa ni kuharakisha uhamishaji wananchi na uwekaji wa mipaka rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2002 hadi 2008 wananchi 1,128 waliokuwa na mazao ndani ya msitu walilipwa stahiki zao zenye jumla ya shilingi 1,633,893,595.85. Malipo hayo yalitokana na ufadhili wa Benki ya Dunia ambayo ilitoa jumla ya shilingi 1,238,653,060.85 na vyanzo vingine mbalimbali ambavyo vililipa jumla ya shilingi 395,240,535/=. Tofauti na zoezi la kwanza ulipaji katika zoezi hili ulizingatia masharti ya Benki ya Dunia, Sheria ya Ardhi 1998 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya 1999 pamoja na miongozo mingine ya fidia za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, thamani ya fidia iliwekwa katika viwango tofauti kulingana na sifa za ukomavu wa mazao, umri wa miche, utunzaji wa shamba na idadi ya mazao. Kulingana na vigezo hivyo, viwango vilivyokubalika vilikuwa shilingi 102/=, shilingi 204/=, shilingi 2,040/=, shilingi 3,315/= na shilingi 5,100/= kwa shina. Tathmini kwa mazao ya wananchi yaliyomo ndani ya msitu ilifanyika kwa ushiriki wa karibu wa timu huru za Wakaguzi kutoa Wizara, Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi, Mashirika ya Kimataifa na wananchi wenyewe. Aidha, kiwango cha chini kilichofidiwa ni shilingi 3,315/= na kiwango cha juu ni shilingi 22,832,172.32 kwa mkulima mmoja. Nakala ya nyaraka za tathmini na malipo yaliyofanyika zinapatikana katika Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya Muheza na Mkuu wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fidia ya ardhi, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Muheza na Mkoa wa Tanga iliahidi kuwapatia wananchi ardhi mbadala ambapo hadi sasa jumla ya maeneo 408 yenye ukubwa wa hekta tatu kila moja yamekwishapimwa na kwamba zoezi hilo la upimaji linaendela hatua kwa hatua kilingana na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya gharama za upimaji. Namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ili kufahamu zaidi hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa zoezi la ugawaji wa ardhi na namna linavyoendelea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Adadi Rajab, swali la nyongeza!

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Wakulima hawa wa Derema 1,128 wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu na malalamiko yao hasa yanazingatia kwamba fedha ambazo wamelipwa fidia ni ndogo sana. Fedha hizo zimezingatia shina la mti wa iliki na shina la mti wa karafuu, halikuzingatia mazao ambayo yanatokana na yale mashina.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu, kwa kuzingatia ubinadamu, acha mbali hizo sheria: Je, Serikali iko tayari kuwaongezea wakulima hawa wa Derema fidia hiyo?

Pili, ni kweli kabisa kwamba wakulima hawa wanatakiwa kuhamishwa na unapomhamisha mtu inahitaji fedha nyingi sana. Wiki mbili zilizopita Waziri Lukuvi alikuwepo kwenye maeneo hayo ya Kibaranga, ametukabidhi hati ya shamba lililofutwa na Mheshimiwa Rais na tunategemea kuwahamisha watu hawa wa Derema kwenye shamba hilo la Kibaranga, lakini uwezo wa kujenga hawana. Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kuja kuongea na wananchi hawa wa Derema ili aweze kuwapa matumaini kwamba wataongezewa fidia yao kidogo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, unaambiwa ujibu siyo kisheria lakini kibinadamu. Sasa sijajua kama ni Serikali inaombwa iongeze ama wewe kama binadamu. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kuhusu swali la kwanza; kwanza, nampongeza kwa kuwaonea huruma wananchi wa Jimbo lake, lakini pia nampongeza kwa jitihada anazofanya kwa kuwatetea kila itakavyowezekana ili waweze kupata wanachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ameshasema hata yeye mwenyewe kwamba majibu haya ni kwa mujibu wa sheria na utekelezaji wa ulipaji wa fidia pale awali ni kwa mujibu wa sheria na sasa anauliza kama Serikali inaweza kuangalia upande mwingine wa ubinadamu, nafikiri hoja ya msingi pale ni kuangalia kwamba fidia ambazo zinalipwa mahali pote, kwa nchi nzima kwa kweli, ziko kwenye viwango ambavyo vinatazamwa kuwa ni vya chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ubinadamu utatumika katika kwenda kuangalia upya sera na utatumika kwenda kuangalia upya sheria ili tuanzie kwenye ubinadamu lakini turekebishe sera zetu na sheria zetu kwa kuzingatia ubanadamu huo na ukweli na uhalisia ili malipo yaweze kulipwa kwa namna ambayo wananchi watakuwa wameona inakidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, nafikiri ni kama mwaliko kwamba niweze kupata nafasi ya kwenda, kwa sababu nikienda nitaona; na kuona ni kuamini. Basi namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, siyo tu mimi kwenda, nafikiri tuongozane naye twende tukaangalie, tuzungumze na wananchi hawa pengine tuwape elimu zaidi na kuweza kushirikiana nao katika kuona ukweli na kuweza kuona jambo gani linawezekana kufanyika kwa maslahi ya Taifa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Zainabu Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar.

Na. 397

Ukatili na Udhalilishaji Dhidi ya Watoto

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR (K.n.y. MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR) aliuliza:-

Vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia unaendelea kushamiri Tanzania hususan Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Visiwa vya Zanzibar, watoto wengi wanakataa kwenda shule kutokana na udhalilishaji huo. Aidha, wengi wao wanaogopa kunyanyapaliwa ama kuona haya au aibu juu ya vitendo wanavyofanyiwa watoto wa kiume na wa kike:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha suala hilo linapungua au linaondoka kabisa?

(b) Je, Serikali ya Tanzania ikishirikiana na Serikali ya Zanzibar inawasaidiaje watoto hawa ili waendelee na masomo bila kunyanyapaliwa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki watoto hawa kwa kuonekana watuhumiwa nje wakati wamewavunjia utu na maisha yao kwa kisingizio cha ushahidi haujakamilika?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza Mpango wa Taifa wa kudhibiti ukatili dhidi ya watoto wa mwaka 2013 - 2016, malengo ya mpango huu yakiwa ni pamoja na kuanzisha na kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto, kuanzisha na kuimarisha Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo vyote vya Polisi nchini, kuendelea kutoa mafunzo ya elimu ya malezi chanya kwa wazazi, Walimu na wanajamii, kuendesha mafunzo kuhusu Sheria ya Mtoto Namba 21 ya mwaka 2009 kwa wasimamizi wote wa sheria na kusimamia utekelezaji wake na kuhamasisha utumiaji wa huduma ya mtandao wa simu ya kusaidia kutoa taarifa za ukatili dhidi ya mtoto kwa kutumia *Child Help Line Number* 116.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo Serikali za Mitaa inaziwezesha Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto kutambua na kutatua matatizo ya watoto yakiwemo ya kisheria, kisaikolojia na kielimu.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ambapo haki za raia wote ikiwemo haki za watoto zinalindwa na kusimamiwa kikamilifu. Mtuhumiwa wa vitendo vya ukatili anapokamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria, taratibu za uendeshaji kesi hufuatwa ikiwa ni pamoja na kuithibitishia Mahakama kuwa kweli mtuhumiwa katenda kosa ua la. Hivyo, Serikali haipendi kuwaachia watuhumiwa wa vitendo vya ukatili punde wanapokamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria, bali mara nyingi kunakosekana ushirikiano wa jamii katika kutoa ushahidi wa kumtia hatiani mtuhumiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Faida Bakar, swali la nyongeza!

MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mbali na suala hili kwamba Serikali inachukua muda mrefu kusema kwamba haijapatikana ushahidi, lakini ushahidi anaweza akautoa mtoto kwamba ni fulani ndiyo kanifanyia kitendo hiki, lakini Serikali inasema bado ushahidi.

Pia kuna baadhi ya wazazi huwa wanaficha makosa haya, ama sijui kwa kuona aibu ama kwa kuoneana sijui vipi, labda huwa wanapewa hela na wale watuhumiwa. Je, Serikali inawachukulia hatua gani wazazi kama hawa wanaoficha ukatili huu dhidi ya watoto wao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, endapo mtoto ameathirika kiafya, yaani yule ni mtoto mdogo ujue, lakini kaathirika kiafya, maumbile yake yameathirika, Serikali inamsaidiaje mtoto kama huyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu!

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Utaratibu wa kesi ni utaratibu wa kisheria na haijalishi sana jambo lenyewe lina maumivu kiasi gani kwa watu wanaohusika kwenye kesi hiyo. Hivyo, utaratibu wa kisheria unataka ushahidi ufikishwe Mahakamani na Mahakama ishawishike bila kuwa na shaka kwamba kosa kweli limetendeka. Kwa sababu raia wote wana haki ya kutendewa sawa mbele ya macho ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, haiwezekani Serikali hata kama ina uchungu kiasi gani na watoto wanaofanyiwa vitendo vya ukatili, basi ikalazimisha tu hatua zichukuliwe dhidi yao bila utaratibu wa Kimahakama kufuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nitoe wito, wazazi watoe taarifa kwenye vyombo vya sheria kuhusiana na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto pindi vinapotokea. Kwa sababu pia jambo lingine ambalo linajitokeza kutokana na utafiti uliofanywa kwa kushirikiana na Wizara yetu pamoja na Chuo kikuu cha Muhimbili, ni kwamba maeneo hatarishi ya vitendo vya ukatili kwa zaidi ya asilimia 60 ni nyumbani ambapo watoto wanaishi, ikifuatiwa na shule kwa zaidi ya takriban asilimia 56.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hayo ndiyo mazingira ambayo watoto wanafanyiwa vitendo hivi, basi wazazi wakishirikiana na Walimu watoe taarifa kwenye mamlaka za kisheria na watoe ushahidi na wawe tayari kwenda kutokea Mahakamani ili kutoa maelezo yatakayowezesha watuhumiwa kuwekwa hatiani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi!

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Nataka tu kuongezea na kutoa rai kwa wazazi na kutoa onyo kwamba pale ambapo mtoto atatoa ushahidi na ikidhihirika kwamba amefanyiwa vitendo vya kikatili, tukigundua mzazi ama jamaa analegalega kwenye kutoa ushahidi, tutamuunganisha na wahalifu na hatua zitachukuliwa bila kujali kwamba yeye ni mzazi wake. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Khadija Nassir Ali, swali fupi la nyongeza!

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kuweza kunipatia nafasi ya kuuliza swali fupi la nyongeza. Je, ni kwa nini Serikali isiwapeleke watoto hawa kwenye makambi ya JKT kwa ajili ya kupatiwa mafunzo ya stadi za kazi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Bila shaka Mheshimiwa Khadija Binti Nassir alikuwa anamaanisha watoto wa Mitaani. Kama anamaanisha watoto wa Mitaani, hawawezi kupelekwa kwenye makambi ya majeshi ya JKT

kinyume na matakwa yao, kwa sababu watoto wana haki za msingi za kupatiwa ulinzi na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, wataendelea na sisi kama Serikali tunapenda waendelee kukaa kwenye familia; na kama kwenye Vituo vya Kulelea Watoto hawapati malezi stahiki, sisi utaratibu tunaoufanya kwenye Serikali ni kujaribu ku-*trace* familia wanazotoka na kuwapeleka kule ili waweze kuunganishwa na jamii yao. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Halima Ali Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa na Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 398

Kupunguza Vifo vya Akina Mama Wajawazito na Watoto

MHE. ANNA R. LUPEMBE (K.n.y. MHE. HALIMA ALI MOHAMED) aliuliza:-

Serikali imedhamiria kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga wakati wa kujifungua:-

Je, Serikali ina mikakati gani kufanikisha dhamira hiyo?

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima Ali Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imedhamiria kupunguza vifo vya wanawake wajawazito, pamoja na watoto wachanga kwa kuweka mipango na mikakati mbalimbali ikiwemo; kwanza, kupandisha hadhi Vituo vya Afya na kuviwezesha kufanya huduma za upasuaji wa dharura wa kutoa mtoto karibu zaidi na wananchi. Hadi sasa vituo 189 vimeshakamilika na vinafanya kazi hiyo.

Pili, kuanzisha Benki ya Damu kwa kila Mkoa ili kuimarisha upatikanaji wa damu; tatu, kugawa kwa wajawazito vifaa muhimu vinavyotumika wakati wa kujifungua; nne, kutoa kutoa huduma majumbani kwa wajawazito hadi wiki sita baada ya kujifungua; na watoto chini ya miaka mitano kwa kuwatumia Wahudumu wa Afya katika Jamii; na tano, kuendelea kutekeleza Sera ya Afya ya kutoa huduma bila malipo kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano, lengo likiwa kuhakikisha kwamba makundi haya maalumu yanapata huduma muda wote bila kuchelewa. Ili kuhakikisha kwamba haya yanatekelezwa, Serikali kwa kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,

Wazee na watoto, imeandaa mpango mkakati wa mwaka 2016 hadi 2020, wenye mikakati ifuatayo:-

(1) Kuboresha huduma zinazotolewa kwa wanawake wajawazito na watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na kuwapatia watoa huduma ya afya elimu kazini, kuongeza dawa, vifaa tiba na vitendea kazi;

(2) Kutoa elimu kwa jamii na hasa vijana kuhusu afya ya uzazi, pamoja na kutilia mkazo juu ya lishe bora;

(3) Kushirikisha jamii katika mambo yanayohusu afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na kuwahimiza wanawake wajawazito wajifungulie katika vituo vya kutolea huduma ya afya; na

(4) Kushirikisha wadau mbalimbali na kufanya kazi kwa pamoja, kwa kutekeleza afua zenye matokeo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutekeleza haya, tunaamini kwamba vifo vya wanawake wajawazito na watoto wachanga vitaendelea kushuka kwa kasi siku hata siku. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza!

MHE. ANNA R. LUPEMBE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Mpanda kuna vifo sana vya akina mama wajawazito na kwa kuwa Madaktari wetu pamoja na Manesi ni wachache:

Je, ni lini Serikali itaongeza Madaktari katika Wilaya ya Mpanda ili vifo vya akina mama wajawazito viweze kupungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Mpanda ni kama vile Hospitali ya Mkoa, hatuna Daktari Bingwa wa akina mama: ni lini Serikali itatuletea Daktari bingwa ili akina mama vifo vyao vipungue?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto!

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa sasa, hatuna uhakika ni lini tutakamilisha utaratibu wa ndani ya Serikali wa kutoa vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi kwenye Sekta ya Afya. Hivyo naomba avute subira mpaka hapo tutakapokuwa tayari kufanya hivyo.

Swali la pili, kuhusu Daktari Bingwa wa magonjwa ya akina mama wajawazito na watoto, kwenye Hospitali ya Mpanda, naomba kumshawishi Mheshimiwa Mbunge kwenye vikao vyao vya Halmashauri vya Bajeti kwenye Bunge linalokuja, wajipange kuanzia chini, kwenye Halmashauri yao kuweka kasma ya watumishi wa aina hiyo, lakini pia sambamba na kuweka kasma ya kuajiri Daktari Bingwa, waandae mazingira yatakayovutia Daktari huyo kuja kwenye hospitali hiyo na akifika, basi akae.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itafanya utaratibu wa kupanga watumishi kwenda kwenye hospitali hiyo kadri ambavyo watakavyokuwa wameomba. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ritta Kabati, swali fupi!

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize Sali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa njia mojawapo ya kupunguza hivi vifo vya mama na mtoto ni pamoja na kuboresha mfumo wa *referral,* yaani kutoka kwenye Vituo vya Afya, ama kwenye Hospitali za Wilaya kwenda kwenye Hospitali ya Mkoa; na kwa kuwa vituo vyetu vingi sana katika Mkoa wetu wa Iringa havina magari ya kubebea wagonjwa na vipo katika miundombinu mibaya sana ya barabara: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kila Kituo cha Afya kinapatiwa gari ili kupunguza hivi vifo vya mama na mtoto? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto!

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa hizi zimfikie Mheshimiwa Ritta Kabati na Wabunge wote ambao wangependa kupata magari ya *ambulance* kwenye Halmashauri zao, kwamba kwanza jukumu la kununua magari haya lipo kwenye Halmashauri zenyewe. Waheshimiwa Wabunge kwa kuwa ni sehemu ya Halmashauri hizi, kwenye mipango yao ya bajeti tayari tutakapomaliza Bunge hili utaratibu wa mchakato mzima wa bajeti utaanza, basi Wabunge wahudhurie vikao hivyo na waweke *ambulance* kama kipaumbele cha kwanza kwenye bajeti zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hivyo, sisi Wizara ya Afya, tutaendelea kuwaomba na kuwashirikisha wadau wa maendeleo watupe ufadhili. Kama tutafanikiwa kupata *ambulance,* basi tutazigawa kwenye hospitali zetu nchini.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwenda, kwa hiyo, inabidi tumalize hapo. Ninalo tangazo moja la wageni waliotufikia asubuhi ya leo. Wageni waliopo Bungeni ni pamoja na wageni waliopo jukwaa la Spika, ambao ni wageni nane wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. Ni mume wake ambaye anaitwa Dkt. Muhajir Kachwamba. Karibu sana shemeji yetu. Pia ameongozana na watoto wake na ndugu zake wengine. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge; kundi la kwanza ni wageni watano wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nao ni familia yake wanatokea Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na mke wake Ndugu Neema Mwigulu. *(Makofi)*

Wageni wetu, mkiitwa mnasimama, simwoni, sijui atakuwa upande gani? Aaah, kumbe wako upande huu! Karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Jitu Soni ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari *Chief Gidobat* na Shule ya Msingi Bagara kutoka Hanang Mkoani Manyara, ambao ni Ndugu Juliana Magwe na Ndugu Betilia Samwel. Karibuni sana.

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Zacharia Issaay, ambao ni wanafamilia yake kutoka Mbulu, Mkoani Manyara wakiongozwa na mtoto wake ambaye ni Benjamin Issaay. Karibubi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo pia wageni nane wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria, Tawi la Dodoma kutoka hapa Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 13 wa Mheshimiwa Shaban Shekilindi wanaotokea Mtaa wa Sechelala uliopo Mkoa wa Dodoma, wakiongozwa na Ndugu Nobart Pangaselo ambaye ni Mwenyekiti wa Mtaa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni 73 wa Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni Wajasiriamali, Vikundi vya Agape, Tumaini, Upendo na Ebeneza, kutoka Mkoa wa Iringa. Karibuni sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Hilo ni Tangazo la Wageni na hatuna matangazo mengine. Kwa hiyo, tunaendelea. Katibu!

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI: Hoja za Serikali kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na

kwamba, Bunge likubali kupitisha mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Majadiliano yanaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2015 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

na

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 – Wizara ya Fedha na Mipango

(Majadiliano yanaendelea)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jasmine Kairuki, atafuatiwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama halafu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa ajiandae!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA – MHE ANGELLAH J. KAIRUKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Bajeti hii Kuu ya Serikali.

Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu kwa maandalizi mazuri ya bajeti na kwa kweli ukiangalia sura ya bajeti hii unaona kabisa ni kwa namna gani Serikali imejipanga katika kumkwamua Mtanzania wa kawaida ili aweze kuona nafuu katika maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napongeza zaidi kwa namna ambavyo Wizara imeandaa Sera ya Matumizi katika kuhakikisha kwamba tunabana matumizi yasiyokuwa na tija na kuhakikisha kwamba Serikali itakuwa na matumizi yale tu ambayo kwa kweli, yataweza kuwa na tija kwa wananchi wake.

Mheshiumiwa Naibu Spika, napongeza zaidi kwa jitihada za Wizara ya Fedha za kuamua kuja na marekebisho ya Sheria ya Manunuzi ya Umma na kwa hakika kupitia Sheria hii pindi itakapopitishwa itaweza kuwa na manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niingie sasa katika hoja ambazo zimegusa Ofisi yangu na katika hoja ya kwanza ilikuwa ni katika suala zima la watumishi hewa. Kulikuwa na hoja, baadhi ya Wabunge walitaka kufahamu ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya Maafisa Masuuli, dhidi ya Wakuu wa Idara pamoja na

vitengo mbalimbali vya Uhasibu ambao kimsingi wao wameamini kwamba wanaweza kuwa walishiriki katika masuala haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba, kimsingi watumishi hewa wanatokana na kwamba, unakuta wakati mwingine labda mtu amefariki, wengine unakuta ni watoro, lakini wanatakiwa wawe wameondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara au *Payroll,* lakini wale waliokasimiwa mamlaka wanakuwa hawajatimiza wajibu wao ipasavyo. Wako watumishi wengine wanakaa katika *Payroll* na walitakiwa waondoke, hadi inafikia hata miezi 10 na zaidi!

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, kama Serikali, ili kukabiliana na tatizo hili tumekuwa tukiendelea kuchukua hatua na tunaendelea kumshukuru sana pia, Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake na kwa msukumo ambao ameupatia katika suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie tu kwamba, kwa sasa ambacho tumkifanya, kwanza kabisa ni kuhakikisha kwamba tunawaondoa watumishi wote ambao tumewabaini mpaka sasa; na tumeshabaini watumishi hewa 12,246 ambao endapo wangeendelea kuwepo katika orodha ya malipo ya mishahara, takriban shilingi bilioni 25.091 ingeendelea kulipwa kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, ukiangalia, hii ni kuanzia Mwezi Machi tu, tarehe 1; mpaka tarehe 30 Aprili, ambapo Mheshimiwa Rais alitangaza, walibainika watumishi hewa 10,295 na mpaka tarehe 30 Mei ndiyo hii watumishi 12,246!

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichokifanya hivi sasa tumezielekeza Mamlaka zote za ajira kuhakikisha kwamba wanachukua hatua za kinidhamu na za Kisheria. Hatutaki tu tutangaze kwamba tumeshaokoa kiasi kadhaa na kuondoa watumishi hawa hewa. Tunachokitaka hivi sasa; na ninapongeza sana mamlaka mbalimbali za ajira katika Mkoa wa Singida, mamlaka mbalimbali za ajira Mkoa wa Dar es Salaam, Mtwara na mikoa mingine yote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya katika kuhakikisha kwamba watu wote walioshiriki katika kusababisha watumishi hewa kuwepo, wameweza kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Mashitaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kuhakikisha kwamba mashitaka yote ambayo yatakuwa yamefunguliwa dhidi ya wale ambao walikuwa wakitafuna fedha za Serikali ambazo hazikuwa zinapaswa kulipwa kwao, lakini vilevile kuhakikisha kwamba, Maafisa Utumishi ambao kimsingi ndio tiumewaidhinishia matumizi ya mfumo huu, tumefundisha Maafisa Utumishi 1,500.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa tayari wakati wowote hata ikibidi kuwasimamisha Maafisa Utumishi hao wote 1,500 ili tuweze kuanza upya, tuwe na Maafisa Utumishi wenye uadilifu, wenye uzalendo na ambao wana hofu ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba, naendelea kuomba mamlaka za ajira wahakikishe kwamba, wanachukua hatua za kinidhamu pamoja na za Kisheria na wahakikishe mashitaka yote yanafikishwa katika mamlaka zinazohusika. Kwa wale ambao watashindwa kuweza kuchukua hatua stahiki kwa zile mamlaka za ajira kwa Maafisa Masuuli na wengineo tutawachukulia hatua kali za Kisheria kwa mujibu wa Sheria, Kanuni pamoja na taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja nyingine iliyouliza, endapo kuna umuhimu wa kuwa na *PDB* au la!

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunafahamu Ofisi ya Rais ya kusimamia ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi. Ofisi hii ilianzishwa mwaka 2013 na niseme tu kwamba, ni ofisi ambayo kwa kweli ni ya muhimu sana. Ukiangalia katika manufaa mbalimbali ambayo yameshapatikana hadi hivi sasa, sekta takriban 13 za kipaumbele zimeweza kuutumia mfumo huu na zimeweza kufuatilia na kutekeleza miradi yake mbalimbali kwa kweli kwa mafanikio makubwa na tumeshuhudia mafanikio ya takribani asilimia 71.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukiangalia katika ushirikiano ambao *PDB* imekuwanao na Pemandu ya Malaysia, ni mfumo ambao ukiangalia Uingereza wameutumia, Rwanda wameutumia, Malaysia wameutumia na kwa kweli, wameona mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kulieleza Bunge lako Tukufu kwamba, pamoja na kwamba, sekta ambazo ziko katika mfumo huu ni 13, lakini hivi sasa Mahakama haikuwepo katika mfumo huu, lakini wenyewe walishaanza kutekeleza mapendekezo ya mfumo huu na wamefanya vizuri sana nawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza pia Jeshi la Polisi na ninapenda pia kupongeza mamlaka mbalimbali za maji Mijini kwa namna ambavyo wameimarisha utekelezaji wa majukumu yao, lakini vilevile namna ambavyo wamekuwa na mafanikio katika kupanga na kufuatilia matokeo ya miradi yao mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ukiangalia ofisi hii itakuwa ya muhimu zaidi hasa katika mwaka huu ambapo tumekuwa na mapinduzi katika

maandalizi ya bajeti. Takribani asilimia 40 ya bajeti yote ya Serikali itaenda katika miradi mbalimbali ya maendeleo. Usipokuwa na ufuatiliaji mzuri na tathmini, ni namna gani fedha zako zimeenda huko? Ni vipaumbele gani ulikuwanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuwa na ripoti mbalimbali za kila wiki ili kuweza kujua namna miradi mbalimbali inavyotekelezwa. Kwa hiyo, niseme tu kwamba, naendelea kuomba mamlaka mbalimbali ambazo ziko katika mfumo huu, lakini na nyingine ambazo bado hazijajiunga na Mfumo wa *BRN* basi wajitahidi kuona ni kwa namna gani wanaweza wakajiunganao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono Bajeti hii Kuu ya Serikali. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jenista Mhagama, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa. Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa dhati kabisa nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa umahiri mkubwa na umakini mkubwa unaoonesha katika kusimamia shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiukweli umejipambanua kama ni mtaalam na mwanamke unayeweza kuhimili mikiki ndani ya Bunge, lakini unao weledi wa hali ya juu wa kuhakikisha kwamba Bunge hili linaongozwa kwa kufuata Kanuni ambazo zimewekwa na sisi Wabunge wenyewe. Naomba nikutie moyo, katika safari yoyote kuna magumu, lakini yastahimili kwa sababu Umma wa Watanzania unaamini kabisa kwamba unao uwezo wa kutusaidia kuliongoza Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi ya pekee pia kuwapongeza sana Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza sana!

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi walikuwa wanadhani kwamba Wabunge hawa wa Chama cha Mapinduzi uwezo wao katika kuyachambua mambo, kuchangia michango yenye kuwawakilisha Watanzania ni mdogo, lakini katika Bunge la Bajeti la mwaka huu, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wameonesha wanao uwezo mkubwa sana wa kujenga hoja; wa kuwakilisha matatizo mbalimbali na mahitaji ya wananchi waliowachagua na kuamua kuwaweka wawakilishe katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge hawa wa Chama cha Mapinduzi wamefanya kazi kubwa ya kihistoria katika Bunge hili kwa mwaka huu na katika

bajeti ya mwaka huu. Kwa hiyo, kwa kweli, naomba niwapongeze. Wameishauri Serikali, wametoa michango ambayo Serikali ikiifanyia kazi, inaweza ikatimiza vizuri Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshiriki kikamilifu katika mchango wa Hotuba ya Bajeti ya kwamba michango yao ambayo wameotoa, kwanza kupitia Kamati za Bunge, lakini na michango ambayo wameitoa na ushauri walioutoa kupitia Kamati ya Bajeti, sisi kama Serikali tutaichukua na kuifanyia kazi ipasavyo. Nasema hivyo kwa sababu gani?

Katika bajeti ambayo tumekuwa tukiijadili ili tuipitishe leo, ingawa watu wengi wanasema kwamba Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wamejiandaa kutokupitisha bajeti yao, jambo ambalo siyo kweli na leo watashuhudia tutakapopitisha bajeti hii! Nasema hayo kwa sababu sitaki Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wachonganishwe na Rais wao na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii ni ya kwetu sisi kama Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi na inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na tunaamini kabisa kama Serikali, haya ambayo yamechangiwa, tena na Waheshimiwa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ndiyo wananchi waliyotutuma kuyafanya ndani ya Bunge la Hamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli wa jambo hili unajidhirisha katika Kanuni yako ya 94 ya Kanuni za Bunge. Kanuni hiyo ya 94 kwa faida ya Watanzania nitaisoma tu kidogo. Kanuni ya 94 inasema, "Katika Mkutano wake wa Mwezi Oktoba na Novemba kwa kila mwaka Bunge kwa siku zisizopungua tano litakaa kama Kamati ya Mipango, ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 63(3)(c) ya Katiba kwa kujadili na kuishauri Serikali kuhusu mapendekezo ya Utekelezaji wa Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika mwaka wa fedha unaofuata." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni hiyo ya 94, kazi ya Mkutano huo, Mkutano ambao ni Mkutano wa Kuishauri Serikali, itapokea na kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mwongozo wa Kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali.

Kwa hiyo, sisi Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuna miaka mitano ya kuishauri Serikali yetu na kuhakikisha tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatuna shaka na tutayafanya hayo yote bila wasiwasi wowote na Serikali yetu itaendelea kutekeleza matakwa ya Watanzania, bajeti moja hadi nyingine kwa kipindi chote cha miaka mitano na

Watanzania wawe na amani Wabunge wa Chama cha Mapinduzi tuko imara na Serikali iko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji wengi wamezungumza matatizo ya Sekta ya wafanyakazi na hasa katika sekta binafsi. Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa Sheria za Kazi, kumekuwa na tatizo kubwa la wageni kufanya kazi bila vibali katika nchi yetu ya Tanzania, lakini vilevile kumekuwa na wageni ambao wanatumia ujanja ujanja tu katika kupata ajira katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote, yako marekebisho ya Kisheria tutayaleta hapa katika Bunge hili yataipa meno Serikali kupambana na waajiri wote wanaokiuka Sheria za Kazi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wabunge wamechangia sana kuhusu masuala ya hifadhi ya jamii kwa maana ya *Social Protection*. Tunajua, tunajipanga kupitia upya Sheria zetu zinazosimamia mifuko ya hifadhi ya jamii ili kero ambazo zinawapata Watanzania katika sekta hiyo ziweze kushughulikiwa inavyotakiwa, lakini kubwa zaidi ni kuhakikisha tunaongeza wigo wa kuwafanya Watanzania wengi wafikiwe na suala zima la hifadhi ya jamii katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Munde na Wabunge wengine wameomba sana tuongeze fao la bodaboda katika mafao ambayo yatakuwa yanatolewa katika sekta hii ya hifadhi ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshakubaliana na mifuko yote kuona ni namna gani sekta binafsi, hawa vijana wetu wa bodaboda nao waingizwe katika suala zima la *social protection* ili waweze kupata faida ya mafao yanayotolewa na mifuko.

Mhshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mimi na Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Mavunde, tumejipanga na tutapita katika Mkoa mmoja baada ya mwingine ili kuona namna gani tunashirikiana na nyie katika suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine tutayajibu kimaandishi, lakini naunga mkono bajeti hii na ninampongeza sana Waziri wa Fedha na Naibu wake. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Sospeter Mwijarubi Muhongo!

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutupa fursa ya kuchangia kwenye hoja muhimu ya Serikali iliyoko mbele yetu. Kabla ya yote, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Wabunge wengi wamechangia, hasa kuhusu miundombinu, kwani Wabunge wengi wanafahamu bila miundombinu nchi yetu haiwezi kuingia katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianzia na Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Miundombinu, ametoa hoja ifuatayo: katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka Mmoja Serikali imeainisha miradi saba ya kielelezo itakayohitaji mtaji mkubwa wa uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi hiyo ni ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge,* ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu, kuboresha Shirika la Ndege Tanzania, ujenzi wa Barabara ya Kidahwa – Kanyani, Kasulu – Kibondo – Nyakanazi na Barabara ya Masasi – Songea – *Mbaba Bay* pamoja na mradi wa makaa yam awe na Mchuchuma na mradi wa chuma wa Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inataka Serikali kuainisha miradi itakayotekelezwa kwa mfumo wa *Public Private Partnership,* muda wa kukamilisha na gharama za mradi husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu hoja hiyo, kama ifiuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutekeleza miradi ya barabara kwa kushirikisha sekta binafsi kwa utaratibu wa PPP.

Kwa sasa mradi pekee wa barabara ambao umepangwa kutekelezwa kwa utaratibu huu ni ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze *Express Way*. Barabara hii inatarajiwa kuwa na urefu wa kilometa 140 itakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu wa mradi huu upo katika hatua za mwisho za kukamilishwa. Mara baada ya hatua hii kukamilika gharama za awali na muda wa utekelezaji wa mradi huo utajulikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Ghasia alikuwa na hoja ifuatayo; ushauri kwa Serikali kuhakikisha inahusisha Sekta binafsi kwa kugharamia mradi kwa njia ya ushirikishi yaani *PPP* pamoja na kutumia fedha zake za ndani ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo. Ushauri umepokelewa, Serikali imepanga kutekeleza miradi

mingi iwezekanavyo ya miundombinu ya usafiri kwa njia ya *PPP* kila inapowezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge kama ifuatavyo; kwanza ushauri kwa Serikali kuhakikisha sekta wezeshi zinatekeleza miradi kikamilifu kwa bajeti iliyotengwa kwa miradi hiyo. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Chunya hadi Itigi, na barabara ya Ipole hadi Ikoga. Ushauri umepokelewa kwa barabara ya Chunya hadi Itigi upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilika kwa barabara yote yenye urefu wa kilometa 413 na barabara hii itajengwa kwa awamu. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 zimetengwa shilingi bilioni 5.84 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwango cha lami wa sehemu ya Itigi - Mkiwa yenye kilometa 35. Kwa sehemu iliyobaki Serikali itaendelea kujadiliana na washiriki wa maendeleo ili zipatikane fedha kwa ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa barabara ya Ipole, Koga hadi Mpanda hatua za ununuzi wa Wahandisi Washauri watakapofanya mapitio ya usanifu na usimamizi, pamoja na mkandarasi atakayejenga barabara hiyo zinaendelea. Ujenzi umepangwa kuanza katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya shilingi bilioni 103.93 zimetengwa kama inavyooneshwa kwenye kitabu changu cha bajeti ukurasa 223.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja kutoka kwa Mheshimiwa Josephat Kandege, Mbunge wa Kalambo kama ifuatavyo; kwanza anatoa pongezi kwa Serikali, pongezi hizo zimepokelewa, pia anatoa ushauri kwa Serikali kuwathibitishia au kuondoa wataalam wanaokaimu nafasi mbalimbali za uongozi katika taasisi na Serikali Kuu ili kuboresha uwajibikaji wa watumishi husika.

Kwanza ushauri huo umepokelewa, pili Serikali inaendelea na utaratibu wa kuhakikisha kuwa wataalam wote ambao sasa hivi wanakaimu wanafanyiwa *confirmation* ili wawe na muda wa kutosha wa kufanya kazi hiyo. Kwa kuanzia tu wiki iliyopita tulitangaza Bodi ya *TPA* ambayo sasa imeanza kufanya kazi, hatua inayofuata sasa hivi ni kumchangua Mtendaji Mkuu wa Bandari au Mamlaka ya Bandari ili aweze kuendelea na kazi hiyo ya kuendesha bandari zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau wa Jimbo la Mafia ambapo hoja yake inasema kama ifuatavyoa; Serikali itoe mchanganuo wa muda wa utekelezaji yaani *timeframe* ya miradi yote ya maendeleo pamoja na gharama zake na siyo tu kwa ujumla kwa mfano ujenzi wa kiwango cha *express way* wa barabara ya Dar es Salaam hadi Chalinze.

Kwanza ushauri umepokelewa Mheshimiwa Mbunge, muda halisi wa ujenzi wa barabara ya *Chalinze express way* utajulikana baada zabuni kutangazwa na mwekezaji kujulikana. Kwa sasa mtaalam elekezi anakamilisha upembuzi yakinifu wa mradi huo na wakati huo utakapofika muda maalum utaelezwa kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia alikuwa anahoja Serikali ijengwe….

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa muda wako umekwisha naomba umalizie.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, narejea tena naomba kuunga mkono hoja asilimia moa moja.

NAIBU SPIKA: Asante sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba ajiandae.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Naibu na Wizara nzima ya Fedha kwa sababu wametengeneza bajeti ambayo ni ya mwaka mmoja lakini iko kwenye picha ya miaka mitano na iko kwenye picha ya dira yetu ya maendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyojadili hii bajeti usiichukue kama ni ya mwaka mmoja, lazima uone kwamba ni bajeti ambayo imeanza safari ya kwenda mwaka 2025. Kwa hiyo ikiwa kweli tumedhamiria kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 inamaanisha bajeti yetu lazima inapanuka, inakuwa kubwa na fedha nyingi zinaenda kwenye maendeleo na siyo matumizi ya kawaida na ndiyo shukrani zangu nazitoa kwenye hii bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema tunataka kuwa nchi ya kipato cha kati mwaka 2025 maana yake ni kwamba ukipiga hesabu, bajeti yetu sasa hivi ni vizuri nikiongea kwenye dola kwa sababu nalinganisha na nchi zingine, *GDP* yetu (Pato la Taifa) karibu kwenye bilioni 55, 56. Kama tunataka kuwa nchi ya kipato cha kati, mwaka 2025 tunataka bajeti yetu ambayo itaonesha kwamba *GDP per capita* (pato la mtu mmoja) litakuwa la dola 3,000 inabidi tuizidishe mara nne. Kwa hiyo hii bajeti ni kubwa kwa sababu ifikapo mwaka 2025 tukiwa nchi ya kipato cha kati ni lazima tuwe na *GDP* ambayo ni zaidi ya bilioni 200 tuzidishe mara nne bajeti ya sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa basi *engines* ziko nyingi sana, *engine* za kupeleka vitu huko mbele huko na *engine* mojawapo ni umeme, na ndiyo maana bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini imekuwa kubwa ni ya shilingi trilioni

1.23 katika hiyo bajeti asilimia 94 zinaenda kwenye maendeleo na ukichukua kwenye maendeleo asilimia 98 inaenda kwenye umeme. Hapo ndipo unajua bajeti ya Serikali iliyotayarishwa na Dkt. Mpango na wenzake imedhamiria kweli kutufikisha uko. Dalili za kusema kwamba fedha zinapatikana ni kweli zitapatikana, mwaka huu tunaomaliza mwezi huu, Wizara ya Nishati na Madini upande wa maedeleo tumeshapata asilimia 82 na *REA* - umeme vijijini tumeshapata asilimia 81.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti yetu kwa hiyo ni kwamba umeme vijijini ndiyo itawatoa watu kwenye umaskini. Bajeti mliyoipitisha ya umeme vijijini imo ndani ya bajeti kubwa ya Serikali ambayo ni ya umeme vijijini shilingi bilioni 534.4, hii imeongezwa kwa asilimia 50 ya bajeti ya mwaka uliopita. Lakini Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ni kwamba kwa mara ya kwanza kwa historia ya nchii hii, na kuonesha hii Serikali ya Awamu ya Tano imedhamiria kujenga nchi ya viwanda, ni kwamba umeme vijijini tutakuja kufikisha trilioni moja. Kwa sababu hii ni Serikali inayoaminika, hata wenzetu wanaopenda kutuchangia maendeleo na wao wanaweza wakachangia zaidi ya bilioni 500 na taarifa nitawapatia ndani ya wiki mbili kutoka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hii bajeti inahakikisha umeme unapatikana, siyo umeme tu kusambaza, lakini hii bajeti ndiyo itatuhahakikishia kwamba vyanzo vyetu vyote tulivyonavyo vya umeme tunaanza kuzalisha umeme. Tumejipanga kuzalisha umeme kutokana na gesi asilia, makaa ya mawe, maji, sola, upepo, joto ardhi, mawimbi *(tides and waves)* na mabaki ya mimiea *(bio energies)*. Hayo yote yako kwenye hii bajeti ya trilioni 29.5, kwa hiyo ndugu zangu Wabunge tusipoipitisha hii, tukiwa na wasiwasi nayo basi haya yote ya umeme hayatakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii bajeti uzuri wake ndiyo inakuja kutuhakikishia kwa mara ya kwanza kwa historia ya nchi hii haya mambo ya umeme ambao unakatikakatika hii bajeti ndiyo nakuja kutoa suluhisho la kudumu. Tunajenga njia za kusafirisha umeme kutoka kilovoti 220 tunakwenda kilovoti 400.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mimi ningependa kuzidi kuwashawishi kwamba hii bajeti siyo ya mwaka mmoja bali inaanza safari ya kutufikisha mwaka 2025 na kwenye hii bajeti ndiyo tumeweka miradi mingi ya usambazaji wa umeme na ni muhimu sana. Waheshimiwa Wabunge wengi mmelalamika kwamba kuna vijiji vimerukwa. Hii bajeti ndiyo ina mradi wa kushusha transfoma na kusambaza nyaya kwenye vijiji ambavyo vimerukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge, mmesema hii sekta ya nishati haijashikwa vizuri sana na Watanzania. Hii bajeti ndiyoina fedha za kuwawezesha wazalishaji wadogo wa umeme na wao waweze kuchangia

kwenye umeme wa Gridi ya Taifa. Vilevile kwa upande wa kuboresha upatikanaji wa umeme, hii bajeti itatuwezesha kuibadilisha *TANESCO* kabisa itoke *TANESCO* ya zamani kuja *TANESCO* ya karne ya 21. *TANESCO* itakuwa na ushindani, lakini bajeti ya kubadilisha muundo, mfumo na utendaji unaolalamikiwa wa *TANESCO* uko kwenye hii bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaoenda huko kuanzia tarehe 1 Julai tunaweka taratibu za kisheria za kunyang'anya *TANESCO* mamlaka ya yenyewe ndiyo inazalisha peke yake, ndiyo inauza umeme peke yake, ndiyo inasafirisha umeme peke yake.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mimi nigependa bado kusisitiza kwamba ni muhimu sana hii bajeti tukaiunga mkono na istoshe tumekuwa na sehemu tunaulizia ni kwamba kwa mfano wengine wamesema fedha za *CAG*, fedha za nani, ukweli ni kwamba bajeti hii acha ianze kufanya kazi na mahali ambapo tutakwama tutarudi tena hapa Bungeni kurekebisha.

Meshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo hii bajeti ni muhimu na diyo itatufikisha mwaka 2025 ambapo *GDP per capita* yetu ambayo itatoka sasa hivi dola *945 GDP per capita* mpaka kwenda dola 3,000 kama *GDP per capital.*

NAIBU SPIKA: Asante Profesa. Mheshimiwa George Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha kwa mipango na bajeti nzuri ya kwanza wa Serikali ya Awamu ya Tano ambayo kusema ukweli ni bajeti ambayo ni *realistic*.

Mimi nimesimama ili nizungumze pamoja na mambo mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge, yanayohusu Wizara ya TAMISEMI ambayo ndiyo Wizara ya wananchi, lakini ndiyo Wizara inayokwenda kubadili maisha kwa maana ya huduma za Jamii ambazo wananchi wanazitarajia kutoka kwenye Serikali yao, pia waheshimiwa Wabunge mliahidi sana kule kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo megi ambayo mmesema juu yamaji, juu ya miundombinu, lakini mimi nimesimama hapa kwa sababu ya muda nizungumzie eneo moja ambalo limeonekana kuchangiwa na Wabunge wengi sana takribani Wabunge 27 wamezungumzia suala la huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nitoe takwimu ya hali tuliyonayo kwa sasa kwenye zahanati na vituo vya afya. Tunavyo vijiji 12,545 na sera yetu inasema kila kijiji lazima kiwe na zahanati, zahanati tulizonazo ni 4,700 tu.

Kwa hiyo, tuna upungufu wa zahanati takribani 7,845 kwa sababu tulizonazo ni asilimia 38 tu, utauona upungufu huu ni mkubwa. Lakini sera yetu pia inasema tutakuwa na kituo cha afya kila kata, tunazo kata 3,963 na tuna vituo vya afya 497 tu ni asilimia 13 ya mahitaji. Kwa hiyo upungufu wetu ni vituo vya afya 3,466.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Serikali za Mitaa zimejitahidi sana, kuna ujenzi mbalimbali ya majengo ambayo sasa tunayaita maboma, tunayo jumla ya maboma ya zahanati 1,443; tunayo jumla ya maboma ya vituo vya afya 244 na tunayo jumla ya maboma ya hospitali za Wilaya 51, kazi hii imefanywa vizuri sana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini. Mpango wetu sasa wa kushirikiana kwa Serikali nzima tumejaribu kuongea na Waziri wa Fedha na Waziri wa Afya ambaye yeye anasimamia utoaji wa huduma na Wizara ya TAMISEMI ndiyo inayojenga, inamiliki na kuendesha utoaji huu wa huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu kuzungumza, jambo la kwanza tulilokubaliana ni kwamba tupitie upya ramani ile ili iwe ramani ambayo inamudu kwa uchumi wetu lakini itatoa huduma zinazostahili zote. Kwa sababu ramani iliyopo Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu ni kubwa kiasi kwamba inakatisha tamaa kwa vituo vya afya kuwa na ramani kubwa kiasi kile. tulipoipunguza ramani ile tunahitaji kiasi kama cha bilioni 2.5 kwa kila kituo cha afya kilichokamilika na huduma zake zote kutolewa ikiwa ni pamoja na upasuaji, fedha hizi bilioni 2.5 Waziri wa Fedha ananiambia tunaweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa bajeti hii ya sasa niombe mambo mawili, la kwanza tuendelee na mpango wetu ule ule wa Halmashauri kuwa na mpango wa kuwa na zahanati kila kijiji waendelee na mpango wa wananchi na Halmashauri kuendelea, isipokuwa sisi Serikali kuu tuone namna ambavyo tutakuja na mpango wetu sasa wa ujenzi wa vituo vya afya, hapa tunaweza tukafanya vizuri kwa sababu kwa upungufu tulionayo, tukiwa tunajenga kila Halmashauri kituo cha afya kimoja kila mwaka wa fedha nina hakika kwa miaka mitatu iliyobakia tutakuwa tumejenga vituo vitatu vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tutakuwa na vituo vya afya vingi tu kuliko hata tulivyojenga toka tulivyopata uhuru. Kwa hiyo, mimi nasema kwa bajeti hii ambayo tunakwenda nayo yakwanza hii ambayo imetenga takribani bilioni 32 kwa ajili ya umaliziaji wa maboma haya niliyoyataja, itatufikisha mahali fulani. Lakini bado niwaombe na niombe sana kwamba tuhakikishe

tunasimamia *own source* hii ambayo tulipanga kukusanya ili maboma haya ya vituo vya afya yakamilike kwa sababu ndiyo tuliyopitisha kwenye bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo yakikamilika haya maboma tutakuwa tumekamilisha zahanati 1.443, vituo vya afya 244 itakuwa ni hatua moja mbele ili tukija kwenye bajeti inayokuja ya mwaka 2017/2018 tutakuja na mpango huu sasa ambao tutakuja na bajeti mahususi kwa ajili ya vituo vya afya kama nilivyosema ambayo kama tutakwenda hivyo kila mwaka, kila Halmashauri ikajenga kimoja ambacho kinakamilika nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukajenga vituo vya afya vingi kwa miaka mitano, na hata tukimaliza miaka yetu mitano tukaweza kusema tumefanya kitu gani kila mmoja kwenye jimbo lake.

Waheshimiwa Wabunge, niwasihi na niwaombe sana, muunge mkono bajeti hii ya Serikali ili iweze kutekelezwa kama ambayo tumepitisha kwa shilingi bilioni 32 katika sekta ya afya lakini tusimamie tu michango yetu kwa makusanya ya Halmashauri yaweze kukusanywa kwa sababu utoaji wa huduma siyo ujenzi tu wa haya majengo, pia kuna suala la watumishi kwa idadi inayotakiwa ya watumishi. Lakini pia ni jambo ambalo linahitaji katika ukamilifu wake ili iweze kutoa huduma ile tunayostahili, kwa hiyo lazima haya yote yaende yakiwa yanaandaliwa kwa pamoja, tusikurupuke tukawa na majengo lakini vitu vingine vikawa haviendi sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnafahamu tuna upungufu wa wataalamu wa afya, lazima tuwe na huo uwezo na wenyewe pia ujengwe sambamba na ujenzi wa haya maboma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani haya ndio machache ambayo yamesemwa,na mimi nimeona nizungumzie kwenye jambo hili la afya, nirudie tena kutoa wito Waheshimiwa Wabunge tukashirikiane kule; tuhimize makusanyo ya Halmashauri ili mipango tuliyoipanga hii maana imepangwa na sisi iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, Mheshimiwa January Yusuf Makamba ajiandae.

WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa na mimi naomba niseme moja kwa moja kwamba, naunga mkono hoja ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuunga mkono niseme tu kwamba Kilimo, Mifugo na Uvuvi karibu Wabunge zaidi ya 60 wamezungumzia mambo

mbali mbali; na kwa manufaa ya muda, naomba nizungumzie tu machache katika hayo ambayo kwa wingi zaidi yamezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nizungumzie tu suala la sukari kwamba sukari ipo nchini. Sukari ipo nchini na inaendelea kuletwa, sasa hivi tunachokifanya ni kusimamia vizuri usambazaji wa hii sukari ili ifike maeneo yale ambayo tulihisi kwamba yanaanza kuwa na upungufu na tumewaomba Wakuu wa Mikoa wasimamie vizuri zoezi hili la upelekaji wa sukari hasa kwenye Wilaya ambazo ziko mbali na Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine lililozungumziwa sana kwa hisia na Waheshimiwa Wabunge, ni kodi nyingi zilizoko kwenye mazao ya kilimo, uvuvi, na ufugaji. Hizi kodi kwanza Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni aliwaahidi Watanzania kwamba zitafanyiwa kazi, na kwa kadri itakavyowezekana, zitapungunzwa au kuondolewa. Bajeti hii imekwishaanza, ziko aina za kodi ambazo Waziri wa Fedha katika hotuba yake alipendekeza ziondolewe; na sasa hizo hazitakuwapo kwenye pamba, kahawa, korosho, ziko kodi ambazo tayari zimekwisha ondolewa na kwenye tumbaku pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivyo hili jambo linaendelewa kufanyiwa kazi, Serikali imeunda Tume ya Makatibu Wakuu, nilikwisha sema kwenye kujibu maswali ya Wabunge hapa, kwamba Kamati hiyo inaendelea kuzipitia, na kodi zile ambazo zitaonekana hazina madhara katika bajeti hii na bajeti za Halmashauri, zitaondolewa mara moja kadri ya mapendekezo yanavyokuja; na zile ambazo zitakuwa na *effect* kwenye bajeti hii, basi tutasubiri tuziondoe muda muafaka kwenye bajeti ya mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumeanza msimu wa pamba. Pamba msimu utazinduliwa kesho huko Mkoa wa Geita, katika kijiji cha Nyang'hwale, naomba sana kwanza bei elekezi nzuri ambayo itakuwa na manufaa kwa pande zote mbili, wanunuzi na wakulima wa pamba itatajwa kesho. Lakini niombe kutumia muda huu kuwaomba Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wa maeneo inakozalishwa pamba, wasimamie vizuri masoko, wananchi wasipunjwe kwenye mizani, kwa sababu wako wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, wanabana mizani kuwaibia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia niseme na upande mwingine, kwamba wako wakulima wasiokuwa waungwana, wanaochakachua pamba kwa maji na michanga ili wapate uzito zaidi na kwa kufanya hivyo wanaharibu ubora wa pamba yetu, kwa hivyo wanapunguza thamani yake katika soko la dunia. Wote hawa niwaombe sana Wakuu wa Mikoa, hakikisheni mnatumia uwezo wa kisheria mlionao kudhibiti vitendo vya namna hii pande zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao lingine linaloleta shida sana katika usimamizi na uendeshaji wake ni tumbaku. Tumbaku umekuwa wimbo, vyama vya msingi vinakufa na wafanyabiashara makampuni ya tumbaku yanaendelea kunufanika na kupata faida. Sasa bahati mbaya sana hapa katikati utaratibu ulilegezwa wakaingizwa na wakulima binafsi na *associations* katika tasnia hii ya tumbaku. Matokeo yake imekuwa ni vyama vingi vya ushirika kudorora au kufa kabisa, kwa sababu hawa *independent farmers* na *associations* hizi, zingine hazina mashamba lakini wana tumbaku wanauza sokoni. Sasa tutahakikisha hili jambo haliendelei tena, maelekezo yalikwisha kutolewa wasisajiliwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naangalia uwezekano wa kupunguza madaraja ya tumbaku. Madaraja ya tumbaku yako 67, haiwezekani. Wakulima hawajui, tumbaku ikisindikwa haitoki na madaraja 67, kwa nini katika kuuza iwe na madaraja 67. Hili jambo tunalifanyia kazi na kwa kweli nadhani tutayapunguza ili yawe yale yanayotambulika kwa wananchi na wakulima; kwamba madaraja ni matano, basi yabaki kuwa matano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wafugaji na wakulima. Hili jambo ukilitazama na chimbuko lake ni ukosefu wa malisho na maji kwa wafugaji, kwa hivyo wanalazimika kuhama kwenda kuvamia maeneo ambayo hayakuwa yamelengwa kwa ajili ya ufugaji. Sasa tunachokifanya tutarajie kwamba kwanza tutapitia upya mgawanyo wa Ranchi zote za Taifa, ili kujua wale waliopewa kweli walikuwa wanastahili; na hicho walichopewa kukifanya huko kama wamekifanya, kwa sababu kilichobainika katika ziara za viongozi wetu, ni kwamba mtu alipewa kipande cha Ranchi, badala ya kufuga yeye mwenyewe anakitumia kuwakodisha wenyeji wa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii haikuwa nia ya Serikali kwamba iwagawie watu maeneo haya kwa ajili ya kukodisha, kwa hivyo tunaangalia upya, yule aliyeshindwa kutimiza masharti aliyokuwa amepewa tutawanyanganya ili wananchi waweze kugawiwa maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa wameombwa waainishe maeneo mapya, yanayowezekana kufanyia malisho na ufugaji wa ng'ombe, ili tuweze kupanua maeneo haya; kwa sababu yako maeneo hayatumiki vizuri, sasa haya yakibainika mkoa kwa mkoa tunaweza tukawathibiti wafugaji wetu katika maeneo ya Mikoa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kusema naunga mkono hoja.*(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako, atafuatiwa na Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie hoja hii iliyoko mbele yetu na nianze kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa bajeti nzuri ambayo wameiwasilisha mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii na nitatoa sababu kwa nini naiunga mkono hoja hii. Bajeti hii imeandaliwa kwa umakini mkubwa na ina dhamira ya dhati kabisa ya kuondoa matatizo ya wananchi na kuleta maendeleo. Ukiangalia sekta ya elimu, sekta ya elimu imetengewa kiasi cha shilingi trilioni 4.77 ambayo ni sawa sawa na asilimia 22.1 ya bajeti yote hii na mgawanyo huu wa fedha unaonesha bayana, jinsi gani ambavyo Serikali ina dhamira ya dhati ya kuwahudumia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa elimu katika maendeleo ya nchi hii na ndio maana fedha zimetengwa za kiasi kikubwa na fedha hizi nyingi zitaelezwa katika miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naipongeza Wizara ya Fedha,kwa kuja na vyanzo vipya vya mapato ambavyo vitaiwezesha Serikali kupata fedha, za kutekeleza mpango ambayo imeahinishwa na kama walivyozungumza wachangiaji wengine, hii ni bajeti ya mwaka mmoja tu.

Mheshimiwa Naibu Spika,hii bajeti imetokana na Mpango wetu wa Maendeleo wa Miaka Mitano na imezingatia katika kutufikisha kule ambako tunatarajia kufika ukizingatia Ilani yetu ya uchaguzi na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwa hiyo niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge wenzangu tuiunge mkono tukitambua kwamba hii ni bajeti ya mwaka mmoja, haiwezi kumaliza matatizo yote kwa sababu Serikali inakwenda hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuunga mkono bajeti hii ya mwaka mmoja, kutaiwezesha Serikali kuanza hatua yake ya kuwatumikia wananchi na kuwaletea maendeleo, katika maeneo ambayo yameainishwa. Vilevile napongeza kwa dhati kabisa, hatua za Serikali za kubana matumizi na kudhibiti matumizi yasiyokuwa ya lazima, hii yote inaonesha jinsi gani ambavyo Serikali ina dhamira ya dhati kabisa kuwatumikia wananchi wake hivyo tuna kila sababu ya kuunga mkono bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa nizungumzie kidogo masuala ambayo yalielekezwa katika sekta ya elimu na kutokana na muda nitazungumzia mambo machache na mengine tutayajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, limejitokeza suala la fedha za utafiti,na Waheshimiwa Wabunge wameonesha wasiwasi wao kwamba kiasi cha fedha kilichotengwa ni kidogo na kwamba msisitizo katika utafiti wa kilimo, haupewi kipaumbele kinachotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kusema kwamba Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya utafiti, kupitia kwenye Tume ya Taifa ya Utafiti yaani *COSTECH; na* kuna kazi nyingi ambazo zimekuwa zikifanyika na utaratibu tu ambao umekuwa ukitumika ni utaratibu wa ushindani. Kumekuwa na hoja kwamba kwa nini utumike utaratibu wa ushindani kutoa fedha za utafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa ushindani kwanza unaihakikishia Serikali kwamba yule anayeomba fedha yuko tayari, kwa maana ya kwamba tayari atakuwa na mpango kazi wake. Anajua anataka kufanya nini kwa hiyo inaihakikishia kwamba yule anayepata fedha kwa ushindani anakuwa anazitumia fedha hizo vizuri, badala ya kuzigawa hata kwa mtu ambaye hajawa yuko tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia suala la ushindani jumla ya miradi 102 imeweza kufadhiliwa,na ambapo kuna masuala mengi tu yamefanyika ikiwa ni pamoja na kujenga rasilimali watu kuwajengea uwezo wa kuweza kufanya utafiti; na katika hilo jumla ya watafiti 517 wamepatiwa mafunzo na jumla ya watu 130 wamepata mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu. Vilevile fedha za utafiti zimewezesha kujenga miundombinu ya kufanyia utafiti ambapo kwa mfano Serikali imeweza kujenga mabwawa 42 ya zege na kukarabati maabara za uzalishaji wa vifaranga vya samaki katika Chuo Kikuu cha Sokoine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika bajeti ya mwaka 2016/2017 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 12.8 kwa ajili ya suala la utafiti. Lakini pamoja na fedha hizi, bado Serikali itaendelea kupata fedha kupitia kwa wafadhili mbalimbali ambao wamekuwa wakipeleka fedha hizo moja kwa moja katika vyuo vyetu vya elimu ya juu.

Suala lingine ambalo limezungumzwa katika Wizara yangu ni suala la kuitaka Serikali iangalie kozi zinazoanzishwa katika vyuo vya elimu ya juu, kujiridhisha kama kuna walimu wa kutosha. Niwahakikishie Watanzania kwamba katika kuhakikisha ubora wa elimu hiyo ndio kipaumbele chetu katika Awamu ya Tano. Hivyo basi hakuna kozi yoyote ambayo itaanzishwa kama Serikali haijaridhika na miundombinu, kama Serikali haijaridhika na uwepo wa elimu

ambao wana sifa stahiki. Pamoja na kuangalia kozi mpya lakini niseme kwamba hata kozi ambazo zipo Serikali inafanya mapitio kuona kwamba kozi zote zinazotolewa katika elimu ya juu zina wataalam wa kutosha na ziko katika mazingira ambayo yanastahiki. Kwa hiyo, tutachukua hatua zinazostahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la ukarabati wa vyuo vikuu, pamoja na miundombinu ya kutolea elimu. Ukiangaliwa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha na kitabu cha hotuba cha Wizara yangu, tumebainisha wazi mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kwamba tunakarabati miundombinu ya shule na vyuo vikuu ili kuhakikisha kwamba Watanzania na wananchi wanapata elimu katika mazingira ambayo ni rafiki na kama nilivyosema tunafanya hatua kwa hatua, kwa mfano katika mwaka huu wa fedha, tutaweza kufanya ukarabari kwenye shule kongwe 40. Lakini vilevile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni Chuo Kikuu kongwe tumekitengea kiasi cha shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kufanya ukarabati na hili zoezi ni endelevu. Kama nilivyosema hii ni hatua tu, lakini ahadi zetu zitatekelezwa katika miaka mitano. Kwa hiyo tutaendelea kukarabati na kuhakikisha kwamba mazingira ya kujifunzia yanakuwa ni rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumziwa ni suala la elimu bure, kwamba hii sera iende mpaka kidato cha sita. Ninachoweza kusema ni kwamba kama Serikali, tumepokea huo ushauri lakini tungeomba kwamba kama tunavyosema tunataka utekelezaji wetu wa ahadi kwa wananchi uende hatua kwa hatua. Kwa hiyo tumeanza na mpaka kidato cha nne tungeomba kwanza tuendelee kuimarisha utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo kwa kidato cha nne na kutatua changamoto ambazo zipo kabla hatujafikiria kuongeza wigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lililozungumziwa katika eneo langu ni suala la *VETA* kuwa na vifaa vya kisasa na hilo tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa January Yusuf Makamba atafuatiwa na Mheshimiwa George Mcheche Masaju**,** Mheshimiwa Dkt. AshatuKijaji ajiandae.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa fursa ya kuchangia. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara; kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kuandaa bajeti hii. Nawapongeza sana Wabunge wa CCM kwa kutimiza wajibu wao waliotumwa na wananchi wao kwa kutimiza sababu yao ya kuchaguliwa kwa kuingia

Bungeni kufanya kazi waliyotumwa na wananchi na kueleza shida za wananchi wao mbele ya Serikali, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo kadhaa ambayo ningependa kuyazungumzia, la kwanza ni suala la *VAT* kwa Zanzibar na Bara. Kuna upotoshaji mkubwa sana kwamba hatua iliyochukuliwa na Serikali, hatua nzuri kabisa ya kuhakikisha kwamba bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara kwenda Zanzibar *VAT* inakusanywa Zanzibar; na bidhaa zinazozalishwa Zanzibar na kuletwa Tanzania Bara *VAT* inakusanywa Tanzania Bara. Kuna upotoshwaji mkubwa sana unaofanywa na wenzetu kule Zanzibar kwamba hatua hiyo inaiumiza Zanzibar, si kweli, ni kunyume chake. Hatua hii inainufaisha Zanzibar, hatua hii itawaumiza wale wadanganyifu wachache, waliokuwa wanatumia utaratibu huu kujipatia kipato ambacho sio halali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ambalo ningependa kulizungumzia ni ahadi ya Chama cha Mapinduzi kwenye Ilani yetu kwamba kila kijiji kitapatiwa shilingi milioni 50 kwa ajili ya uwezeshaji, ukopeshaji wa wajasiliamali. Ahadi hii ya CCM ni hatua kubwa ya kimapinduzi ya kumuondoa Mtanzania katika lindi la umaskini. Mzunguko wa shilingi milioni 50 katika kijiji ni pesa nyingi sana zitakazoleta chachu ya maendeleo pale kijijini. Serikali katika mwaka huu wa fedha kama ambavyo mmeona, imetenga shilingi bilioni 59 kama kianzio, lakini zaidi ya hapo Serikali imeunda jopo la wataalam ambalo linatengeneza utaratibu madhubuti kabisa. Utaratibu utakaozingatia uzoefu wetu huko nyuma wa mifuko mbalimbali na mafanikio ya mifuko hiyo ili tuwe na utaratibu mzuri utakaohakikisha fedha hizi zinatumika kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa linabidi lifanyike kwa umakini na umahiri mkubwa ili tusipoteze fursa hii adhimu katika kuwaokoa watu wetu. kwa hiyo utaratibu mzuri unaotengenezwa na Serikali utaletwa hapa Bungeni ili kabla ya kutumika na ninyi Waheshimiwa Wabunge muwe na mchango wenu katika aina ya utaratibu ambao Serikali itautumia na ikiwezekana kabisa aidha ni kwa kuleta Sheria mpya au kufanya mabadiliko ya Sheria katika Sheria ya Uwezeshaji sasa hivi. Ili fedha hizi ziwe katika msingi wa kisheria na ziweze kutumika vizuri kuliko mifuko mingine yote huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli kwamba zimetengwa shilingi bilioni 59, haina maana kwamba tutashindwa ndani ya miaka mitano kufanya vijiji vyote; tumeweka hizi ili tuanze na tujifunze na kadri tutakavyokuwa na utaratibu mzuri, kasi ya kupanga fedha nyingi zaidi ili tutimize ahadi hii kwa miaka mitano inakuwepo. Kwa hiyo napenda kuwahakikishiwa Waheshimiwa Wabunge na watanzania, kwamba hii ni ahadi ya CCM, hii ni ahadi ya Rais na itatimia bila shaka yoyote. *(Makofi)*

Naomba niseme kidogo jambo moja muhimu. Sisi Chama cha Mapinduzi tulipomteua Dkt. John Pombe Magufuli kuwa mgombea wetu, tulitoa *statement* duniani kwamba tunahitaji aina mpya ya nchi kutokana na aina ya kiongozi huyo. Kwetu sisi kumteua yeye tulitoa kauli duniani kwamba tunataka mabadiliko ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya kweli hayawezi kuletwa kwa hatua ndogo ndogo, mabadiliko ya kweli yanaletwa hatua kubwa na yanaletwa na uthubutu na uthubutu huo umeanza kujidhihirisha katika bajeti ya mwaka huu, tumethubutu kwamba tunaweza kukusanya shilingi trilioni 29.5; tumethubutu kwamba tunaweza kutenga asilimia 40 kati ya hizo kwa maendeleo. Unapothubutu jambo kubwa kuna watu watatia shaka, sisi wana CCM Serikali hii ni ya kwetu, Bunge hili ndio wengi, ilani ni ya kwetu, tusitetereke katika uthubutu wetu wa kukusanya shilingi bilioni 59 tumsaidie Rais tuisaidie nchi yetu kufikia malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa suala la hatua za kikodi hapo mbalimbali imetokea malalamiko kwamba kodi ni kubwa, kodi ni nyingi zitadhohofisha uwekezaji. Jambo hilo si la kweli kwa sababu utafiti unaonyesha mimi hapa ninayo ripoti inaitwa *Tax incentive in a global perspective* inasema kwamba; *survey analysis shows that host country taxation and international investment incentives generally play only a limited role in determining the international pattern of FDI. Factors like market characteristics, relative production costs and resource availability explain most of the cross-country variation in FDI inflows. Transparency, simplicity, stability and certainty in the application of the tax law and in tax administration are often ranked by investors ahead of special tax incentives.*

Suala siyo kiwango cha kodi, suala ni mfumo wa kodi. Kwa hiyo, miaka yote tumeaminishwa kwamba ukiweka kodi ndogo wanakuja, ukiweka kodi kubwa hawaji, dhana hiyo si ya kweli. Ukitengeneza mambo mengine vizuri zaidi ndiyo wanakuja ikiwemo uhakika wa mfumo wa kodi. Kwa hiyo, tusiwatishe wananchi na tusitishane hapa kwamba kiwango cha kodi tulichoweka kitafukuza wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja nimalize kwa kusema kwamba Rais Magufuli tumempa usukani wa kuiongoza nchi yetu, lakini nchi hii ni yetu sote na sisi tunawajibu wa kumsaidia ili tufanikiwe. Rais Magufuli akifanikiwa, nchi yetu imefanikiwa sisi tusiwe kama watazamaji kwamba ngoja tumuone atafanyaje, sisi tuko naye kwenye basi hili tumsaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua tunazochukua nchi yetu ni sawasawa na gari nzuri aina ya benzi iliyoingia kwenye matope tunataka kuirudisha kwenye lami, hatua ya kuirudisha kwenye lami itakuwa na

misukosuko, kuna wengine wataamua kushuka lakini tuendelee kuwa ndani ya gari hilo mpaka likae kwenye lami lifike safari. Maendeleo yanahitaji *sacrifice,* katika bajeti hii Wabunge sisi tume-*sacrifice*, tume-*sacrifice* kwa kukubali kukatwa kodi, kila mtu lazima a-*sacrifice,* wafanyabiashara, waendesha bodaboda, kila mmoja lazima a-*sacrifice* ili nchi yetu iende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalize kwa kusema mwaka 1961 wakati Rais Kennedy wa Marekani anaapishwa aliwaambia wa Marekani kwamba *ask not what your country can do for you, but what you can do for your country.* Ni wakati sasa kwa Watanzania wote kutokaa siku zote na kujiuliza nchi hii itanifanyia nini bali sisi tutaifanyia nini nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Masaju nilikuwa nimeshakuita uniwie radhi ukae kidogo. Sasa namuita Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Charles Mwijage.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii mimi yangu ni machache, ninakuja kuwaeleza kwamba tunakwenda kwenye kujenga uchumi wa viwanda na nakuja kuwahakikishia kwamba uwezo wa kujenga uchumi wa viwanda tunao, na sekta itakayoongoza ujenzi wa uchumi wa viwanda mhimili wetu ni sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda mbele nichukue fursa hii kwako wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge niwakaribishe kwenye maeneo ya 40 kwenye Saba Saba *Mwalimu Nyerere Dar es Salaam International Trade Fair* ya 40 itafanyika kuanzia tarehe 1; karibuni nyote mtaingia na *VIP pass. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianzie pale alipoishia Mheshimiwa Makamba. Dhamana niliyopewa ni kuhakikisha kwamba kunakuwepo wepesi wa kufanya shughuli, ni wepesi wa kufanya biashara jambo ambalo ninalisimamia mimi litakalowawezesha wawekezaji kuja hapa, mengine yote yatafuata baadaye. Ikitokea hakuna wepesi wa kufanya biashara mimi nitalaumiwa lakini mimi ndiyo mdogo nitawakumbusha Mawaziri wote kwamba wawekezaji wote tuwape wepesi wa kufanya biashara, mengine ya kodi yanafuata baadaye, kinachotangulia ni wepesi wa kufanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la mitumba ambalo mama yangu alilizungumza, hatuna dhamira ya kuwafanya Watanzania watembee uchi, tunajenga uchumi wa viwanda, viwanda vyangu vya nguo ambavyo vinazalisha 40% viende kwenye 100% na tunatengeneza nguo kusudi watu wavae na tunaanza kuwavika watoto wa nyumbani kabla ya kuuza nje. Kwa

hiyo, kama tunawavika watoto wa nyumbani hawawezi kuvaa mitumba msiwaombee Watanzania kuvaa mitumba, kwa nini tumeongeza tozo kwenye mitumba, tumeongeza tozo kwenye mitumba tunawa-*beep* wenye viwanda kwamba sasa tunawalinda, zalisha nguo nzuri, watu wetu wavae na mitumba itapigwa marufuku yenyewe katika miaka mitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie mafuta ya kula. Sekta ya mafuta ya kula *(the edible oil)*, mbegu zinazotengeneza mafuta ya kula ukianzia migaze, ukaja karanga, alizeti zinaajiri watu milioni 1.5 lakini Tanzania tunahitaji laki nne mafuta ya kula, sasa mafuta yanalimwa nchini hayafiki 70,000, kiburi chetu ni kwamba tujenge ujasiri wazalishe kiasi hiki kama 70,000, zinatengeneza ajira milioni 1.5 laki nne itatengeneza kiasi gani ndipo mimi nitakpopata ajira ya Watanzania, wenye viwanda vya mafuta Tanzania msikate tamaa, najua wasiwasi wenu ni kwamba mafuta kutoka Kenya na Uganda yatakuwa na advantage kwa sababu kwao yanaingia kwa sifuri, ngoja niwaeleze.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tarehe 1 Julai, mafuta yatakayoingia Tanzania ambayo hayakupitia kwenye viwanda vya Watanzania wale watatu yatalipishwa asilimia 25 na asilimia 18 nimemwambia Waziri wa Fedha kwamba tuhakikishe mafuta yanayotoka Kenya na Uganda kuingia Tanzania yanalipishwa zaidi kusudi viwanda vya Tanzania viweze kupata *advantage*. Wenye viwanda nitawalinda, leteni habari kwangu niweze kuwapa wepesi wa kufanya shughuli. Lakini siwafichi nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wa Kigoma kwa mara ya nne mkiweza kuzalisha migaze kwenye hekari laki moja tutaweza kuzalisha mafuta ya kuweza kutosheleza mafuta yetu. Tunapojenga *standard gauge rail* kwenda Kigoma maana yake ni nini, treni ikipanda na mizigo ya Congo irudi na mawese kwenye viwanda vya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limekuwepo swali tata watu wanasema Mwijage umepewa shilingi bilioni 40 utajengaje uchumi wa viwanda? Nitaujenga hivi Jimbo la Jiangsu juzi walikuja kumuona tajiri namba moja, wameahidi kwamba wataleta dola trilioni tano kujenga viwanda, ndiyo maana nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji ameandamana kuja kwangu na nimemwambia anipe hekta 15,000 nitamletea mtengenezaji wa kiwanda cha sukari kuzalisha tani 150,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Makamba, ngoja nikueleze muingie kwenye benzi hii, muingie kwenye treni hii tunaondoka atakayekataa kujiunga na sisi atajuta na kusaga meno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba bajeti hii ipite, nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Simbachawene ametoa maelekezo kwenye Wilaya yote na Mikoa kutenga maeneo ya uwekezaji natoa mimi maelekezo kwa wale

walio chini yangu *SIDO* ndiyo itakuwa *gateway,* na Serikali ya China sisi tuna marafiki zetu bwana, Serikali ya China watatoa dola milioni 100 kusaidia viwanda vidogo zinakuja kwangu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge *SIDO* ndiyo itakuwa *gateway,* tutatafuta mbinu zote kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi kusudi Watanzania wote waweze kwenda vizuri.

Niwaeleze moja, pacha yangu amekwenda Mambo ya Ndani, tumedhamiria kwamba kiwanda cha *Karanga Prison,* tutawapatia vifaa kutoka Wizarani kwangu kupitia *TIB* watengeneze *sole* za viatu ili ngozi zinazotengenezwa Tanzania zitengeneze viatu tuanze kuvaa viatu na kabla Bunge lako halijaisha watu wa *Karanga Prison,* watu wa *Imo Tannaries* watakuja kuonyesha viatu vinavyozalishwa, viatu vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa uchumi wa viwanda ni lazima tukubali sisi wenyewe kuvaa bidhaa zetu, ukipende chako kabla wenzako hawajakipenda na kama nilivyowaeleza ujenzi wa uchumi wa viwanda ni vita hakuna anayecheka kwenye vita wote tunune tujenga uchumi wa viwanda, tuongeze *GDP*. Kama alivyosema Profesa Muhongo, *GDB* ikikua ukigawanya kwa watu wetu unapata dola 3000 kwa kila mtu, ifikapo 2025 Tanzania inakuwa uchumi wa kati, uchumi ambao mambo ya umaskini na ujinga itakuwa ni historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwijage nadhani kila Mbunge hapa anasubiria kiwanda jimboni kwake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa George Mcheche Masaju, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa hii ya kuchangia, nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia na nianze kusema tu kwamba naunga mkono hoja hii kwa sababu mbili kubwa zifuatazo; kwanza hoja yenyewe iliyoletwa mbele yetu ya bajeti imeandaliwa vizuri kukidhi matarajio na matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni kwamba bajeti ndiyo *interface* kwa kiingereza, wanaita *interface* yaani kiunganishi kati ya wananchi na Serikali yao. Kwa hiyo, mkutano wa bajeti ni mkutano muhimu sana na wananchi wanaufuatilia wanataka kuona kile ambacho Serikali iliahidi kinatekelezwa na kwa sababu hiyo mimi naunga mkono hoja hii na ni kwa sababu ya bajeti hakuna mkutano ambao ni mrefu kuliko mikutano yote isipokuwa mkutano wa bajeti. Katiba ambayo imetoa jukumu kwa Wabunge la kuisimamia na kuishauri

Serikali inapokuwa inatekeleza wajibu wake pia imetoa jukumu kwa Wabunge kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa bajeti na ninawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge, mmefanya kazi kubwa sana ya kuisimamia Serikali yenu na kuishauri ili matarajio ya wananchi mnaowawakilisha yaweze kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mfupi uliopita tumewasikiliza Mawaziri wakitoa mchango wao namna gani watatekeleza zile hoja ambazo zimezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, imezungumzwa hoja hapa kwamba, kwamba sasa hivi hakuna mgawanyo wa Serikali. Hii siyo kweli kwa sababu sisi wote tuna katiba Ibara ya 4 imeweka mgawanyo wa dola, kuna Serikali, inaitwa vyombo vya utendaji, kuna Bunge na mahakama, halafu Katiba hiyo imeendelea kutoa ufafanuzi wa kazi wa kila mhimili na ndiyo maana leo tuko hapa Bungeni, sisi leo hapa tunajadili bajeti ya Serikali na ndiyo jukumu la Bunge, *yes* hapa atuhumu kwa sababu hukumu ni mambo ya mahakama.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Bunge hili unaweza kujiuliza, kama Katiba imeweka utaratibu katika Ibara ya 26 kwamba kila mmoja lazima aifuate na kutii Katiba hii na sheria za nchi na kwamba imetoa fursa mtu yeyote kwenda mahakamani kulinda hifadhi ya Katiba na sheria hiyo iweje leo iseme kwamba kama kungekuwa na hiyo fursa yenyewe au mwanya au viashiria tu kwamba sasa mgawanyo wa madaraka katika hii mihimili mitatu imevunjwa mpaka sasa hivi hakuna kesi yoyote iliyokwishakufunguliwa mahakamani na kwa hiyo, kama kungekuwa na viashiria hivyo mtu yeyote ana haki ya kwenda mahakamani. Kwa hiyo, hii ni hoja ambayo haina msingi na haiwezi ikawa na maana tu kwa sababu kwamba hakuna matangazo ya hadharani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshasema ndani ya Bunge hili kwamba Ibara ya 100 imetoa huru na haki kwa Wabunge huru wa kujadili bila hata mipaka yoyote, siyo uhuru wa kutangazwa, haiwezekani yasipokuwa matangazo ya moja kwa moja ukasema kwamba madaraka ya Bunge yanapokwa au Wabunge wanazuiliwa kujadili, Wabunge wangeweza kuwa wanazuiliwa kujadili leo wasingeweza kujadili wakaishauri Serikali mpaka Serikali ikatoa maelezo kiasi hiki. Ninaloweza kusema pia kwamba kumekuwepo na hoja hapa kwamba Bunge limegeuzwa kuwa *rubber stamp* haiwezekaniki, kwa sababu kwanza mfumo wenyewe Bunge ambalo limepewa mamlaka kwa niaba ya wananchi kuisimamia Katiba litawezaje kuwa *rubber stamp* haiwezekaniki kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha pili kwa hiyo Serikali haiwezi ikapitisha bajeti yake bila Bunge kushiriki na kuamua kwa hiari yao. Lakini mfumo

wenyewe wa maandalizi ya bajeti na utendaji wa Serikali ni kwamba ni shirikishi kwanza unaona katika Katiba yenyewe Ibara ya 63(2)(3) lakini pia sheria kwa sababu hiyo ikatungwa sheria ya bajeti na Sheria ya Bajeti ni shirikishi na kanuni zenyewe unaweka ushirikishi kati ya Serikali na Wabunge kuhusu bajeti. Kwa hiyo, kifungu cha tano na cha sita kinatoa mamlaka kwa mfano kifungu cha tano *fiscal policy object*, halafu cha sita *microeconomic policies* na kifungu cha saba kinasema kutakuwa na uanishaji wa mpango mfupi na mpango mrefu na bajeti sasa inaandaliwa kwa ajili ya mpango wa mwaka mmoja, mmoja. Kwa hiyo, bajeti katika mpango ambao umegawanyika katika kipindi cha mpango mrefu wa miaka mitano inakuja kutekelezwa kupitia mpango wa mwaka mmoja ambao ndiyo unaandaliwa bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana nahoja za Wabunge wana kiu kwa ajili ya maendeleo ya majimbo yao kwa sababu ndiyo hasa, lakini pia kuwakumbusha tu ni kwamba kiu itatimizwa au itakidhiwa haja pale ambapo kila mwaka tunaleta mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji huo. Kwa hiyo, yale ambayo hayakutekelezwa mwaka huu yatatekelezwa mwaka mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo niseme tu kwamba kanuni zenyewe zinaweka ushirikishi na Bunge lenyewe limepewa mamlaka chini ya kifungu cha nane na Kamati ya Bajeti imepewa mamlaka chini ya kifungu cha tisa namna ya kuangalia hivyo. Kwa hiyo, hoja ya kwamba Bunge limebaki *rubber stamp* haiwezekani ikawa ni ya kweli. Kwa hiyo, mimi nimeshiriki mle kwenye Kamati ya Bajeti, nimeshiriki humu Bungeni mnajua mimi siyo Mbunge mtoro, nakuwepo karibu muda wote humu ndani nimeona jinsi ambavyo Wabunge wamechangia sana, wameshauri Serikali yao na Serikali imeitikia vizuri, tumempigia makofi mengi sana hapa Mheshimiwa Mwijage muda mfupi uliopita kuonyesha kwamba Wabunge wametekeleza sana jukumu lao la Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nikushukuru Mheshimiwa Naibu Spika na hili ni la msingi sana, kwenye jambo la msingi sana kama la bajeti linalowaunganisha wananchi na Serikali yao ambayo ndiyo *interface* yao, Bunge hili linahitaji kwa kweli kuendeshwa kwa namna ambayo italiwezesha Bunge lifanikishe utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunapofanya maamuzi haya chombo kinachoendeshwa kwa majadiliano kinahitaji kizingatie Katiba, sheria na kanuni zilizojiwekea. Kwenye hili mimi nakuomba na umefanya vizuri sana kuendelea kulisimamia hivi vizuri kusudi matarajio ya wananchi yaweze kutekelezwa, tunafanya *reform* ambazo lazima ziendane na kuzingatia Katiba na sheria za nchi. Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati hoja ya kumthibitisha Waziri Mkuu alisema juu ya umuhimu wa kuzingatia Katiba na sheria tunapotekeleza majukumu yetu hapa. Kwa hiyo, mimi naomba

sana usikatishwe tamaa, umefanya vizuri na ndio maana Bunge hili linakuja na mapendekezo mazuri sasa. Bunge kama hili la bajeti ambalo ndiyo kiungo cha wananchi na Serikali yao likianza kuvurugwa matarajio ya wananchi yanaenda wapi? Kwa hiyo, usikate tamaa, uwezo unao, nia ya kufanya vizuri unayo na sababu za kuongoza Bunge hili unalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, mtoa hoja.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutufikisha hatua hii siku ya leo. Ni hatua muhimu sana kwa taifa letu na naamini ni kwa rehema zake tu tumeweza kufika hatua hii siku ya leo na naamini kwa pamoja Waheshimiwa Wabunge hatuna budi kusema *Alhamdulillah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mafundisho ya dini yangu baada ya Mwenyezi Mungu huja wazazi wangu. Naomba niwashukuru sana wazazi wangu kwa kunilea vyema na kunifikisha hapa nilipo. Najua kama mtoto wa kike haikuwa rahisi lakini nimeweza kwa sababu walinisaidia, waliniamini na sasa namshukuru Mungu naweza kuwatumikia Watanzania kwa ujumla. Pamoja na wazazi wangu wapo dada zangu, yupo pacha wangu, nawashukuruni sana kwa kuendelea kunipa *support*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru watoto wangu wapendwa, Samira na Abubakar, nasema ahsanteni sana. Naamini bado ni wadogo mnahitaji kuwa na mimi lakini mmeniruhusu na ninaweza kusimama na kuwatumikia Watanzania. Ahsanteni sana na nawapenda sana watoto wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa sasa naomba nimshukuru mume wangu mpenzi. *(Makofi/Vigelegele)*

MBUNGE FULANI: Shemeji!

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa kipekee kabisa. Safari ya ndoa yetu ilianza mbali tukiwa wanafunzi Chuo Kikuu Mzumbe, tumekwenda pamoja mpaka tunapata *PhD* yetu, yeye kapata leo na mimi nimepata kesho. Ahsante sana mume wangu. Nakushukuru sana kwa mapenzi yako kwangu, kwa ushauri wako kwangu kama Mchumi, naamini kwa pamoja tutafika salama na nakuahidi mapenzi yangu ya dhati kwako, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa ujasiri wako kama mwanamke, kwa weledi wako katika utendaji wako wa kazi na umetufikisha leo siku hii ya mwisho ya kujadili bajeti ya Serikali yetu. Hongera sana, endelea kusimama imara. Wewe bado mdogo sana, nafasi yako ni kubwa na utafika pakubwa zaidi ya hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu bunifu kabisa, tumeipokea kwa mikono miwili na tutaifanyia kazi. Naamini haitakuwa rahisi kujibu hoja zote hapa mbele lakini naamini tutazijibu zote kwa maandishi. La muhimu zaidi ni kuyafanyia kazi mawazo yenu yote ambayo mmetupatia kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wetu na taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijibu baadhi ya hoja na hoja ya kwanza ambayo ilisisitizwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wakiongozwa na Mheshimiwa Andrew Chenge, namheshimu sana Mheshimiwa Andrew Chenge, nayo ilikuwa ni Serikali itumie mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti ya *Chenge One* ili kuongeza wigo wa mapato na uendelezaji wa sekta ya viwanda. Naomba kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu ni sikivu sana, ilizingatia sehemu kubwa ya mapendekezo ya ripoti ya *Chenge One* tangu ilipotolewa hadi kufikia hivi leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitasema baadhi tu ya mambo ambayo Serikali yetu imeshayatekeleza. Jambo la kwanza kabisa lilikuwa ni *TRA* kuyafanyia kazi kwa wakati taarifa za Wakala wa Ukaguzi wa Madini (TMAA). Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali yetu kupitia *TRA* imekuwa ikitumia ripoti za ukaguzi wa hesabu za *TMAA* kama nyenzo mojawapo muhimu katika mchakato wa ukaguzi na ugunduzi wa maeneo hatarishi. Tunafahamu Waheshimiwa Wabunge na mmeyasema kwa nguvu zote kwamba katika eneo tunalodanganywa sana ni sekta ya madini. Kwa kushirikiana na *TMAA, TRA* tumeweza kugundua mambo mengi na tunaendelea kuyafanyia kazi na ndipo mnapoona hata makusanyo ya Serikali yetu yakizidi kuimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ilikuwa ni kuanzisha kodi katika usafirishaji wa fedha kwa njia ya simu za mkononi. Serikali yetu katika hatua hii ilizingatiwa kwenye mapendekezo ya hatua mpya za kodi kwa mwaka 2013/2014. Waheshimiwa Wabunge mliokuwemo kwenye Bunge hili kipindi hicho mliona na katika mwaka huu wa fedha naamini sote tunakumbuka Serikali imewasilisha maboresho ya hatua hii kwa kupendekeza kutoza ushuru wa bidhaa kwa asilimia kumi kwenye ada zinazotozwa na watoa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewane. Asilimia kumi hii ni kwa ada zile zinazotozwa na watoa huduma na si kwenye pesa anayoituma Mtanzania kwenda kwa Mtanzania mwingine. Hivyo, naomba

tupeleke ujumbe huu kwa wananchi wetu, Serikali ina dhamira nzuri kabisa kwa Watanzania, kuwawezesha kiuchumi waweze kusimama imara, hivyo ada hii haiendi kuwa ni mzigo kwa wananchi bali sasa tunataka na makampuni yale yalipe kodi stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika ripoti ya *Chenge One* ilikuwa ni kuanzisha ada ya utumiaji wa kadi za simu *(sim card)*. Kama tutakavyokumbuka, hatua hii tuliichukua kipindi kilichopita lakini pamoja na kuichukua na kuiwasilisha hapa Bungeni ilikumbana na vikwazo vingi kutoka kwa wadau na hivyo Serikali kuamua kuchukua hatua ya kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye huduma za simu hadi kufikia kiwango cha sasa cha asilimia 17. Naomba tufahamu kwamba unapokua sokoni kwa sisi Wachumi tunafahamu, kunapokuwa na *win-lose situation* wewe ndiwe utapoteza zaidi hivyo tuliweza kuihamishia kodi hii upande huu na kuthibitisha kwamba ripoti ya *Chenge One* tunaendelea kuifanyia kazi hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lilikuwa ni kuimarisha usimamizi wa utozaji wa kodi katika makampuni ya simu. Serikali yetu sikivu kama kawaida imelifanyia kazi suala hili ambapo mtambo wa *telecommunication traffic monitoring system* tayari umefungwa na umeanza kutumika. Hivi sasa Serikali inaendelea kuweka mfumo wa kutambua aina na kiasi halisi cha miamala na thamani ya miamala inayofanywa na makampuni ya simu. Aidha, Mamlaka yetu ya Mapato wataendelea kufanya kazi kwa karibu sana na Mamlaka ya Mawasiliano *(TCRA)* ili kukagua hesabu za makampuni ya simu katika kuhakikisha kuwa kodi stahiki zinalipwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumelifanyia kazi lilikuwa ni pendekezo la kupunguza kiasi cha misamaha ya kodi hatua kwa hatua hadi kufikia asilimia moja ya *GDP* ambapo tunafahamu misamaha imeendelea kushuka. Kwa historia tu, katika mwaka 2012/2013 misamaha hiyo ilishuka hadi kufikia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa, asilimia 2.3 ya Pato la Taifa katika mwaka 2013/2014 na asilimia 1.9 ya Pato la Taifa katika mwaka 2014/2015. Serikali inaendelea na juhudi hii ya kupunguza misamaha hasa ile isiyokuwa na tija na hivyo ifikie walau asilimia moja ya Pato la Taifa katika muda wa kati na mfupi ujao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwamba hadi kufikia Juni 30, 2016 wiki moja ijayo, ni matarajio ya Serikali kwamba misamaha itakuwa chini ya asilimia moja, tutakuwa ndani ya 0.84 ya Pato la Taifa. Hivyo ripoti cha *Chenge One* Serikali yetu imeendelea kuifanyia kazi vizuri hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme hayo yanatosha katika ripoti ya *Chenge One* lakini yapo mengi ambayo tumekuwa tukiyafanyia kazi na kwa pamoja tutashirikiana. Kama nilivyosema tutawajibu kwa maandishi na mtaona ni hatua zipi nyingine ambazo zimefikiwa katika kuifanyia kazi ripoti hii ya *Chenge One* kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu na wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa Wizara ya Fedha na Mipango na Benki Kuu ya Tanzania wasimamie na kudhibiti mfumuko wa bei na riba za mikopo. Katika suala la kudhibiti riba za mikopo, Serikali yetu pia inafahamu hili ni tatizo kubwa, linawaumiza wananchi wetu. Pamoja na kuliachia suala hili katika soko lakini pia mkono wa Serikali bado uko pale pale na zifuatazo ni sehemu tu ya hatua tunazochukua kama Serikali kuhakikisha kwamba riba inakuwa si ile inayoumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, tunaendelea na usimamizi imara wa sera za fedha na bajeti *(monitory policy and fiscal policy),* tunaendelea kuzifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba riba hizi haziendi kuwa ni mzigo kwa wananchi. Jambo la pili, Serikali imeendelea kuhamasisha benki za biashara kutumia takwimu za *Credit Reference Bureau* kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za historia na uaminifu wa wakopaji. Kupitia njia hii ni imani yetu kwamba kama benki hizo za biashara zitaweza kutumia *statistics* zilizopo katika kitengo hiki itakuwa ni rahisi kufahamu historia ya wateja wao na hivyo haitakuwa jambo jema kuona tena riba ile inapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kulifikia jambo hili, Serikali pia inaendelea kukamilisha mradi wa vitambulisho vya taifa kwa sababu tunafahamu moja ya kitu kinachosababisha riba iwe kubwa ni pale benki au mkopeshaji hana taarifa sahihi za mtumiaji wa huduma hii. Kwa hiyo, tunaendelea kukamilisha vitambulisho vya taifa, nina imani kubwa sasa kila Mtanzania atajulikana yuko wapi na benki hizi zitakuwa na uhakika wanamkopesha nani na yuko wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili pia Serikali inaendelea kusimamia uandikishwaji wa hati za umilikishwaji wa viwanja kwa Watanzania ili kuwawezesha wananchi kuwa na dhamana wanapohitaji kukopa. Pia Serikali inaendelea kuboresha soko la dhamana za Serikali na soko la jumla la fedha za kigeni ili kuongeza ushindani katika masoko. Pia Serikali yetu inaendelea kuimarisha benki maalum za maendeleo ambazo ni Benki yetu ya Kilimo na Benki ya Maendeleo ya *TIB* ili ziweze kutoa huduma kwa wahusika na kwa riba ambayo ni sahihi ambayo Watanzania wengi hawataumia. Huo ulikuwa ni mpango wa kudhibiti riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti mfumuko wa bei, Serikali imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei ambapo kwa muda wa kati umebaki

kiwango cha wastani wa tarakimu moja. Aidha, kwa mwaka 2015 kiwango kilikuwa wastani wa asilimia 5.6. Pia katika kudhibiti mfumuko huu wa bei Serikali itaendelea kuhakikisha kwanza ujazi wa fedha kwenye uchumi unakuwa sawia na ukuaji wa shughuli za kiuchumi ili upande mmoja usije ukazidi upande mwingine na hatimaye kupelekea madhara yake kwenye mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Serikali itaendelea kutoa chakula kwa bei nafuu kupitia Hifadhi ya Taifa ya Chakula kwenye maeneo yenye upungufu wa chakula kwa sababu tunafahamu sehemu moja kubwa inayopelekea kuongezeka kwa mfumuko wa bei ni bei ya chakula. Hivyo, tumejipanga vizuri katika suala hili na tuna imani kubwa mfumuko wa bei utaendelea kubaki katika tarakimu moja. Pia Serikali itaendelea kudhibiti bei za nishati ya mafuta na pia kuvutia na kuhimiza uongezaji wa tija katika kila nyanja za uzalishaji na utoaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo napenda kuitolea ufafanuzi ilisema utajiri wa madini bado haujawanufaisha wananchi hivyo Serikali inapoteza mapato mengi katika *transfer pricing* na *mis-invoicing*. Serikali ijenge uwezo wa watumishi kuongeza mapato kwenye sekta ya madini. Katika suala hili Serikali yetu pia imeendelea kulifanyia kazi kwa umakini kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika na sekta hii ya madini. Kama nilivyosema tuna ushirikiano wa karibu kati ya *TMAA* na *TRA* na katika hili *TRA* tumeendelea kuijengea uwezo ambapo *TRA* ilianzisha Kitengo cha Kodi za Kimataifa *(International Taxation Unit)* mwisho wa mwaka 2011. Kitengo hiki kimeendelea kujengewa uwezo kupitia mafunzo ya kiutaalam ndani na nje ya nchi yetu. Mafunzo haya yalidhaminiwa na Serikali ya Norway kupitia *Norwegian Tax Agency* ambapo walitoa fedha ya mafunzo na Serikali ya Marekani kupitia *US Treasury* ambao wanaendelea kuleta mtaalam *wa transfer pricing*. Tunawashukuru watu wa Norway pamoja na Serikali ya Marekani kwa kuendelea kutujengea uwezo katika hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kuimarisha uwezo wa kiutaalam kwenye kitengo hiki *TRA* imenunua haki ya kutumia *(transfer pricing data base)* itakayowezesha kupata taarifa mbalimbali za kulinganisha, *that is comparable data* kwa ajili ya upatikanaji wa taarifa na kurahisisha ukokotoaji wa kodi. Vilevile *TRA* kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha imetengeneza kanuni za *transfer pricing* pamoja na *transfer pricing guidelines* kwa ajili ya kutoa mwongozo wa jinsi ya kukokotoa kodi. Hivyo, tuna imani kubwa kabisa kupitia vitengo hivi na jitihada hizi tatizo hili litaondoka na Watanzania wataweza kunufaika na sekta hii ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya wataalam wetu kupata utaalam huu kwa sasa wataalam wa kitengo hiki wanaendelea na ukaguzi katika makampuni matatu ya madini katika eneo hili la *transfer pricing*. Kazi hii

inatajaria kukamilika katika robo ya kwanza ya 2016/2017 na tutaona wazi mbivu na mbichi ni zipi na Watanzania haki yao iko wapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *TRA* imeshajiunga na Shirika la Kimataifa la *OECD Global Forum* pamoja na *Africa Tax Administration Forum* na inaendelea na mchakato wa kusaini makubaliano ya kubadilishana habari za kodi. Hii inaturahisishia kujua ni kiasi gani kimetoka Tanzania bila sisi kujua katika *black market* na tuweze kuelewa nini cha kufanya na jinsi gani ya kupata kodi yetu stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kuhakikisha kuwa maeneo yanayohitaji weledi maalum yanapata wataalam wa aina hii ya kuyasimamia *TRA* pia hubadilishana uwezo na mamlaka nyingine za mapato na mamlaka za udhibiti nchini zinazohusika na usimamizi wa mapato na taasisi na idara nyingine za Serikali kama vile *TCRA, TMAA, Contractors Registrations Board, TANROADS* na kadhalika. Hali kadhalika, Serikali inaendelea na jitihada za kukiimarisha kitengo hili ili kuwa na wataalam wengi zaidi kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za kikodi zinazoendelea kuibuka katika eneo hili la kodi za kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulitolea ufafanuzi ilikuwa Serikali itatumia utaratibu gani kuhakikisha kuwa majukumu ya taasisi zilizokuwa zikijiendesha kwa fedha za *retention* hayaathiriki. Napenda kulithibitia Bunge lako Tukufu kwamba nia ya Serikali ni njema katika eneo hili, imedhamiria kuhakikisha sasa mapato yote ya Serikali yanatumika kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu. Napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba taasisi zote zilizokuwa kwenye utaratibu wa *retention* zitatakiwa sasa kuwasilisha mahitaji ya bajeti kila mwaka kulingana na kalenda ya uandaaji wa bajeti. Serikali itachambua mahitaji ya taasisi husika na kisha kupangiwa ukomo wa Bajeti. Aidha, Wizara ya Fedha na Mipango itahakikisha kwamba bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya taasisi hizi na migao ya fedha kutoka Mfuko Mkuu inatolewa bila kuchelewa ili tusikwamishe utendaji kazi wa taasisi zetu hizi. Tunafahamu umuhimu wa majukumu yao na hivyo, hatutachelewesha fedha kuzipelekea taasisi zetu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hii italeta usawa katika matumizi ya taasisi zetu na kuzuia matumizi yasiyo ya lazima kwa taasisi zote za taifa letu. Nia ya Serikali yetu ni njema kama nilivyosema mwanzo, naomba Waheshimiwa Wabunge muendelee kutuunga mkono. Hii ni tiba sahihi sana ya lile ambalo tulilisikia huko nyuma kwamba zipo taasisi zilizokwenda kufanyiwa mikutano yao ya bodi nje ya nchi, hatuna sababu ya kufanya hivyo. Kama mchumi ukiwa na pesa ambayo unaiona ni nyingi huna matumizi unaweza kutumia vyovyote vile lakini kwa mfumo huu ni imani yangu sasa tutarejesha nidhamu ya matumizi ya

pesa za Serikali na pesa hizi ziweze kuleta tija kwa wananchi wetu hasa wa kipato cha chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni Serikali ilete Muswada wa Sheria ambapo itaanzisha mamlaka ya kusimamia na kudhibiti taasisi ndogo za fedha nchini. Serikali inakamilisha Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha. Sera hiyo itawezeshwa kutungwa kwa Sheria ya Kusimamia Taasisi Zinazotoa Huduma Ndogondogo za Fedha *(The Microfinance Act)*. Sheria hii itaanzisha Mamlaka za Kusimamia na Kudhibiti Taasisi hizo kwa kutumia madaraja kama, moja, tutakuwa na udhibiti wa taasisi ndogo za fedha zinazopokea amana kwa wananchi (*deposit taking microfinance institutions)* utakaosimamiwa moja kwa moja na Benki Kuu ya Tanzania. Mbili, tutakuwa na udhibiti wa taasisi za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana kutoka kwa wananchi (*non deposit taking microfinance institutions)*. Pamoja na programu na mifuko maalum ya Serikali ya kuwezesha wananchi kiuchumi itakuwa chini ya taasisi hizi na chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kutakuwepo na udhibiti wa huduma za fedha zinazotolewa na vyama vya ushirika wa akiba na mikopo chini ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania. Mwisho, udhibiti wa huduma za fedha zinazotolewa na vikundi kama vile *Village Community Banks (VICOBA), Voluntary Savings Loans Association, Rotating Savings and Credit Association* na watu binafsi wanaotoa mikopo na kuweka akiba yaani *money lenders and saving collectors* chini ya mamlaka ya Serikali za Mitaa. Sheria hii pia itaainisha vigezo na masharti ya ukuaji wa taasisi hizo kutoka daraja moja kwenda daraja lingine ili kuwa na udhibiti imara na ukuaji endelevu wa sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulichowaahidi Waheshimiwa Wabunge wakati tunawasilisha bajeti ya Wizara ya Fedha tutamiza ahadi hii ili wananchi wetu waondokane na adha ya usumbufu wa mfumo usio rasmi katika sekta ya fedha. Tunafahamu waathirika wakubwa ni akina mama katika hili na ni imani yangu kubwa tutalisimamia kwa uhakika kabisa ili akina mama waondokane na adha hii ya kukopeshwa bila kuwa mtu yeyote anayeratibu taratibu hizi ili akina mama hawa waondokane na lindi la umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ambayo napenda kuitolea ufafanuzi ni kwa nini Serikali hailipi madeni inayodaiwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii takribani shilingi trilioni 8.942? Waheshimiwa Wabunge kama mnakumbuka nimekuwa nikilisemea jambo hili kwa nguvu zangu zote na tumeji-*commit* kama Serikali. Naomba tufahamu kwamba katika mapitio ya awali yaliyofanyika, yalionesha kwamba madai ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii yalifikia jumla ya shilingi trilioni 3.89 hadi Juni, 2015. Madai haya yanajumuisha deni la *PSPF* la kabla ya mwaka 1999 la shilingi trilioni 2.67 na shilingi trilioni 1.22 kwa ajili ya

madai ya mifuko yote yaliyotokana na uwekezaji katika miradi mbalimbali ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina nia ya dhati ya kulipa madeni haya yote ili kuimarisha Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii mara tu baada ya kukamilisha uhakiki wa madai hayo. Tunafahamu tumekuwa na tatizo la wafanyakazi hewa na tumemsikia Mheshimiwa Rais wetu amesema, unapokuwa na wafanyakazi hewa utakuwa na wastaafu hewa pia. Hivyo, tunaendelea kuhakiki hatua kwa hatua tutafika mwisho mzuri na mifuko yetu ya hifadhi ya jamii itaweza kufanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mmojawapo katika hili hadi kufikia Mei, 2016 uhakiki wa madai ya mfuko wa *PSPF* ulikuwa umekamilika ambapo kiasi kilichokubalika ni shilingi trilioni 2.04 kutoka madai ya awali ya shilingi trilioni 2.67, kuonyesha kwamba kulikuwa na madai hewa katika wastaafu hawa. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuipatie Serikali yetu muda tukamilishe uhakiki huo ambao umeanza kufanywa na Mkuguzi wetu wa Ndani wa Serikali ili tuweze kuondokana na madeni tata na tuweze kulipa kile tunachostahili kukilipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha majibu ya hoja zangu kwa maneno yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika na Bunge lako Tukufu, naomba tufahamu kwamba uchumi wa Tanzania ya viwanda kama alivyosema shemeji yangu Mwijage haupo mikononi mwa vijana wanywa viroba na watafuna mirungi bali mikononi mwa vijana walio tayari kabisa kuingia kwenye uchumi wa kati kiakili na kimwili. *Very aggressive to take and tape opportunities that are ahead of us in our country*. Kama Wabunge na wawakilishi wa wananchi tuna jukumu la kurejea majimboni mwetu na kuwaandaa vijana wetu wa Tanzania kwa Tanzania ya viwanda iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha ya vijana wetu hayapo kwenye bangi na *pool table,* hapana, bali yapo mikononi mwa mama yao Tanzania chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Magufuli na Serikali yake ambayo imelenga kwenye ubunifu utakaoleta fursa za kiuchumi kwa vijana wetu. Yapo mikononi mwa Serikali makini ambapo ipo tayari kutengeneza ajira kwa ajili ya watu wake. Serikali yetu ipo tayari kwa hayo yote, naomba tuwaandae Watanzania kuingia kwenye uchumi wa kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mratibu na msimamizi wa sera za uchumi mpana (*micro-economic policies)*, Wizara ya Fedha na Mipango tutafanya kila linalowezekana kuhakikisha tunakuwa na ufanisi katika soko la fedha (*Money market*), soko la ajira *(labor market)* na soko la bidhaa (*commodity market)*.

Masoko haya yote matatu yanategemeana, yanatafsiri pia juhudi zetu za kuelekea uchumi wa kati na yanaathiri au yanaathari za moja kwa moja katika maisha ya Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utayari wetu Waheshimiwa Wabunge wa kulipa kodi kwa hiari ni njia pekee ya kutufikisha katika maendeleo endelevu na uchumi wa kati. Hivyo, ni lazima tuangalie kwa umakini rasilimali zetu tulizonazo ndani ya nchi yetu na kuzitumia kwa ufanisi katika kuleta maendeleo ya uchumi jumla *(inclusive growth)*. Hii ni pamoja na kuongeza wigo wa vyanzo vyetu vya mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia kwa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa ujasiri, uvumilivu na umakini wake katika utendaji wa kazi zake. Naomba nikuambie Mheshimiwa Waziri, mti wenye matunda ndiyo hupigwa mawe, usikate tamaa endelea kwenda mbele. Najifunza mengi kutoka kwako, endelea kunilea na kunijenga, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipngo, Mheshimiwa Dokta Philip Mpango.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumshukuru Mungu kwa kuniruhusu kusimama hapa ili kuhitimisha mjadala wa Bunge lako Tukufu kuhusu Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa ya mwaka 2015, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 niliyoyawasilisha tarehe 8 Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nakupongeza sana kwa umahiri na weledi wa hali ya juu ulioonesha katika kusimamia Kanuni za Bunge wakati wote wa kikao hiki cha Bunge la Bajeti. Hakika viwango vyako ni vya kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa Mheshimiwa Kakunda, mwanafunzi wangu wa Idara ya Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alichomekea sehemu fulani akidai kwamba mimi ni bahiri. Nadhani alimaanisha kwamba ni bahari wa kutoa maksi za upendeleo. Nataka niliambie Bunge lako Tukufu kwamba viwango vyako Mheshimiwa Naibu Spika ambavyo umevionyesha humu ndani hakika ningekuwa bado niko kule chuoni ningekupatia maksi za haki, asilimia 100 kama walivyofanya Maprofesa wako wa Sheria pale Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini pia *University of Cape town*, hongera sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutambua michango iliyotolewa na Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Japokuwa ameingia mitini, napenda pia kutambua mchango wa Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Fedha na Mipango lakini pia michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa kuzungumza au kwa maandishi hapa Bungeni, nawashukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Wabunge 171 wamechangia hoja niliyowasilisha. Kati ya hao, 146 wamechangia kwa kuzungumza na 25 kwa maandishi. Napenda kuwashukuru wote. Pia niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri tisa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali waliochangia asubuhi hii. Kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Dokta Ashatu Kachwamba Kijaji kwa kunisaidia kujibu hoja kwa umahiri mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hatua ambazo zilipongezwa na Wabunge wengi wakati wa mjadala huu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017. Moja ambalo Waheshimiwa Wabunge mlilisema na kulipongeza ni Serikali kuthubutu kuweka lengo la bajeti ya shilingi trilioni 29.5 ikilinganishwa na shilingi trilioni 22.5 mwaka huu fedha tunaomalizia na kati ya hizo kutenga asilimia 40 ya bajeti yote kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Miradi hii ya maendeleo ni pamoja na uthubutu wa kuanza kujenga reli mpya ya kati kwa kiwango cha *standard gauge,* barabara, umeme, ununuzi wa meli mpya na ndege tatu za abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Waheshimiwa Wabunge walipongeza sana uamuzi wa Serikali kuongeza nguvu katika ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi na hadi sasa tumefikia wastani wa shilingi trilioni 1.2 kwa mwezi kwa kuziba mianya ya uvujaji wa mapato na kuimarisha matumizi ya vifaa vya kieletroniki *(EFDs)*. Pia Waheshimiwa Wabunge walipongeza uamuzi wa Serikali wa kusimamia nidhamu ya matumizi na kupunguza matumizi yasiyo ya lazima na kuelekeza fedha hizo kwenye miradi ya maendeleo. Pamoja na mambo mengine Waheshimiwa Wabunge wamepongeza azma ya kufanya kazi na kurejesha nidhamu ya watumishi kazini kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengine mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge walipongeza. Napenda nimalizie tu na moja la mwisho ambalo ni azma ya Serikali kujielekeza kutekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2015, ahadi za Viongozi Wakuu na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2020-2025 ili kutatua kero za wananchi hasa masikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Waheshimiwa Wabunge walitoa ushauri katika maeneo mbalimbali, nitazungumzia machache. Moja, Waheshimiwa Wabunge wameshauri kuongeza tozo ya mafuta ili mapato hayo yatumike kupanua huduma za maji na kukamilisha vituo vya afya na zahanati vijiji. Pia walishauri kwamba mfumo wa kodi uboreshwe ikiwa ni pamoja na kufuta kodi zaidi, ushuru na tozo za kero kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyabiashara hasa wadogo. Pia kutoa ahueni ya kodi kwenye taulo za akina mama na vifaa vya watu wenye ulemavu, vifaa vya michezo, zana za uvuvi na kulinda viwanda vya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walishauri kwamba ni muhimu kuimarisha elimu na kuhakikisha inaendana na mahitaji na wataalam wa Tanzania ya leo na kesho. Walishauri Serikali ichukue hatua za ziada kuimarisha sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi na hususan kuongeza kilimo cha umwagiliaji, pembejeo, ugani, utafiti, mnyororo wa thamani, masoko, ruzuku, mikopo na bajeti ya kilimo. Waheshimiwa Wabunge waliishauri Serikali ipanue wigo wa kodi hasa katika sekta ambazo zina mapato makubwa kama mawasiliano, madini, maliasili na ardhi na sekta zenye fursa kama uvuvi na biashara kwenda nchi jirani lakini pia *e-commerce,* gawio kutoka kwenye mashirika ya umma na kuhakikisha kila mwananachi analipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri uliotolewa ni mwingi sana na mzuri na Serikali itauzingatia katika bajeti hii na bajeti zinazokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nianze kufafanua baadhi ya hoja na kama nilivyosema michango ilikuwa mingi haitakuwa rahisi kujibu hoja zote pamoja na zile zilizojibiwa na Waheshimiwa Mawaziri, nitajibu chache tu. Najua hoja hizi nyingine zilielezwa kwa hisia kali na wengine walinikaribisha Bungeni wakisema Waziri wa Fedha na Mipango amewa-*beep* Waheshimiwa Wabunge na wengine walisema Waziri wa Fedha hana jimbo ndiyo maana haoni machungu. Mimi nadhani walikuwa wananikaribisha tu Bungeni, kazi ya Waziri wa Fedha ina changamoto nyingi, inanilazimu niwe mtu ambaye hana maneno matamu tu lakini matupu, inanilazimu niwe mkweli na kuwaeleza kile ambacho kinawezekana na kile kisichowezekana ili kujenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja moja ambayo ilisemwa sana ni pendekezo la kuongeza tozo ya Sh.50 kwenye mafuta kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Maji na kukamilisha ujenzi wa vituo vya afya na zahanati vijijini. Niseme tu kwamba hili ni pendekezo ambalo lina lengo zuri na Serikali inalipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni vyema kutambua kwamba kufuatia kupungua kwa bei ya mafuta katika soko la dunia gharama ya mafuta yote ambayo tumeagiza kama taifa kutoka nje imepungua kwa takribani asilimia 20 na imechangia kushuka kwa mfumuko wa bei na sasa mfumuko wa

bei uko asilimia 5.2 na mwenendo huu umeleta ahueni kwa maisha ya wananchi wetu walio wengi. Hata hivyo, Serikali imeamua kwamba kwa wakati huu hatutaongeza tozo kwenye mafuta ili wananchi waendelee kunufaika na huo unafuu wa bei ya mafuta. Ni wazi kwamba ongezeko la tozo katika mafuta ya petroli na dizeli litasababisha kupanda kwa bei ya mafuta jambo ambalo litaongeza gharama ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa chakula na bidhaa ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi na huduma nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwaambie Waheshimiwa Wabunge pia kwamba wataalam wa uchumi wanashauri kwamba katika kipindi ambacho kuna uwepo wa bei ndogo ya mafuta, ni wakati mzuri kwa nchi kuwekeza hususan katika miundombinu, viwanda ambavyo ni *energy intensive* na kuendeleza ujuzi na teknolojia. Kwa hiyo, ndiyo sababu Serikali inaona kwamba ni busara zaidi badala ya kuongeza tozo kwenye mafuta tujielekeze kuongeza bajeti ya kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu ya usafirishaji, nishati na elimu sambamba na kutumia pesa zilizopangwa kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa huduma ya maji nchini ambayo pia ni Ilani ya CCM, tuliongeza bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Maji kutoka shilingi bilioni 373 hadi shilingi bilioni 690.16 kwa mwaka ujao wa fedha. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI alivyoeleza, Serikali inapenda itumie mwaka huu kujipanga na kujua majengo ya afya ambayo yamekwama kwa mwaka huu ili utekelezaji uanze ukiwa umepangwa vizuri mwaka 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni pendekezo la kuondoa msamaha wa kodi ya mapato kwenye kiinua mgongo cha Waheshimiwa Wabunge. Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332, kodi ya mapato inatozwa kwenye vyanzo vyote vya mapato na kiinua mgongo ni chanzo kimojawapo cha mapato kinachotambuliwa na sheria na hutozwa kodi. Kupitia Jedwali la Pili la Sheria ya Kodi ya Mapato kiinua mgongo kinacholipwa kwa Wabunge wakati wanapomaliza muhula wa miaka mitano kimesamehewa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msamaha huu hauzingatii usawa wa utozwaji kodi kwani watu wengine wote wanaopata malipo ya kiinua mgongo, iwe ni sekta binafsi au utumishi wa umma wanatozwa kodi katika mapato hayo. Kwa hiyo, hatua niliyoitangaza tarehe 8 Juni, 2016 imechukuliwa ili kujenga msingi wa usawa na haki katika ulipaji wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kufanya marekebisho hayo hivi sasa ni kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kisheria utakaotumika kukokotoa stahili za Mbunge endapo ukomo wa Mbunge yeyote utatokea katika kipindi cha

kuanzia sasa (Julai 2016) na kuendelea. Pia mabadiliko haya yanafanyika sasa ili kuzingatia msingi wa utozaji kodi ambao unataka kodi iwe inatabirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliarifu Bunge lako Tukufu na wananchi wa Tanzania kwamba siku nilipowasilisha pendekezo hili la kufuta msamaha wa kodi kwenye kiinua mgongo cha Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwanza alinishangaa akasema yeye ni Mtanzania na ni lazima Watanzania wote walipe kodi ili kuijenga nchi yetu. Kwa kuwa kiongozi lazima aongoze kwa mfano, Mheshimiwa Rais alielekeza kuwa yeye ni Mbunge wa Tanzania yote na anapenda awe wa kwanza kukatwa kodi stahiki kwenye mafao yake ya kustaafu. Naomba nirudie, alielekeza kuwa yeye ni Mbunge wa Tanzania nzima na anapenda awe wa kwanza kukatwa kodi yake stahiki kwenye mafao yake ya kustaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napenda kufafanua kwamba marekebisho niliyowasilisha tarehe 8, Juni, 2016 maana yake ni kuwa kiinua mgongo cha viongozi wote wa kisiasa ambao wametajwa kusamehewa kodi chini ya Sheria ya Mafao ya Viongozi wa Kisiasa sasa kitakatwa kodi. Maana yake ni kwamba Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, kiinua mgongo chake kitakatwa kodi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, yeye ni Mbunge wa Ruangwa, kiinua mgongo chake kitakatwa kodi. Mheshimiwa Naibu Spika na wewe kiinua mgongo chako kitakatwa kodi. Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri, sisi wote ni Wabunge, lazima tuongoze kwa mfano, kiinua mgongo chetu kitakatwa kodi. Vivyo hivyo kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, kiinua mgongo chao kitakatwa kodi. Waheshimiwa Wabunge, hii ndiyo dhamana ya uongozi, *we have to lead by example*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, palikuwepo hoja ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwamba imetengewa fedha kidogo na haitaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Wengine walizungumza kwa lugha kali kidogo kwamba Waziri wa Fedha na Mipango ana dhamira gani na *CAG,* je, *CAG* ni adui wa Serikali, la hasha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukomo wa bajeti ya *OC* ilitengwa kwa mafungu mbalimbali kwa kuzingatia maamuzi ya Serikali na mkakati wa kupunguza matumizi ya kawaida ili tuelekeze fedha nyingi zaidi kwenye miradi ya maendeleo. Katika kufikia ukomo wa matumizi mengine kwa Serikali nzima, uchambuzi wa kina ulifanyika ili kubaini mahitaji ya fedha ambayo siyo ya lazima kwa wakati huu na hayawezi kuathiri utendaji. Kwa hiyo, tulitazama yote hayo na fedha ambayo tumeweza kutenga kwa sasa ndiyo hiyo na tuna hakika kabisa kwamba Ofisi ya *CAG* itaendelea kufanya kazi yake ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua umuhimu wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kama ilivyo kwa taasisi nyingine nyeti ikiwemo vyombo vya ulinzi na usalama, mihimili mingine ya dola na uwezo wa kukabiliana na dharura, kama patajitokeza mahitaji ya lazima, napenda tena kusisitiza mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba tutahakikisha kwamba ofisi hiyo haikwami. Mahitaji hayo ya ziada yatazingatiwa wakati wa mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uhuru wa CAG katika kufanya kazi zake ni wa kikatiba na hautaingiliwa. Waziri wa Fedha na Mipango atakuwa mtu wa mwisho kukwamisha kazi za ofisi hiyo ambayo inamsaidia kufichua mchwa wa fedha za umma kwenye Wizara na halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya tathmini ya hali ya umaskini kimkoa. Naomba tu niseme kwamba viashiria vya kupima umaskini nchini huwa vinapatikana kwa kutumia utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ambao unafanyika katika nchi yetu kila baada ya miaka mitano. Utafiti huo kwa mara ya mwisho ulifanyika mwaka 2011/2012. Utafiti huo ukichanganya na taarifa zinazotokana na sensa iliyofanyika mwaka 2012 ndiyo unatuwezesha kuweza kuchambua hali ya umaskini wa kila mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba sababu ambazo zinaeleza kwa nini kiwango cha umaskini katika Mikoa kama Mwanza, Kigoma, Singida, Geita na Kagera ni kikubwa ukilinganisha na Mikoa kama Lindi na Mtwara ni nyingi. Kwanza kwa ujumla umaskini wa kipato ni mkubwa zaidi pale ambapo kuna wananchi wengi zaidi wanaishi vijijini ukilinganisha na mijini. Kwa mfano ukiangalia Mkoa wa Mwanza, mwaka 2000/2001 wakati bado Geita iko humo kiwango cha umaskini kilikuwa ni asilimia 48. Umaskini wa kipato wa Geita kabla ya kugawanywa ulikuwa ni asilimia 62.3 lakini baada ya kutenganishwa kiwango cha umaskini wa kipato katika Mkoa wa Mwanza unateremka lakini kiwango cha umaskini katika Mkoa wa Geita kinaendelea kubakia juu na sababu kubwa ni kwamba wananchi wengi zaidi wa Geita wanaishi vijijini ambapo shughuli zao za uzalishaji mali hazikidhi kupunguza kiwango cha umaskini kwa kasi inayotarajiwa. Ukiangalia wilaya ambazo ziko karibu na miji, kiwango cha umaskini ni kidogo zaidi kuliko kiwango cha umaskini katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, umaskini pia ni lazima uende na hali ya kimaeneo. Kwa mfano, Mkoa wa Kigoma kwa kiasi kikubwa umaskini wa kipato katika mkoa huu unachangiwa na miundombinu hafifu ya usafirishaji ambayo inapunguza fursa ya kufikia masoko. Kigoma pia inabeba mzigo mkubwa sana wa wakimbizi na kusababisha ziada ambayo inazalishwa kutumika kulisha wakimbizi na kupunguza ustawi wa kaya katika mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama ni mkakati, cha kwanza ni kutambua kwamba kuna hilo tatizo na sababu zake lakini pia kujielekeza sasa kufungua fursa katika mikoa na wilaya husika. Pia kuja na *interventions* kama zile za *TASAF* ambazo zinalenga kusaidia kaya maskini kabisa lakini pia miradi ya afya na maji na pia *specific interventions* ambazo zinakwenda kushughulikia matatizo katika maeneo mahsusi kama vile tatizo la mnyauko wa migomba kule Kagera na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tutawasilisha maelezo ya kina kwa maandishi kwa hoja zote ambazo Waheshimiwa Wabunge walizitoa. Naomba nieleze moja kabla ya kuhitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ililetwa hoja hapa kwamba *dollarization* imekuwa ni kero kubwa na inasababisha thamani ya shilingi kuteremka. Naomba tu niseme *dollarization* ni matumizi ya sarafu ya kigeni katika nchi husika sambamba na sarafu ya nchi hiyo. *Dollarization* kitaalam inachochewa na vitu kadhaa hususan mfumuko wa bei kama ni mkubwa lakini pia kama thamani ya sarafu ya nchi husika nayo inateremka lakini katika nchi ambazo hakuna usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Tanzania sababu kubwa ni kwamba tumekuwa na mapato kidogo ya fedha za kigeni lakini pia dola imeongezeka sana nguvu kutokana na kuongezeka kwa uchumi wa Marekani na kuchelewa kupata misaada ya *general budget support*. Kwa kawaida wananchi wanatumia hiyo sarafu ya kigeni ili kujikinga na athari za mfumuko wa bei yaani *they hedge against the inflation risk.* Mazingira mengine ambayo yanachochea *dollarization* kama nilivyosema ni kukosekana utulivu wa kisiasa ambayo sisi bahati nzuri hatuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa hili tatizo linahitaji muda na ukichukua hatua za kiamri, za kiutawala kusema tu sasa kuanzia leo watu wasitumie dola, uzoefu wa nchi mbalimbali ulimwenguni unaonesha kwamba hizo sera hazifanyi kazi. Utatia woga katika uchumi na watu wataanza kukimbiza fedha za kigeni na kuleta matokeo yasiyotarajiwa. Kwa hiyo, mkakati siyo kulazimisha au kudhibiti matumizi ya hizo dola, inatakiwa iende sambamba na sera za kisoko za kudhibiti tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watu ambao wanapenda kusoma wanaweza wakatafuta jarida linapatikana kwenye *internet* '*Dollarization in Sub-Saharan Africa: Experience and Lessons* 2015', inawaonesha *experience* ya nchi nyingine na hatua ambazo walichukua hazikufanikiwa. Kwa hiyo, tunachukua kila tahadhari kuhakikisha tunaendelea kubakia na uchumi wetu tulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwasihi Waheshimiwa Wabunge, kwamba bajeti niliyowasilisha inajielekeza kuanza kazi ngumu ya kuitoa Tanzania kutoka nchi inayotegemea kilimo duni kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, nchi ambayo wananchi wake wameondoka kwenye lindi la umaskini ili twende mbele. Kwa hiyo, yote tunayopanga, katika mipango na bajeti ya Serikali, ni muhimu sana kutanguliza maslahi ya Taifa letu lakini pia maslahi ya Watanzania maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kuikubali bajeti hii, utekelezaji wake utahitaji kujitoa. Mheshimiwa Makamba amesema tutahitaji *sacrifice,* tutahitaji *selfless service to our country*. Tunahitaji kuvuja jasho ili tuweze kuwainua maskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mambo mawili tunaweza kufanya, tunaweza tukaamua kuendelea na mazoea yaani *business as usual* ambayo siyo *option* kwetu lakini njia sahihi ni kuachana na mazoea. Ili kuachana na mazoea lazima tuanze sisi viongozi. Itatubidi tuachane na maslahi binafsi hata kama mara kadhaa inaonekana tunayavisha koti au kilemba cha maslahi ya wengi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba ukae kidogo, naona muda unakimbia.

Waheshimiwa Wabunge, naona Mheshimiwa Waziri anahitaji dakika kadhaa ili aweze kuhitimisha. Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), naongeza nusu saa, kwa hiyo, nadhani atapata dakika chache ili ahitimishe hoja yake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, endelea. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nilikuwa nasema tuna dhamana kubwa ya kuleta mabadiliko makubwa katika kuendesha shughuli zote za umma na matumizi ya rasilimali za Taifa ili tuweze kupiga hatua kubwa za kuitoa nchi yetu katika umaskini. Ni lazima kila mwananchi atambue wajibu wake wa kufanya kazi kwa bidii, kuwa na nidhamu ya hali ya juu katika nyanja zote na uzalendo kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena kuzielekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuzingatia hatua za kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kusimamia matumizi ya Serikali na hatua za kupunguza gharama na kulipa na kuzuia ongezeko la madeni ya Serikali. Serikali ina dhamira ya dhati ya kuchukua hatua hizo na naomba Watanzania watambue kwamba ni lazima kujinyima, kujituma na kuvuja jasho ili kupata maendeleo na kupunguza utegemezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudie tena, wajibu wa kwanza wa kuiendeleza nchi yetu ni ya sisi Watanzania wenyewe, tunazo akili za kutosha na rasilimali nyingi na fursa tele kuweza kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda na ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Nawaomba tena Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono hatua zinazoongozwa na Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kuwa tunaimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, mapato ya kodi na yasiyo ya kodi na kuelekeza matumizi kwenye maeneo yenye tija na hususani ujenzi wa viwanda kwa manufaa ya Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Nabu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono, tutaendelea na hatua nyingine hapo baadaye. Ahsante Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo moja hapa, kuna Mheshimiwa amesahau miwani na peni yake alipokwenda kumtembelea Mheshimiwa Mbaraka Dau. Sasa aliyesahau miwani na peni yake ataifuata ofisi ya walinzi pale nje anaweza akapewa.

Tangazo lingine dogo tu, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa viongozi wote wa siasa wametajwa kwamba viinua mgongo vyao vitakatwa kodi na wewe ukatajwa hapa lakini jirani yako Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Spika, nadhani hao wamesamehewa kwenye kudaiwa kodi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni leo.

(Saa 07.05 Mchana Bunge Lilisitishwa Hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka hoja imehitimishwa asubuhi kwa hiyo zoezi linalofuata sasa hivi tutaelekezana kwa mujibu wa Kanuni zetu. Kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 107, kabla sijasimama kutoa maelezo kidogo, Katibu tusaidie upige kengele ili Wabunge wote waingie humu ndani wale walio nje ili tuweze kuendelea na utaratibu, lakini wakati kengele

ikipigwa nitoe maelezo na wakati huo huo utatusaidia kuhesabu sasa walipo ili tuone kama tunayo *quorum* kwa mujibu wa kanuni.

(Hapa kengele ilipigwa ili kuita Wabunge walioko nje kuingia ukumbini)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati kengele yetu ikiendelea kuita Wabunge wengine ili waingie humu ndani na Katibu akitusaidia kuhesabu, Kanuni ya 107 inatutaka sasa tuanze kufanya maamuzi baada ya zoezi la mjadala kuisha. Kanuni ya107 inaeleza kuhusu utaratibu wa kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Serikali. Kwa sababu tumeshahitimisha mjadala tunatakiwa kufanya uamuzi ambayo ni fasili ya (2), inasema:-

"Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja".

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, hilo ndiyo zoezi tutakalolifanya. Pia zoezi letu hili linazingatia Kanuni ya 77(1) ya Kanuni yetu ambayo pamoja na mambo mengine inaeleza kwamba akidi ya kuanza kwa kikao chetu hiki ambacho ni cha maamuzi leo lazima tuwe nusu ya Wabunge wote. Kwa hiyo, Katibu anaendelea kuhesabu kwamba Wabunge tuko wangapi ili tuanze kazi iliyotuleta mchana huu.

Waheshimiwa Wabunge, pia Ibara ya 94(2) inatuelekeza kwamba kwa sababu tunatakiwa kufanya maamuzi tutaamua kwa kufuata wingi wa kura za Wabunge waliohudhuria. Kwa hiyo, tukishapata idadi ya Wabunge waliohudhuria na kwa kuzingatia ile Kanuni inayotaja akidi yetu basi tutahesabu kura tumepata ngapi halafu tutafanya maamuzi. Ibara ya 94(2) inaendana na Kanuni ya 79(1) na yenyewe inaeleza kwamba uamuzi utatolewa na Wabunge walio wengi waliohudhuria siku hiyo. Kwa hiyo, Katibu anatusaidia kufanya hesabu atatuambia sasa hivi tuko wangapi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini tukumbushane tu wakati namsubiri Katibu hapa na idadi ya Wabunge kamili kwamba majukumu yetu hasa katika zoezi hili la bajeti ni kwamba Serikali imeshauriwa na majukumu yetu yako kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba ambayo inaeleza kuhusu kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa mkutano wa Bunge la bajeti na hili zoezi tulishalifanya. Kanuni ya 107 nimeshawasomea ambapo leo tutaamua sasa kupitisha ama kutokupitisha bajeti ya Serikali kwa kuzingatia vigezo vya akidi. Pia tunakumbushwa tu kwamba Ibara ya 90 ya Katiba, fasili ya 2(b) inaeleza kuhusu kukataliwa kwa bajeti na matokeo yake na uamuzi leo utakuwa ni wa ndiyo au hapana au kukaa kimya. Kwa hiyo, Katibu atuletee idadi halafu tuanze zoezi letu la kupiga kura.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Katibu anamalizia kuhesabu labda tukumbushane tu idadi yetu. Mpaka sasa Wabunge tulionao Kikatiba ni 389. Mheshimiwa Rais atakapokamilisha idadi yake ya Waheshimiwa Wabunge wa Kuteuliwa tutakuwa jumla 393 sasa hivi tuko 389. Maana ya hii namba ni kwamba nusu ya Wabunge wote ni 195, hiyo ndiyo akidi ambayo tunatakiwa kuanza nayo kabla hatujaanza kikao chetu cha kupiga kura. Halafu tutakapopiga kura ili tuseme bajeti imepita lazima iwe na kura zaidi ya 98, kwa sababu ndiyo zaidi ya nusu ya 195. Kwa hiyo, hayo mahesabu ndiyo tunasubiri Katibu atuambie kama humu ndani tayari tunao Wabunge 195 ili tuanze kikao chetu kwa mujibu wa Kanuni ambayo nimekwishawasomea inayohusu akidi kwamba lazima tuwe nusu kwa sababu kikao cha leo ni cha maamuzi.

Waheshimiwa Wabunge, naona Katibu bado anafanya mahesabu. Makatibu mnaotusaidia kuhesabu muangalie na Wabunge wanaoendelea kuingia.

Waheshimiwa Wabunge, nimeshaletewa idadi ya Wabunge tuliopo.

WABUNGE FULANI: Bado wanaingia.

NAIBU SPIKA: Wanaruhusiwa tu kuingia kwa sababu tulitaka kujua kama tunayo akidi ya kuanza kikao lakini Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuendelea kuingia mpaka tutakapoanza kupiga kura. Kwa hiyo, mpaka sasa tunao Wabunge 214. Mtakumbuka nilikuwa nimewaambiwa ili tufikie nusu ni lazima Wabunge wawe 195 kwa hiyo tunaweza kuanza kikao chetu sasa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hesabu hizo, Katibu ataanza utaratibu wa kusoma majina na Waheshimiwa Wabunge majibu ni matatu moja ni ndiyo, lingine ni hapana na lingine ni la kutokuamua. Kwa hiyo, Katibu utusaidie. Mwisho wa hili zoezi tutahesabu kura kama tumeweza kufikia ndiyo za kutosha au hapana za kutosha ili kuikubali ama kuikataa bajeti, Katibu.

Mhe. Job Y. Ndugai ... ... Hakuwepo
Mhe. Kassim M. Majaliwa ... ... Ndiyo
Mhe. Freeman A. Mbowe ... ... Hakuwepo
Mhe. Andrew J. Chenge ... ... Ndiyo
Mhe. Mussa A. Zungu ... ... Ndiyo
Mhe. Najma Murtaza Giga ... ... Ndiyo
Mhe. George M. Masaju ... ... Ndiyo
Mhe. George B. Simbachawene ... ... Ndiyo
Mhe. Angellah J. Kairuki ... ... Ndiyo
Mhe. January Y. Makamba ... ... Ndiyo

Mhe. Jenista J. Mhagama … … … Ndiyo
Mhe. Mwigulu L. Nchemba … … … Ndiyo
Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa … Ndiyo
Mhe. Dkt. Philip I. Mpango … … … Ndiyo
Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo … … Ndiyo
Mhe. Dkt. Harrison G. Mwakyembe … … Ndiyo
Mhe. Dkt. Augustine P. Mahiga … … Hakuwepo
Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi … … … Ndiyo
Mhe. William V. Lukuvi … … … Ndiyo
Mhe. Prof. Jumanne A. Maghembe … … Ndiyo
Mhe. Charles J. Mwijage … … … Ndiyo
Mhe. Prof. Joyce L. Ndalichako … … Ndiyo
Mhe. Ummy A. Mwalimu … … … Ndiyo
Mhe. Nape M. Nnauye … … … Ndiyo
Mhe. Eng. Gerson H. Lwenge … … … Ndiyo
Mhe. Selemani S. Jafo … … … … Ndiyo
Mheshimiwa Luhaga J. Mpina… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Abdallah S. Possi... … … …Ndiyo
Mheshimiwa Antony P. Mavunde... … … …Ndiyo
Mheshimiwa William T. Olenasha... … … …Ndiyo
Mheshimiwa Eng. Edwin A. Ngonyani … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji... … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Medard M. Kalemani... … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Susan A. Kolimba... … … …Ndiyo
Mheshimiwa Angeline S. Mabula... … … …Ndiyo
Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani … … …Ndiyo
Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangalla... … …Ndiyo
Mheshimiwa Anastazia J. Wambura... … Hakuwepo
Mheshimiwa Eng. Isack A. Kamwelwe … …Ndiyo
Mheshimiwa Eng. Hamad Yussuf Masauni… … ... Ndiyo
Mheshimiwa Hawa A. Ghasia … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hasna S. Mwilima… … … ... Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mohamed O. Mchengelwa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Balozi Adadi M. Rajab…… … …Ndiyo
Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Peter J. Serukamba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Mary M. Nagu … … …Ndiyo
Mheshimiwa Prof. Norman A. Sigalla… … …Ndiyo
Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika… … …Ndiyo
Mheshimiwa Eng. Atashasta J. Nditiye… … …Ndiyo
Mheshimiwa Vedasto E. Ngombale…… Hakuwepo

Mheshimiwa Doto M. Biteko… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Raphael J. Michael… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Ruth H. Mollel… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Ally Saleh Ally… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Ester A. Bulaya… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Halima J. Mdee…… … Hakuwepo
Mheshimiwa James F. Mbatia … … … Hakuwepo
Mheshimiwa John John Mnyika... … … Hakuwepo
Mheshimiwa Mch. Peter S. Msigwa… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya... … … Hakuwepo
Mheshimiwa Juma Hamad Omar... … … Hakuwepo
Mheshimiwa Godbless J. Lema … … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare... … … Hakuwepo
Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko … … Hakuwepo
Mheshimiwa Antony C. Komu … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Godwin O. Mollel… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Joseph O. Mbilinyi… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Hamidu H. Bobali… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Tundu M. Lissu… … … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Joseph M. Mkundi… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Pauline P. Gekul … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Yussuf K. Makame… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Maftaha A. Nachuma… … Hakuwepo
Mheshimiwa David E. Silinde… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Qambalo W. Qulwi… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa John W. Heche… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali… … Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Immaculate S. Semesi… ... Hakuwepo
Mheshimiwa Mwita M. Waitara… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim… … Hakuwepo
Mheshimiwa Salma M. Mwassa… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Cecilia D. Paresso… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Cecil D. Mwambe… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf… ... Hakuwepo
Mheshimiwa Zubeda H. Sakuru... … … Hakuwepo
Mheshimiwa Devotha M. Minja… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Peter A. Lijualikali… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Abdallah A. Mtolea… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah… … ... Ndiyo
Mheshimiwa Hamida M. Abdallah… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Munde T. Abdallah… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Bahati A. Abeid…… … … Ndiyo

Mheshimiwa Abdul-Aziz M. Abood… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud… … Hakuwepo
Mheshimiwa Khalfan H. Aeshi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Lameck O. Airo… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Ajali R. Akbar… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Stella I. Allex… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Abdallah Haji Ali… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Jamal Kassim Ali… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Khadija Nassir Ali … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Khamis Mtumwa Ali… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Khadija Salum Ally… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Hussein Nassor Amar… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Ussi Salum Amjadi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Saul H. Amon… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Jumaa H. Aweso… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Omary A. Badwel… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar… … …Ndiyo
Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Hussein M. Bashe… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Innocent L. Bashungwa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Mbaraka S. Bawazir… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Kasuku S. Bilago… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Innocent S. Bilakwate… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Halima A. Bulembo… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Jasmine T. Bunga… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Selemani S. Bungara… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Felister A. Bura… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Marwa R. Chacha… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Josephine T. Chagula… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hawa M. Chakoma… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Lathifah H. Chande… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Mary P. Chatanda… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Raphael M. Chegeni… … …Ndiyo
Mheshimiwa Sikudhani Y. Chikambo… … …Ndiyo
Mheshimiwa Abdallah D. Chikota… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Rashid M. Chuachua… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Cosato D. Chumi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mbaraka K. Dau … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. David M. David… … … ... Ndiyo

Mheshimiwa Makame Mashaka Foum… … ... Ndiyo
Mheshimiwa Tauhida C. Gallos… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Leonidas T. Gama… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Alex R. Gashaza… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Josephine J. Genzabuke… … …Ndiyo
Mheshimiwa Boniphace M. Getere… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Anna J. Gidarya… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Seif K. Gulamali… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Haji Ameir Haji… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Miza Bakari Haji… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Mwantum Dau Haji… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Othman Omar Haji… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Khatib Said Haji… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Azza H. Hamad… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Juma Kombo Hamad… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Pascal Y. Haonga… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Japhet N. Hasunga… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Joseph L. Haule…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Juma Othman Hija … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mansoor S. Hiran … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Augustine V. Holle… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Joram I. Hongoli … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Christine G. Ishengoma… … …Ndiyo
Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa…… Hakuwepo
Mheshimiwa Zacharia P. Issaay… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Emmanuel P. John… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Asha Abdullah Juma… … … …

NAIBU SPIKA: Katibu, Mheshimiwa Abdullah Juma.

Mheshimiwa Asha Abdullah Juma… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma… … …Ndiyo
Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Jafar Sanya Jussa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ritta E. Kabati… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Risala S. Kabongo… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Naghenjwa L. Kaboyoka… … Hakuwepo
Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika… … … Hakuwepo
Mheshimiwa John P. Kadutu… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Haji Khatib Kai… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Moshi S. Kakoso… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Joseph G. Kakunda… … … …Ndiyo

Mheshimiwa Bonnah M. Kaluwa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus B. Kamala… …Ndiyo
Mheshimiwa Vicky P. Kamata … … … ... Ndiyo
Mheshimiwa Josephat S. Kandege… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Maria N. Kangoye… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Constantine J. Kanyasu… … …Ndiyo
Mheshimiwa Sebastian S. Kapufi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Katani A. Katani… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Zainab A. Katimba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hassan S. Kaunje… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Dkt. Shukuru J. Kawambwa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Kanali (Mst) Masoud Ali Khamis… …Ndiyo
Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ali Salim Khamis…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis… … …Ndiyo
Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib… … Hakuwepo
Mheshimiwa Munira M. Khatibu… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Aida J. Khenani…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Omari A. Kigoda … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mendrad L. Kigola… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua… … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Pudenciana W. Kikwembe… …Ndiyo
Mheshimiwa Ridhiwani J. Kikwete… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ali Hassan Omar King… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Elibariki E. Kingu…… … … Ndiyo
Mheshimiwa Mariam N. Kisangi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Jumanne K. Kishimba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Jesca D. Kishoa…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Boniventura D. Kiswaga… … …Ndiyo
Mheshimiwa Dunstan L. Kitandula… … … Ndiyo
Mheshimiwa Charles M. Kitwanga … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Allan J. Kiula… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Susan L. Kiwanga… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Grace S. Kiwelu…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Silvestry F. Koka… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Leah J. Komanya… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Yosepher F. Komba… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Kiteto Z. Koshuma… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Saed A. Kubenea… … ... Hakuwepo
Mheshimiwa Zuberi M. Kuchauka… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Rhoda E. Kunchela… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Elias J. Kwandikwa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Julius K. Laizer… … … … Hakuwepo

Mheshimiwa George M. Lubeleje… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Kangi A. Lugola…… … … Ndiyo
Mheshimiwa Riziki S. Lulida… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Anna R. Lupembe… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Livingstone J. Lusinde… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Kemirembe J. Lwota… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hamad S. Maalim… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Amina I. Mabrouk… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Stanslaus S. Mabula… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Elly M. Macha… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Khamis Y. Machano… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Lucy S. Magereli… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Catherine V. Magige… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ester A. Mahawe… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Almas A. Maige…… … …Ndiyo
Mheshimiwa Ezekiel M. Maige… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Kunti Y. Majala… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Salome W. Makamba … … Hakuwepo
Mheshimiwa Makame Kassim Makame… … …Ndiyo
Mheshimiwa Joel M. Makanyaga… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Amina N. Makilagi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu… … …Ndiyo
Mheshimiwa Tunza I. Malapo… … Hakuwepo
Mheshimiwa Angelina A. Malembeka… … …Ndiyo
Mheshimiwa Ignas A. Malocha … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Issa A. Mangungu… … … Ndiyo
Mheshimiwa Vedastus M. Manyinyi… … Hakuwepo
Mheshimiwa Sixtus R. Mapunda … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Agness M. Marwa … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Gimbi D. Masaba … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Hassan E. Masala… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Stephen J. Masele… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Augustino M. Masele… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Susanne P. Maselle… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Yahaya O. Massare… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Flatei G. Massay… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Aisharose N. Matembe … … …Ndiyo
Mheshimiwa Silafu J. Maufi … … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Lucy T. Mayenga … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mussa B. Mbarouk … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Prosper J. Mbena… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Janeth Z. Mbene… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Richard P. Mbogo… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Taska R. Mbogo… … … …Ndiyo

Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Gibson B. Meiseyeki… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Bhagwanji Maganlal Meisuria… … Hakuwepo
Mheshimiwa Subira K. Mgalu… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Neema W. Mgaya… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mahmoud H. Mgimwa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Godfrey W. Mgimwa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Suzana C. Mgonokulima… … Hakuwepo
Mheshimiwa Omary T. Mgumba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Joseph K. Mhagama… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mboni M. Mhita… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Esther L. Midimu…… … … Ndiyo
Mheshimiwa James K. Millya… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Desderius J. Mipata… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Nimrod E. Mkono… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Martha M. Mlata … … … ...Ndiyo
Mheshimiwa Goodluck A. Mlinga… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Lucia M. Mlowe…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Ester M. Mmasi… … … Ndiyo
Mheshimiwa Ally K. Mohamed… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Halima Ali Mohammed… … Hakuwepo
Mheshimiwa Twahir Awesu Mohammed… … Hakuwepo
Mheshimiwa Ibrahim Hassanali Mohammedali… Hakuwepo
Mheshimiwa Amina Saleh Mollel… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Maryam S. Msabaha… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Jacqueline N. Msongozi … … …Ndiyo
Mheshimiwa Martin M. Msuha… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Daniel E. Mtuka… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Maulid Said Mtulia… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed … Hakuwepo
Mheshimiwa Oscar R. Mukasa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Joyce J. Mukya… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Phillipo A. Mulugo… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mary D. Muro… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Benardetha K. Mushashu… … …Ndiyo
Mheshimiwa Mussa Hassan Mussa… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Raisa Abdallah Mussa…… … Hakuwepo
Mheshimiwa Joseph K. Musukuma… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Hawa S. Mwaifunga… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Frank G. Mwakajoka… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Sophia H. Mwakagenda… … Hakuwepo
Mheshimiwa Bupe N. Mwakang'ata… … …Ndiyo

Mheshimiwa Emmanuel A. Mwakasaka… … …Ndiyo
Mheshimiwa Fredy A. Mwakibete… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Edward F. Mwalongo… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa… … …Ndiyo
Mheshimiwa Venance M. Mwamoto… … …Ndiyo
Mheshimiwa Zainabu N. Mwamwindi … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa … … …Ndiyo
Mheshimiwa Savelina S. Mwijage … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Abbas Ali Mwinyi … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mariam D. Mzuzuri … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha … … …Ndiyo
Mheshimiwa Onesmo K. Nangole … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Joshua S. Nassari … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Suleiman M. Nchambi … … Hakuwepo
Mheshimiwa Mashimba M. Ndaki … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Richard M. Ndassa … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Faustine E. Ndugulile … … …Ndiyo
Mheshimiwa Deogratias F. Ngalawa … … …Ndiyo
Mheshimiwa William M. Ngeleja … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Stephen H. Ngonyani … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Oran M. Njeza … … … … Ndiyo
Mheshimiwa Juma S. Nkamia … … … …Ndiyo
Mheshimiwa William D. Nkurua … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko … … ...Ndiyo
Mheshimiwa Musa R. Ntimizi … … … Ndiyo
Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Stanslaus H. Nyongo… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Nassor S. Omar… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Lucy F. Owenya… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Upendo F. Peneza… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Haroon M. Pirmohamed… … …Ndiyo
Mheshimiwa Shally J. Raymond… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Salum M. Rehani… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Conchesta L. Rwamlaza… … Hakuwepo
Mheshimiwa Suleiman A. Saddiq… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Machano Othman Said… … …Ndiyo
Mheshimiwa Saumu H. Sakala… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Mattar A. Salum… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ahmed A. Salum… … … … -
Mheshimiwa Salum K. Salum… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Saada M. Salum… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Deo K. Sanga… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Edwin M. Sannda… … … …Ndiyo

Mheshimiwa Njalu D. Silanga…… … … Ndiyo
Mheshimiwa Joseph R. Selasini… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Oliver D. Semuguruka… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Rashid A. Shangazi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Shabani O. Shekilindi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Juliana D. Shonza… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Mussa R. Sima… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Sophia M. Simba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Margaret S. Sitta… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Joyce B. Sokombi… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Jitu V. Soni… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Rose K. Sukum… … … … Hakuwepo
Mheshimiwa Khalifa S. Suleiman… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Sabreena H. Sungura… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Grace V. Tendega… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Anatropia L. Theonest… … … Hakuwepo
Mheshimiwa Prof. Anna K. Tibaijuka…… … …Ndiyo
Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Fatma H. Toufiq… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Salim H. Turky… … … … …Ndiyo
Mheshimiwa Rose C. Tweve… … … … Ndiyo
Mheshimiwa Abdallah H. Ulega… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Martha J. Umbulla… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Ally S. Ungando…… … … Ndiyo
Mheshimiwa Kassim Ali Vuai… … … … … -
Mheshimiwa Zaynabu M. Vulu… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Selemani J. Zedi… … … …Ndiyo
Mheshimiwa Kabwe R. Zitto… … … … Hakuwepo

NAIBU SPIKA: Katibu hebu rudia jina namba 355.

Mheshimiwa Ahmed Ally Salum … … … …Ndiyo

MBUNGE FULANI: Na Vuai hapo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa kuna Mbunge yeyote ambaye hajapiga kura naona kuna watu…

MBUNGE FULANI: Nipo.

NAIBU SPIKA: Upande upi ambao hujapiga kura?

MHE. KHAMIS ALI VUAI: Nipo umekosea jina.

NAIBU SPIKA: Enhe tutajie jina.

MHE. KHAMIS ALI VUAI: Khamis Ali Vuai.

NAIBU SPIKA: Khamis Vuai ngoja tulitafute. Katibu Namba 386 Mheshimiwa Khamis Ali Vuai. (*Makofi)*

MHE. KHAMIS ALI VUAI… … … …Ndiyo

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vuai subiri kwanza Katibu akuite. (*Kicheko)*

NDG. JOHN N. JOEL - KATIBU MEZANI: Mheshimiwa Khamis Jadi Vuai.

MHE. KHAMIS ALI VUAI: Sio Jadi, Ali Vuai.

Mhe. Khamis Ali Vuai … … … … …Ndiyo

NAIBU SPIKA: Wheshimiwa Wabunge, sasa Katibu atusaidie tumepata kura ngapi za Ndiyo na Hapana na ambao hawakupiga. Waheshimiwa Wabunge wanataka kwenda kuhesabu kura, wanahitaji wawakilishi wawili. Mheshimiwa Nahodha, Mheshimiwa Nahodha umetajwa na Mheshimiwa Mwamoto.

WABUNGE FULANI: Mwamoto, Mipata, Gulamali.

NAIBU SPIKA: Kura za wanawake huku jamani Mheshimiwa Mwanne Mchemba. (*Makofi)*

(Hapa kura zilihesabiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wakati tunamsubiri Katibu na wawakilishi wetu waliokwenda kuhesabu kura, nitoe maelezo kidogo kwa hatua itakayofuata baada ya Katibu kutuletea idadi ya kura. Kwa kuwa tulivyokaa hapa mbele na mimi nilikuwa naweka *tick,* naamini kura za Ndiyo zitakuwa ni nyingi.

Waheshimiwa Wabunge, kama kura za Ndiyo zitakuwa zimeshinda, utaratibu utakaofuata ni wa kupitisha Muswada wa Sheria wa Fedha za Matumizi (*The Appropriation Bill, 2016)*. Sasa tupitie huu utaratibu ili tutakapopewa matokeo ya kura, basi tutaingia moja kwa moja kwenye shughuli inayofuata. Kanuni ya 108 inaelezea utaratibu kuhusu Muswada wa Fedha za Matumizi, kwa sababu tuna dakika chache nitawasomea halafu nitatoa ufafanuzi.

Waheshimiwa Wabunge, 108(1) inasema: "Kabla ya tarehe 30 ya mwezi Juni kwa kila mwaka, baada ya Bunge kukamilisha kazi ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka unaohusika, Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi utawasilishwa Bungeni na kupitishwa mfululizo katika hatua zake zote.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii "*Muswada wa Fedha za Matumizi*" maana yake ni Muswada wa Sheria ya Fedha za Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(3) Muswada wa Fedha za Matumizi hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Kudumu wala Kamati ya Bunge Zima, na masharti kuhusu Miswada Kusomwa Mara ya Kwanza hayatatumika.

(4) Muswada wa Fedha za Matumizi hautatangazwa kwenye *Gazeti* kabla haujawasilishwa Bungeni."

Sasa hili ni Bunge jipya na kwa hivyo tutakuwa tukipitisha hii Sheria ya Matumizi ya Fedha kwa mara ya kwanza. Sasa kwa sababu mmeisikia hii kanuni inasema Muswada huu utapitishwa mfululizo na kwa mujibu wa kanuni hii pia hakuna mjadala kuhusu Muswada huu, hivyo, baadaye tutakapoingia kwenye hiyo hatua tusije tukawa na kutokufahamu kwamba, mbona Muswada huu kila kitu kimepitishwa leo!

Waheshimiwa Wabunge, ndivyo kanuni zetu zinavyosema kwa kuwa tumepitisha bajeti Muswada huu wa Matumizi ya Fedha unapitishwa bila mjadala na unapitishwa hatua zote saa hizi hizi. Kwa hiyo, Mara ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu, vyote vitasomwa hapa hapa tukiwa Bungeni na hakutakuwa na mjadala. Tukishapitisha huo Muswada tutakuwa tumemaliza zoezi la bajeti. Tutaelekea sasa kwenye hatua nyingine ambazo sio za leo, hatua za hapo baadaye za kuangalia ule Muswada wa Fedha (*Finance Bill)*. Ambayo tayari ilishasomwa hapa kwa mara ya kwanza na imeshapelekwa kwenye Kamati husika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, nikasema nitoe haya maelezo kwa maana ya kwamba, tuelewe tu Muswada huu utapitishwa mfululizo, pia hautapelekwa kwenye Kamati yoyote ya Bunge ama hata sisi hapa hatutajadili, lakini kikubwa kingine ni kwamba, hautatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, mtu asije akaanza kuuliza kwa nini Muswada huu hapa tumeupitisha, mbona hakuna mahali umetangazwa, kanuni zetu, Kanuni ya 108 inatoa utaratibu huo na ndiyo tutakaoufuata tukishapata majibu ya kura tulizozipiga mchana huu.

(Hapa kura ziliendelea kuhesabiwa)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Kamati yetu ya kuhesabu imerudi, naomba Katibu atusomee matokeo ya kura.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilete matokeo ya zoezi la kupiga kura kama ifuatavyo:-

Idadi ya Wabunge Kikatiba ni 393, idadi ya Wabunge waliopo kwa sasa ni 389, idadi ya Wabunge mliokuwepo katika Ukumbi huu ni 252. Idadi ya Wabunge ambao hawakuwepo Bungeni wakati wa kupiga kura ni 137, idadi ya Wabunge waliopiga kura na kusema ndiyo ni 251. Kura za hapana ni sifuri, kura za kutokuamua ni sifuri, kura za ndiyo ni 251. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kuna kura moja ya uamuzi, Katibu hakuisoma lakini haina athari. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tuliisoma ile idadi na tulisema hivi, bajeti hii itakuwa imepita ikiwa nusu ya Wabunge 195 ambao ndiyo nusu ya Wabunge wote ambao wako Kikatiba, ambao nusu yao ni 98. Sasa kura alizotusomea Katibu za Ndiyo ni 251, kwa hivyo bajeti imepita kwa kishindo.

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2017 yalipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni. Tutaendelea tena na hayo makofi baadaye. Kwa hiyo, kwa kuwa hakukuwa na kura za Hapana, Wabunge wote waliohudhuria leo wamepiga kura za ndiyo na kwa sababu hiyo nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kutoa hoja ya bajeti Bungeni na Bunge kuipitisha hiyo bajeti. *(Makofi)*

Pia nitoe pongezi za kipekee kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango na niwatakie kila la heri katika hatua zinazofuata. Kama nilivyosema tangu huko mwanzo wakati tukijadili bajeti za Wizara zote, tunawatakia kila la heri na wakati wa kuwasimamia tunaamini tutakuwa tunapiga makofi kama haya, wakati wa kusimamia utekelezaji wenu wa bajeti hii. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunakwenda katika hatua inayofuata. Kama nilivyokuwa tayari nimewasomea utaratibu, sina haja ya kurudia. Kwa hiyo, tunakwenda katika hatua inayofuata, Katibu.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH - KATIBU WA BUNGE: Muswada wa Sheria ya Serikali, kusoma kwa hatua zake zote. Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa mwaka 2016, *(The Appropriation Bill, 2016)*.

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuidhinisha Jumla ya Shilingi 29,539,603,196,184 kwa Matumizi ya Serikali Kutoka Katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Mwaka Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2017, Kutumia Fedha Zilizoidhinishwa kwa Mwaka Huo, Kuruhusu Kuhamisha Baadhi ya Fedha Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Malengo Hayo)

(A Bill for an Act to Apply a Sum of 29,539,603,196,184 out of the Consolidated Fund to the Service of the Year Ending on the 30st of June, 2017 to Appropriate the Sum Granted for that Year to Authorize the Reallocation of Certain Appropriations and to Provide for Matters Connected with Those Purposes)

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

NAIBU SPIKA: Katibu

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2016 *(The Appropriation Bill, 2016)*

(Kusomwa Mara ya Pili)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. NENELWA M. WANKANGA - KATIBU MEZANI:

(Muswada wa Sheria kwa Ajili ya Kuidhinisha Jumla ya Shilingi 29,539,603,196,184 kwa Matumizi ya Serikali Kutoka Katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa Mwaka Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2017, Kutumia Fedha Zilizoidhinishwa kwa Mwaka Huo, Kuruhusu Kuhamisha Baadhi ya Fedha Pamoja na Mambo Yanayohusiana na Malengo Hayo)

(A Bill for an Act to Apply a Sum of 29,539,603,196,184 out of the Consolidated Fund to the Service of the Year Ending on the 30st of June, 2017 to Appropriate the Sum Granted for that Year to Authorize the Reallocation of Certain Appropriations and to Provide for Matters Connected with Those Purposes)

(Kusomwa Mara ya Tatu)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Muswada umeshapitishwa na Bunge na sasa nichukue fursa hii kuitakia Serikali utekelezaji mwema wa sheria hii itakapokuwa imesainiwa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, tumemaliza zoezi letu, bajeti imeshapita na Muswada pia umekwishapita, lakini ninayo matangazo mawili. Tangazo la kwanza…..

MBUNGE FULANI: Mwongozo wa Spika, mwongozo wa Spika.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nikiwa nimesimama hakuna mwongozo, kwa sababu hutakiwi kuongea mimi nikiwa naongea, sasa hapa niko naongea, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tufuate huo utaratibu.

Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Wabunge wa CCM, anawatangazia kwamba mmegawiwa leo Dodoso na nawasihi muondoke nazo hapa na mjaze leo ili kesho asubuhi mzirudishe. Wale watakaokuwa wamemaliza kujaza hapa hapa wanaweza kuzipeleka ofisi namba 231, jengo la Utawala, ghorofa ya pili au kumpatia Mheshimiwa Richard Ndassa au kumpatia Mheshimiwa Joseph Mhagama. Kwa hiyo, mnasisitizwa kwamba hizo Dodoso mlizogawiwa mtoke nazo humu ili msisahau kuzijaza mapema.

Pia Mwenyekiti, Mheshimiwa Richard Ndassa anawakumbusha, pamoja na kwamba nimetoka kusema na yeye ameleta ujumbe hapa kwamba tafadhali msiziache humu ndani hizo Dodoso.

Tangazo la mwisho, linahusu Wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya mechi kati ya Wabunge wa Simba na Yanga itakayochezwa mwezi Julai. Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anawatangazia Wajumbe hao ambao ni Mheshimiwa John Kadutu, Mheshimwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood, Mheshimiwa Turky, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete na Mheshimiwa Zaynabu Vulu kwamba leo hii mara baada ya kuahirisha Bunge, mkutane kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge, anaomba mfike bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.32 Jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 21 Juni, 2016, Saa Tatu Asubuhi)